Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

**Kikao cha Tano - Tarehe 2 Februari, 2009**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):**

Hati ya Matumizi ya Nyongeza Na. 1 ya Mwaka 2008/2009 *(The Supplementary Estimates of Expenditure No. 1 of 2008/2009).*

## MASWALI NA MA JIBU

Na. 54

**Kubadilisha Madaraja ya Mishahara ya Watumishi**

**MHE. MWANAWETU SAIDI ZARAFI** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna watumishi ambao ni wahitimu walioanza kazi na ngazi ya mishahara yao *TGS. III* na sasa wapo *TGS. C* na baadhi yao hustaafu katika daraja hilo na kwa kuwa wahitimu wa Chuo Kikuu huanza kwa mshahara wa *TGS. E* na kwa kuwa watumishi wahitimu hao wa nyuma hawakupandishwa kufikia daraja la *E* la mishahara.

Je, Serikali inasemaje juu ya watumishi wenye utata kama huo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Mwanawetu Said Zarafi, Mbunge wa Viti Maalum, naomba nitoe maelezo machache ya ufafanuzi:-

Mheshimiwa Spika, kwa rejea ya Waraka wa Maendeleo ya Utumishi Namba 6, 12, 19 na 20 ya mwaka 2002 inayohusu kada zilizo chini ya Wizara ya Ardhi, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Nishati na Miundombinu, vianzia vya mishahara ya kada ya wapima ardhi, maafisa mipango miji, wathamini, wanasheria, wajiolojia na wahandisi vianzia vya mishahara yao baada ya kuhitimu chuo kikuu ni *TGS*. E. Aidha, kufuatia mabadiliko ya miundo ya mishahara ya kada ya madaktari ya mwaka 2008, hivi sasa kianzia mshahara wao ni *TGS.* E.

Mheshimiwa Spika, sambamba na maelezo haya utaratibu unaotumika kupandisha cheo mtumishi katika utumishi wa umma kwa hivi ni ule wa kuzingatia utendaji kazi mzuri wa mtumishi kwa kuzingatia vigezo vya upimaji na utendaji kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya machache ya ufafanuzi sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwanawetu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sio kweli kwamba wahitimu wote wa Chuo Kikuu huanzia mishahara wa *TGS. E.* Kianzia mshahara cha *TGS. E* kinatolewa kwa kada chache tu kama nilivyoeleza katika maelezo yangu ya ufafanuzi hapa juu. Wahitimu wengine wa Vyuo Vikuu wanaoajiriwa katika utumishi wa umma vianzia mshahara wao ni *TGS. D* kulingana na Waraka wa Maendeleo ya Utumishi wa kada inayohusika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hakuna utaratibu alioeleza Mheshimiwa Mbunge, naomba kupitia Bunge lako Tukufu kama wapo watumishi wenye matatizo yanayofanana na maelezo ya Mheshimiwa Mbunge, wawasiliane na waajiri wao kwa maandishi na nakala za barua zao ziletwe kwenye ofisi yangu ili matatizo yao yafanyiwe uchambuzi na kutatuliwa.

**MHE. MWANAWETU SAIDI ZARAFI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utaratibu aliosema waliohitimu ni wa *TGS*. E ni kwa kada kama alivyoelezea. Na kwa kuwa swali langu hasa lilikuwa linahusu utumishi wa siku za nyuma ambao ulikuwa kwa mtumishi kila baada ya miaka mitatu hupandishwa cheo kama hana matatizo yoyote. Sizungumzii kuhusu utaratibu uliopo sasa hivi na kwa kuwa wapo watumishi wa aina kama nilivyozungumza na hawajapandishwa cheo na wamefikia hatua ya kustaafu. Mheshimiwa Waziri asaidiaje watumishi hao japokuwa hawakufuata huo mlolongo. Lakini walikuwa katika huo utaratibu wa kila baada ya miaka mitatu kupandishwa na hawakupandishwa na kwa kuwa kipindi hicho ilikuwa watu walikuwa wanapandishwa kwa mkupuo pindi mtu anapopeleka malalamiko na haikuwahi kutokea.

Je, atawasaidiaje watu kama hawa ambao wana matatizo kama hayo wamefikia hatua ya kustaafu lakini mafao yao watapata katika stahili za nyuma ambazo hakustahili kuwa nazo?

**SPIKA:** Majibu kwa swali refu sana hilo. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la watumishi ambao waliajiriwa wakiwa katika *TGS III* wakati tunabadilisha miundo badala ya *TGS III* na kwenda *TGS. E, A, O* au *B* kufuatana na kada au nafasi ya mtumishi watumishi wote walihamishiwa kulingana na nafasi zao.

Kwa wale ambao walikuwa wamemaliza tu chuo kikuu na ambao walipaswa kwenda *TGS. E* walihamishiwa *TGS*. E na wale ambao walistahili kwenda katika *TGS*. D walipelekwa *TGS*. D na wale ambao walikaa muda mrefu bila kupandishwa cheo tuliwaagiza waajiri wote kuwarekebishia mishahara yao kabla utaratibu wa upimaji upya wa watumishi haujaanza. Zoezi hilo limefanyika na katika kipindi cha mwaka 2006/2007/2008. Ofisi yangu imelishughulikia suala hilo la kuondoa kero kwa wale watumishi ambao walikuwa hawajarekebishiwa mishahara yao kulingana na miundo. Lakini kama wapo ambao Mheshimiwa Zarafi anao ushahidi kwamba bado hawajarekebishiwa naomba anileteee. Kuhusu suala la waliostaafu kwa kweli hatuna utaratibu wa kumshughulikia mtumishi aliyestaafu kumrekebishia mishahara yake. Hata tunapokokotoa mafao ya mtumishi wakati wa kustaafu tunaangalia kile cheo ambacho amekaa nacho kwa kipindi kinachotimia miezi 6.

Kwa hiyo, kama utapandishwa cheo leo na kesho yake ukastaafu hatutakokotoa mshahara kwa cheo ambacho umekipata leo. Ahsante sana.

Na. 55

**Upimaji wa Safi za Watendaji wa Serikali**

**MHE. MUSSA AZZAN ZUNGU** aliuliza:-

Kwa kuwa mipango mingi mizuri ya Serikali huwa inashindwa kutekelezwa ama kutokana na sababu kuwa baadhi ya watendaji wake hawana sifa wanazodai kuwa nazo:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kupima upya sifa za watendaji wake na taaluma zao ili mipango yake iwafikie wananchi kwa haraka na kwa ufanisi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala, ninapenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, watumishi wa Serikali huajiriwa na kuendelea kubaki katika utumishi wa umma kwa kuzingatia sifa za kielimu, taaluma, uwezo na uzoefu kama ilivyoainishwa katika miundombinu ya utumishi *(scheme of services)* ya kada mbalimbali Serikalini. Aidha, mchakato mzima wa kuajiri hufanywa kwa umakini mkubwa ikiwa ni pamoja na kuhakiki sifa ambazo zinahitajika kwa nafasi husika.

Mheshimiwa Spika, miundo ya utumishi Serikalini hupitiwa kila mara inapotokea umuhimu wa kufanya hivyo na kuhuishwa ili kukidhi sifa na mahitaji ya kazi kwa wakati husika. Aidha, kila mwaka watumishi wa Serikali hupimwa utendaji kazi kwa kuzingatia sifa zao na malengo waliojiwekea.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia sera ya menejimenti na ajira ya mwaka 1998, ilikwishaona umuhimu wa kupima sifa za watendaji wake na taaluma zao ili mipango yake iwafikie wananchi kwa haraka na kwa ufanisi.

**MHE. MUSSA AZZAN ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali inasema kutoka mwaka 1998 imeanza kupima sifa za watendaji wake.

(a) Je, kwa kipindi hiki cha miaka 10 toka imeanza kupima imegundua nini?

(b) Kwa kuwa bado kuna watalaam wengi wana sifa zao lakini hawana mapenzi ya kufanyakazi hizi. Je, Serikali inachukua hatua ipi kwa watendaji kama hawa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema ni kweli Serikali imeanza kupima watumishi wake kwa utaratibu ambao tumeuweka ambao tunautumia sasa hivi tangu mwaka 1998 na katika kupima yafuatayo tumeyagundua. Wapo watumishi ambao kwa kweli tumewaona wana utendaji mzuri na wanamudu nafasi zao ambazo wamepewa. Kutokana na hivyo basi baadhi yao na wengi wao tumewapandisha vyeo na pia tumewapa motisha mbalimbali ili waweze kufanyakazi kwa ufanisi. Lakini pia wapo wachache wao ambao tumewagundua wamekuwa na udhaifu katika utendaji wao wa kazi na hivyo baadhi yao wamekaa muda mrefu bila kupandishwa vyeo na baadhi yao tumewapunguzia madaraka kwa kuwa tumewaona wameshindwa kumudu kazi walizopewa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili sikulipata vizuri ningeomba Mheshimiwa Mbunge alirejee.

**SPIKA:** Tafadhali Mheshimiwa Zungu rejea swali la nyongeza la pili.

**MHE. MUSSA AZZAN ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, nimelifuta. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Lakini hapo hapo amesimama jirani yako wa Jimbo la Kinondoni.

**MHE. IDD M. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wapo watendaji ambao wana sifa na taaluma inayostahili lakini ama kwa uzembe ama kwa makusudi wamekuwa

wakitumia madaraka ama fedha za miradi mbalimbali kwa ubadhirifu mkubwa hasa katika Halmashauri; na kwa kuwa Serikali mara nyingi imekuwa ikiwahamisha kutoka Halmashauri moja kwenda Halmashauri nyingine pamoja na ubadhirifu waliofanya.

Je, ni lini sasa Serikali itakuwa tayari kuwachukulia hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kuwafukuza kazi watendaji wabovu wa namna hii? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge amesema kwamba wapo watumishi ambao wamebainika kufanyakazi kwa uzembe na pia kufanya ubadhirifu katika maeneo mbalimbali na kwamba Serikali imekuwa ikiwahamisha kutoka eneo moja hadi eneo jingine. Ni kweli tumekuwa tukipata malalamiko kutoka katika maeneo mbalimbali kuhusu watumishi.

Lakini tunapokuwa tukiwafuatilia ili tupate uhakika wa kuweza kuwachukulia hatua zinazostahili mara nyingi tumekuwa hatupati ushirikiano katika maeneo wanayofanyia kazi, badala yake unasikia mara nyingi wakidai tu wakiomba tuwahamishe. Hata katika ziara zangu maeneo mengi tumekuwa tukiwaambia kwamba sasa hivi Serikali imeshatoa hayo madaraka kwa mamlaka za ajira kuweza kuwachukulia watumishi hatua pale pale walipo badala ya kuwahamisha.

Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge kwa sababu wote sisi ni Madiwani katika Halmashauri zetu. Tunapowaona watendaji ambao ni wabadhirifu naomba tuwachukulie hatua wakiwa pale pale badala ya kusubiri wahamishwe halafu tulalamike wakiwa wameondoka.

Uwezo huo mnao wa kuwachukulia hatua. Kwa hiyo, suala la kwamba mtumishi alioko kwenye Halmashauri atachukuliwa hatua na Ofisi ya Rais, Majenementi ya Utumishi wa Umma au TAMISEMI halipo. Madaraka hayo yako kwenu ninyi. *(Makofi)*

Lakini maeneo mengi unakuta kuna mivutano unapotafuta ushahidi wa kuweza kumchukulia mtumishi hatua zinazostahili hupati. Kwa hiyo, huwa tunawahamisha kuwapeleka maeneo mengine tukawaangalie. Je, kutakuwa na malalamiko kama yale ambayo yametolewa katika Halmashauri nyingine au kulikuwa na tofauti ambazo labda zinashindwa kuelezwa na sisi tukaweza tukichukulia hatua.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Kweli umebobea katika masuala ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Majibu mazuri sana. *(Makofi)*

Na. 56

**Mpango wa Kuleta Dawa za Kuua Wadudu wa Malaria**

**MHE. JANETH M. MASSABURI** aliuliza:-

Kwa kuwa, kinamama wengi wa watoto wa Dar es Salaam hupata tabu sana ya kutafuta tiba ya magonjwa ya malaria, na wakati mwingine kipindupindu; na kwa kuwa, hali hiyo huwaathiri wanawake kutoshiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo:-

(a) Je, Serikali ipo tayari kuwa na mpango kabambe wa kusaidia Mkoa wa Dar es Salaam kwa kuleta dawa za kupulizia wadudu wa Malaria kama jinsi ilivyofanyika Zanzibar?

(b) Je, Serikali haioni kwa kuzuia magonjwa kama hayo kutapunguza mzigo wa fedha za madawa na Tiba?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Maurice Massaburi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara imeandaa mpango kabambe (*master plan*) wa upuliziaji wa dawa za ukoko majumbani katika Wilaya 60 zilizo katika hatari ya milipuko ya malaria na zile zenye maambukizi kwa kipindi kirefu cha mwaka (epidemia- *prone and endemic*). Mpango huu utatekelezwa katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2008 – 2012.

Katika mwaka huu wa fedha, mpango wa upuliziaji umepangwa kutekelezwa katika Wilaya zote za Mkoa wa Kagera na Wilaya za Mafia na Mkuranga katika Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Wilaya za Mkoa wa Dar es Salaam hazipo katika mpango kabambe wa Wilaya 60 za upuliziaji wa dawa za ukoko majumbani ili kudhibiti malaria.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa tu, Dar es Salaam ndiyo Mkoa pekee unaotekeleza mpango wa unyunyiziaji wa viuatilifu katika mazalia ya mbu (l*arviciding*) katika kata mbalimbali za Wilaya ya zote tatu. Mpango huu ukisimamiwa kikamilifu unaweza kupunguza tatizo la malaria kwa kiwango kikubwa.

Natoa wito kwa Halmashauri na Mganga Mkuu wa Jiji akishirikiana na Mbunge ili wasimamie zoezi hili kwa sababu matokeo yake yatakuwa mazuri kama tutasimamia vizuri.

Mheshimiwa Spika, sote hapa ukumbini tunajua mbu wanazaliana katika mazingira ya namna gani. Ni katika maji yanayotuama kama madimbwi, vifuu vya nazi, hata katika magereji na nyenzo muhimu ambayo tungependa kuisambaza kwa wenzetu ambao hawajui ili waelewe kwamba tukiweza kutowaruhusu mbu kuzaliana hakutakuwa na haja ya kupuliza, hakutakuwa na haja ya dawa ya vyandarua au kutumia dawa ya *ALU* vyombo ambavyo ni gharama kubwa.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa kwa kuzuia magonjwa kama hayo si tu kutawafanya wananchi wawe na afya bora kwani hawataugua mara kwa mara, lakini pia kutaipunguzia Serikali mzigo wa gharama za dawa na tiba. Ni kwa kulitambua hilo ndiyo sababu siku zote kipaumbele na msisitizo katika shughuli za Wizara ya Afya unawekwa kwenye huduma za kinga. Kinga ni bora kuliko tiba. Vilevile kinga ni gharama nafuu kuliko tiba.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri ingawaje sikuridhika. Kwa kuwa, Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam uwezo wake wa mapato ni mdogo na ukizingatia Mkoa wa Dar es Salaam una wakazi wanaokaribia milioni tano (5).

Je, Serikali haikuona umuhimu wa kuupa Mkoa wa Dar es Salaam upendeleo ikizingatia idadi hiyo ya wakazi ili uweze kuzuia hayo maradhi ambayo yanaukabili Mkoa mara kwa mara na pia mlipuko wa mara kwa mara wa ugonjwa wa kipindu pindu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Janeth Massaburi kwamba Jiji la Dar es Salaam lina wakazi wengi karibu milioni 4, lakini nilivyokuwa najibu swali lake la msingi nimeeleza kwamba tulitumia vigezo vya kitaalam kuangalia maeneo ambako kuna maambukizi mengi ya malaria na tukaona tulenge kwanza Wilaya hizo 60, na kwa vigezo tulivyoweka kusema kweli Wilaya za Manispaa za Dar es Salaam hazikukidhi vigezo hivyo.

Lakini hata hivyo, nilisema tutaanzia na Wilaya 60 sikusema kwamba Dare es Salaam itaachwa. Lakini ameingiza suala la kipindupindu ambalo siyo la msingi kuna mikakati tofauti na kama atapenda tunaweza tukaleta jibu ambalo litalenga kipindu pindu hapo baadaye katika utaratibu wa kawaida.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wawili, Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vulu na Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya.

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na kueleza kwamba Mkoa wa Pwani kuna baadhi ya Wilaya zitafanyiwa zoezi la upuliziaji wa dawa. Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba Mkoa wa Pwani kuna baadhi ya maeneo wanaathirika zaidi na magonjwa ya malaria, matende na ngiri maji, zoezi hilo litafika lini katika maeneo mengine ambayo hayakupangiwa kwa hivi sasa ili kuweza kuokoa maisha ya wananchi hao waweze kushiriki vizuri katika masuala mbalimbali ya kazi na kilimo?

**SPIKA:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Waziri wa Afya.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mkoa wa Pwani kuna maambukizi ya matende, malaria, na mabusha, na kwa upande wa malaria ndiyo maana tukachagua Wilaya mbili kama nilivyosema Mkuranga

na Pwani kwa kutambua hilo. Na Mpango wa kudhibiti ngiri maji ni ambao unafanya kazi kwa bidii sana katika Mkoa Pwani. Sasa kama anataka tupe ratiba hiyo tunaweza tukaishughulikia na tukampa. Lakini kazi kubwa katika upande wa ngiri maji na matende inafanyika katika Mkoa wa Pwani na wamependelewa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, swali la nyongeza la mwisho.

**MHE. MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nimefurahi sana Waziri amejibu kwamba jambo muhimu ingekuwa ni kuzuia maeneo ambayo mbu wanazaliana. Sasa swali langu ni kwamba kwa kuwa, vyandarua na madawa yanayotumiwa ni ya ghali. Je, Serikali ingekubaliana nasi kwamba inatakiwa ianzishe *operation* maalum ya kuua mbu maeneo yote ambayo ndiyo mwanzo wa mazalia ya mbu?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Mzindakaya amekubaliana na mimi kwamba kuzuia ni bora kuliko kutibu na ni gharama nafuu. Nilivyosema ni kwamba kutumia dawa za ukoko za kupulizia katika majumba pamoja na kusafisha mifereji ni baadhi ya nyenzo za kuzuia. Sasa huo mpango kabambe niliouzungumza unalenga hilo kwamba tuone kinyaa kuona maji yanatuama mahali kwa sababu hapo una *encourage* mbu kuanza kuzaliana tukiweza kufanya hivyo hatakuwa na haja ya kupulizia. Hakutakuwa na haja ya vyandarua wala dawa ya ghali kama ya *ALU*.

Na. 57

**Kujenga Mahakama Kuu Mkoani Singida**

**MHE. MARTHA M. MLATA (K.n.y. MHE. DIANA M. CHILOLO)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imeahidi kujenga Mahakama Kuu Mkoani Singida kwa Bajeti ya mwaka 2008/2009 na kwamba Uongozi wa Mkoa umeanza taratibu za ujenzi huo:-

Je, Serikali itatuma lini fedha kwa ajili ya ujenzi huo ili kuunga mkono juhudi za Uongozi wa Mkoa kwani tayari wamekwishajiandaa?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Diana Chilolo, kama ifuatavyo:-

Kutokana na kuchelewa kupitishwa kwa mpango kazi wa mwaka 2008/2009 na wafadhili uliokuwa unahusu ujenzi wa Mahakama Kuu Mikoa ya Mara na Mtwara miradi hiyo ambayo ilitegemewa kukamilishwa ili tuanze mradi mpya wa ujenzi wa Mahakama Kuu Mkoa wa Singida, imelazimika kuendelea na miradi hiyo kwanza

ambayo haijakamilika katika mwaka huu wa fedha. Vilevile kutokana na ufinyu wa Bajeti ya Maendeleo ambayo tuliyopewa kwa ajili mradi wa Mahakama Kuu Mkoa wa Singida kwa mwaka 2008/2009. Serikali imeshindwa kuanza mradi wa ujenzi wa majengo ya Mahakama Kuu Mkoani Singida ni kama tulivyoahidi.

Hata hivyo, tunaomba uongozi wa Mkoa uendelee na juhudi zake wakati Serikali inaangalia uwezekano wa kupata fedha kwa ajili ya kazi hiyo.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya kukatisha tama wananchi wa Mkoa wa Singida ya Mheshimiwa Waziri, ningependa nimwulize swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa yeye mwenyewe amekiri kwamba kwa kuchelewa kwa miradi miwili ambayo wao walikuwa wameipangia katika Mikoa aliyoitaja na kwa kuwa ni Serikali hiyo hiyo ambayo iliahidi kupeleka fedha katika Mkoa wa Singida na hali ikijua kwamba ina ujenzi mwingine. Sasa je, Mheshimiwa Waziri atawahakikishiaje wananchi wa Mkoa wa Singida pamoja na juhudi zote ambazo wamezifanya wakisubiri ahadi yao kwamba itawapa kipaumbele katika mwaka huu wa fedha utakaoanza? Ahsante.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ina nia madhubuti kabisa na nataka Mheshimiwa Mbunge, akubaliane na mimi kwamba tuna nia madhubuti kabisa ya kujenga Mahakama Kuu Mkoa Singida. Lakini katika mipango yetu tulidhani tungemaliza kwanza ile ya Mara na Mtwara kishwa twende Singida. Fedha tulizokuwa tunategemea kujengea nyingi zilikuwa zinatoka kwa wafadhili. Kwa bahati mbaya wafadhili kutokana na matatizo yao wamechelewa kabisa kutupa fedha zile za Mara na Mtwara. Lakini tuna hakika tuko katika hatua za mwisho za kukamilisha za kukubaliana nao ili watupe fedha za Mara na Mtwara. Baada ya hapo tunataka kuwahakikishia kwamba tutajenga Mahakama ya Singida na naomba wananchi wa Singida waendelee na utaratibu wa maandalizi ya ujenzi huo. (*Makofi*)

**MHE. FAIDA M. BAKARI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mbali na ujenzi wa Mahakama Kuu ya Mkoa wa Singida, lakini kuna mahakama nyingi hapa nchini petu ambazo ni mbovu na zinahitaji kufanyiwa ukarabati. Je, Serikali ina mpango gani wa kuzifanyia ukarabati mahakama zake ambazo ni mbovu? Ahsante sana.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na yeye kwamba tunazo mahakama nyingi sana katika nchi yetu ambazo hali ya majengo yake hairidhishi. Kutokana na hiyo, tuna mipango miwili ambayo tunaitekeleza kwa sasa.

Mpango wa kwanza uko chini ya mradi wa kuboresha sekta ya Serikali *(Legal Reform Program)* mpango wa pili ni mradi endelevu chini ya mahakama ambayo yote miwili kazi yake kubwa ni kurekebisha, kukarabati mahakama zile mbovu na kujenga mahakama mpya hasa mahakama za Mwanzo na za Wilaya. Chini ya mipango hii miwili tunatarajia kwamba tutaweza kukamilisha Mahakama zote 1056 ambazo zinahitaji ukarabati na nyingine zinahitaji kujengwa upya.

Na. 58

**Uharibifu wa Mazao Kandokando ya Hifadhi**

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH** aliuliza:-

Kwa kuwa, kumekuwepo na matukio ya uharibifu wa mazao ya wananchi wa Wilaya ya Pangani katika Vijiji vinavyopakana na hifadhi ya Taifa ya Saadani; na kwa kuwa, orodha ya wananchi waliopatwa na maafa hayo inajulikana:-

(a) Je, ni lini wananchi hao watalipwa kifuta machozi kwa mazao yao kuharibiwa?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani kudhibiti uharibifu huu unaozidi kuendelea kila siku?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, matukio mengi ya uharibifu wa mali za wananchi yanayosababishwa na wanyamapori, yanatokana na ongezeko la idadi ya watu na shughuli zao, ikiwa ni pamoja na makazi, kilimo na ufugaji katika maeneo yenye wanyamapori. Hali hii imesababisha ongezeko la matukio ya mazao ya wananchi kuharibiwa na wanyamapori. Kutokana na hali hiyo, mwaka 2006 Wizara yangu iliweka utaratibu wa kulipa kifuta jasho kwa wananchi ambao mazao yao yameharibiwa na wanyamapori. Kwa kuzingatia kwamba utaratibu huu ulikuwa haujawekwa kwenye Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori Sura Na. 283, ulipaji wa kifuta jasho umekuwa unachukua muda mrefu kuliko wananchi walivyotarajia kwani unafanyika tu baada ya kukamilika kwa kazi ya kuhakiki na kutathmini athari za uharibifu uliofanywa na wanyamapori hao. Kwa kutambua upungufu huu, suala hili limewekewa mwongozo kwenye muswada wa sheria mpya ya wanyamapori inayoendelea kujadiliwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, katika kuzingatia hayo, mnamo mwezi Aprili, 2008 Wizara yangu ilipata taarifa kuhusu uharibifu uliotokana na Tembo katika baadhi ya vijiji vya Wilaya ya Pangani. Kufuatia taarifa hiyo, wataalamu wa Wizara yangu walifuatilia tatizo hilo kwa ajili ya kufanya tathmini ya uharibifu wa mazao. Taarifa ya tathmini iliyotolewa ilibaini upungufu mkubwa ikiwa ni pamoja na majina ya wahanga kurudiwa, baadhi yao kutoorodheshwa na athari za uharibifu kwa baadhi ya wahanga kutoweza kuthibitika.

Katika kuzingatia hali hiyo, Wizara yangu imelazimika kuhitaji muda zaidi wa kuhakiki uharibifu uliofanyika. Kazi ya uhakiki inayoendelea hivi sasa na hatimaye kulipa kifuta machozi inatarajiwa kukamilika mwezi wa tatu mwaka huu.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Pangani itaendelea kufanya doria za msako wa wanyama wakali na waharibifu wa mazao kama njia ya kupunguza tatizo lililopo. Aidha, katika rasimu ya muswada wa uhifadhi wa wanyamapori unaoendelea kujadiliwa na Bunge lako Tukufu, Serikali imependekeza kutengwa kwa maeneo ya mapito ya wanyama yaani *corridors,* maeneo yanayozunguka hifadhi yaani *buffer zones* na maeneo ya mtawanyiko wa wanyamapori yaani *dispersal areas* ili kupunguza mogogoro kati ya wanyama na wananchi na mali zao. Wizara yangu itaendelea kushirikiana kwa karibu na Halmashauri pamoja na wananchi wa Pangani ili kuona uwezekano wa kuanzisha maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori yaani *WMA*, ambazo zitatoa mchango mkubwa katika kushirikisha wananchi kudhibiti wanyama waharibifu.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu maziri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu yake ya kusema kwamba uharibifu huu wa mazao unaongezeka kwasababu ya kuongezeka shughuli za binadamu katika maeneo yale lakini akiri vilevile kwamba na idadi ya tembo imezidi. *(Makofi).*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri; Kwa kuwa, sasahivi umeshapita muda wa zaidi ya miaka mitano na tembo wanaendelea kuharibu mazao ya wananchi. Pamoja na kwamba mwaka 2009....

**SPIKA:** Mheshimiwa Rished, hilo neno linawakera wenzako, mnyama huyo ana jina lingine la kistaarabu zaidi, hivyo litumie. *(Makofi/Kicheko).*

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, asante badala ya neno nililolisema la jina la mnyama huyu basi iwe ndovu. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, unalihakikishia Bunge hili kwamba itakapofika Machi, wananchi hawa watalipwa fidia zao? Hilo la kwanza. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, la pili ni tatizo hili linajitokeza kwasababu tukiri vilevile kuna matatizo ya doria kwa maana ya vifaa kama magari na askari wa kutosha kufanya hii kazi, lakini naona Mheshimiwa Waziri, hakuligusia hilo na hilo ni uhakika kabisa; Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha kwamba sasa tunaongeza askari na doria ziongezeke ili kudhibiti mpaka hapo watakapopata ufumbuzi wa kudumu juu ya suala hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimshukuru Mheshimiwa Rished kwa kulizungumzia suala hili na kwa kweli limekuwa ni miongoni mwa mambo ambayo amekuwa akifuatilia kila mara Wizarani kwetu.

Niseme kwamba kama ambavyo wananchi wamesubiri kwa muda mrefu ni kweli hata sisi pale Wizarani suala hili tumechoka kulisikia masikioni, kwa maana hiyo hii dhamira tuliyoisema kwamba ifikapo Machi tutakuwa tumekamilisha na kulipa ni dhamira ya kweli. Kitakachoweza kukwamisha jambo hili ni kitu ambacho kiko nje ya uwezo wa kibinadamu, kwahivyo matumaini yetu ni kwamba jambo hili litakamilika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matatizo ya doria. Tatizo la kutokuwa na vifaa na askari wakutosha ni kubwa na katika muswada wa sheria ambao tunaendelea kujadili tumedhamiria kufanya mabadiliko makubwa sana kwenye sekta nzima ya Idara ya Wanyamapori kwa maana ya kwamba tunategemea kuanzisha kikosi kama ambavyo muswada umependekeza. Kikosi hiki kitakuwa na uwezo wa kufanya kazi kama *paramilitary unit* lakini pia katika muswada huohuo tumependekeza kuanzisha Mamlaka ya wanyamapori. Tunafikiri kuanzishwa kwa Mamlaka hii kutaiwezesha kuwa na maamuzi ya haraka ya kuweza ku-*empower* wafanyakazi wake na hata kuboresha vitendea kazi.

Kwa hiyo, tunafikiri baada ya muswada kupita, utendaji kazi utakuwa ni mzuri na matatizo ambayo yapo sasa yatapungua kwa kiasi kikubwa.

**SPIKA:** Asante, sijamuona Mheshimiwa Mudhihir, siku nyingi sana. Mheshimiwa Mudhihir, swali la nyongeza na hongera sana kwa ushindi mkubwa sana wa timu ya Yanga. *(Makofi/Kicheko).*

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa, katika majibu ya swali la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri, amesema uharibifu wa mazao ya wakulima unatokana na kuongezeka kwa shughuli za binadamu wanaokaa kandokando ya Hifadhi. Na kwa kuwa, Jimbo la Mchinga halipo kandokando ya Hifadhi ya Wanyamapori lakini ndovu bado wanashambulia mazao. Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba tatizo hili chanzo chake ni kuhifadhiwa kwa wanyamapori hao, ndovu, kuliko kuhifadhiwa kwa mazao ya wakulima?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir, Mbunge wa Mchinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sababu zinazosababisha kuongezeka kwa migongano hii kati ya wanyama na binadamu ni nyingi. Ongezeko la idadi ya wanyama ndovu, inaweza ikawa ni moja ya sababu lakini pia *disturbances* zinazofanyika kwenye maeneo yaliyohifadhiwa inaweza ikawa ni sababu. Kwa maana ya kwamba binadamu anapokwenda kwenye eneo lililohifadhiwa kukata mbao au kufanya shughuli nyingine kwa mfano ujangili. Kunawafanya wanyama hawa watoke kwenye maeneo hayo ambayo wangekuwa hawajawa *disturbed* isingekuwa hivyo.

Lakini ili kujua sababu halisi na nini cha kufanyika, tumewaelekeza wenzetu wa taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori *(TAWIRI)* waweze kutupa takwimu halisi ya idadi ya ndovu waliopo na ni nini hasa ambacho tunaweza tukafanya kwa kuzingatia mtawanyiko wa wanyama hawa kwenye baadhi ya maeneo ambayo mengine yana wanyama wengi zaidi na mengine si wengi. Lakini mambo ambayo tumeyapendekeza kwenye muswada wa sheria nayo pia yanakusudia kupunguza tatizo hili. Kwa hiyo, nafikiri baada ya utafiti huo kukamilika tutaweza kupata jibu sahihi na mkakati mzuri zaidi utaweza kuwekwa.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa, suala la fidia kuhusiana na mazao yanayoharibiwa na wanyama pamoja na maisha ya wananchi yanavyoathirika kutokana na wanyama hao limeonyesha kwamba sio endelevu, haliwezi kutekelezeka. Kwa nini Wizara isiandae au ku-*commission* utafiti wa kina wa kutafuta njia mbadala ya kushughulikia suala hilo ikiwa ni pamoja na kuanzisha, k wa mfano, mfuko wa bima kwa ajili ya maeneo au vijiji ambako wanyama hao wanapatikana au yanazungukwa au yako karibu na uhifadhi wa wanyamapaori. Ni kwanini usianzishwe mfuko kama huo kwa mfano?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mbunge wa Ludewa, kwa kifupi kwanza kwa kumshukuru kwamba swali hili mimi nalichukulia kama ni ushauri ambao kwa kweli hakuna haja ya kubishana au kusita kuupokea. Ni ushauri mzuri, tutautafakari kwa kuangalia hasa ni gharama kiasi gani inaweza ikahitajika kwa ajili ya kufanya *study*. Lakini kimsingi suala la kufanya utafiti kupata njia ya uhakika na endelevu ya kukabiliana na matatizo ya fidia na kifuta machozi ni wazo la msingi; nikiri kwamba tumelipokea tutalifanyia kazi. *(Makofi).*

Na. 59

**Ufugaji wa Nyuki Mkoani Rukwa**

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA** aliuliza:-

Kwa kuwa, ufugaji wa nyuki Mkoani Rukwa unawaingizia kipato kizuri wananchi wa Mkoa huo; na Kwa kuwa, bado Serikali haijaweza kuhamasisha wananchi kuzingatia ufugaji wa kisasa ili kupata mazao bora ya Nyuki:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuelimisha wananchi na kusambaza mizinga ya kisasa ili kuongeza kipato cha wananchi hao?

(b)Je, wananchi wa Tatanda, Kaluko, Katete na Kasesya watasadiwa vipi ili nyuki wanaokaa katika nguzo za umeme zenye nafasi ndani wahame katika nguzo hizo na wahamie katika mizinga?

(c) Je, Serikali inatoa fidia gani kwa wananchi hao kukosa asali kwa kuwa nyuki huweka makao yao zaidi kwenye nguzo za umeme badala ya kukaa kwenye mizinga?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mbunge wa Kalambo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inahamasisha wananchi kufuga nyuki kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kusambaza vipeperushi, kutoa vipindi vya kuhamasisha kwa njia ya radio, kutoa huduma za ugani kutoka kwa wataalamu walioko katika kanda saba za huduma ya ugani na maafisa nyuki walioko katika Halmashauri za Wilaya.

Aidha Wizara inayo mashamba manne ya mfano ya kufugia nyuki katika Wilaya za Kibondo Mkoani Kigoma, Handeni Mkoani Tanga, Kondoa Mkoani Dodoma na Manyoni Mkoani Singida. Pamoja na shughuli za uzalishaji, mashamba haya hutumiwa kwa mafunzo kwa wafugaji wa nyuki kutoka sehemu mbalimbali wanaotembelea mashamba haya.

Aidha Wizara ina mkakati maalum wa kuendeleza shughuli za ufugaji nyuki katika wilaya zote nchini zenye fursa ya rasilimali ya ufugaji nyuki. Kwa sasa Wizara imeanza na Wilaya thelathini na shughuli zilizofanywa kwenye wilaya hizi ni kuainisha vijiji na maeneo ambayo yanafaa kwa shughuli za ufugaji nyuki, kuanzisha vikundi vya ushirika vya wafugaji nyuki na kutoa vifaa vya kisasa na kutoa mafunzo kwenye vikundi hivyo. Mpaka sasa jumla ya Mizinga 1,200 imesambazwa kwa wananchi na Serikali inaendelea kuhamasisha wananchi kuendelea kununua na kutumia mizinga ya kisasa.

(b) Mheshimiwa Spika, kazi ya kuhamisha makundi ya nyuki yaliyoko kwenye nguzo za umeme kwenda kwenye mizinga hufanywa kitaalamu na maafisa nyuki endapo nyuki hao wanahamishika. Wizara yangu imeshafanya mawasiliano na Sekretarieti ya Mkoa wa Rukwa kutembelea vijiji vilivyotajwa na Mheshimiwa Mbunge, ili kuangalia uwezekano wa kuwahamisha nyuki hao kutoka kwenye nguzo za umeme kwenda kwenye mizinga. *(Makofi)*

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali haina utaratibu wa kutoa fidia kwa wananchi kwa sababu ya nyuki kutokuingia kwenye mizinga. Kwani nyuki kama viumbe wengine wana mahitaji muhimu kama chakula, maji, kivuli na mahali pasipokuwa na usumbufu. Kundi la nyuki kukaa katika nguzo za umeme ni kiashiria cha kuharibiwa kwa mazingira yao ya asili. Hivyo, napenda kuchukua fursa hii kutoa wito kwa wananchi, kutunza mazingira kwa ajili ya uhifadhi wa viumbe mbalimbali wakiwemo nyuki.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata majibu kama haya kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini naomba nimthibitishie kwamba pamoja na majibu aliyoyatoa sijawahi kuona juhudi zozote za kupeleka vipeperushi na mafunzo katika Wilaya yangu ya Sumbawanga. Na pia kwasababu hata Redio Tanzania tumeilalamikia kwa muda mrefu kwamba haisikiki

katika Mkoa wa Rukwa hivyo wananchi wala hawapati taarifa hizo anazosema zinatumika kupelekwa kwa njia ya redio.

Lakini kwa kuwa, Wilaya ya Sumbawanga na Wilaya ya Nkasi, hali yake ya mazingira ya misitu ni sawasawa kabisa na wilaya ya Mpanda, Wilaya ya Manyoni na Wilaya nyingine zote, lakini Maofisa Maliasili wanaohusika na Nyuki hawajawahi kufanya kazi yoyote ya maana kuwasaidia wananchi katika vijiji kama vile vya Kisumba, Pombwe, Kasitu, Katete, Mkowe, Mbozi na Mwimbi ili waweze kuleta mapinduzi na kuleta utaalamu mpya wa ufugaji nyuki katika nchi. Ni lini Wizara hii itachukua juhudi za kuhakikisha Wilaya yetu ya Sumbawanga na hususan Jimbo la Kalambo, tunapata Wataalamu watakaoeneza utaalamu huu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa, Mheshimiwa naibu Waziri ana...

**SPIKA:** Liwe fupi, manaake hilo la kwanza ni refu mno.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, ili wananchi waweze kusikia. Kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri, amezungumza habari ya kuhamisha nyuki kutoka kwenye nguzo lakini bila kuziba matundu ya nguzo hizi itakuwa ni vigumu kwasababu watarudia tena.

Je, kwanini asiwasiliane na watu wa Nishati na Madini ili kazi hii iweze kufanyika? Na badala ya kutoa fidia watu wa umeme waweze kutuwekea umeme katika vijiji vyetu? *(Kicheko).*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwananzila, ambayo ukiainisha unakuta ni matatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza amezungumzia suala la vipeperushi; vipeperushi tumesema tumesambaza kwenye wilaya wilaya thelathini. Ni kweli katika mkoa wa Rukwa, tumepeleka kwenye Wilaya ya Mpanda pekee ambayo ndio inaongoza kwa kuwa na fursa nyingi za nyuki, na tumesema wilaya hizi ni za kuanzia, kwa hivi ni kweli kwamba wilaya ya Sumbawanga Vijijini ambako Mheshimiwa Mbunge, anatoka kwamba vipeperushi havijafika. Tuchukue kwamba hili ni ombi na tutajaribu kuangalia namna ya kufanya ya kupeleka mahususi kwenye Jimbo la Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, kuhusu watumishi kwamba watumishi hawajafanyakazi yoyote; ni kweli kwamba watumishi walioko ni wachache lakini kuna kazi ambazo wamezifanya. Na kwasababu *concentration* kwenye suala la nyuki kwa mkoa wa Rukwa limekuwa Wilaya ya Mpanda, ni kweli kwa Wilaya ya Sumbawanga Vijijini, unaweza ukaona kwamba hakuna kinachofanyika.

Lakini tuseme kwamba *focus* imekuwa ni eneo lingine hasa kwa kuangalia uwezekano, *potential* ya nyuki kufugika kwenye eneo hilo. Hili tumelichukua kama

changamoto, tutaangalia namna ya kuwatumia wataalamu wetu wachache walioko kwenye mkoa wa Rukwa ili waweze pia kufika kwenye Wilaya ya Sumbawanga Vijijini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kuziba matundu kwenye nguzo. Katika jibu la msingi nimesema kwamba tumewasiliana na Sekretarieti ya Mkoa. Kwenye Sekretarieti ya Mkoa, pia inajumuisha watu wa *TANESCO* na watu wa Idara nyingine za Serikali, jambo hili *RAS* wa Mkoa wa Rukwa analo na watatuma wataalamu hawa wa kuona namna gani litafanyika kwahivi watu wa *TANESCO* au watu wa Nishati watakuwepo kuona namna ya kutatua tatizo hili kwa njia ya kudumu.

Nilikuwa namwomba Mheshimiwa Mbunge, awe na subira ili Sekretarieti ifanye kazi yake kama tulivyoiomba, hakika naamini kwamba jibu litapatikana kwasababu wataalamu wote watahusika. *(Makofi)*

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini naomba niulize kama ifuatavyo. Kwa kuwa, Mkoa wa Tabora kuna Chuo cha Ufugaji Nyuki. Na kwa kuwa, Chuo hicho kinatambulika kimataifa na Chuo hicho ni cha muda mrefu. Je, Serikali haioni kukamilisha ukarabati wa Chuo kile kutasaidia kutoa mafunzo bora hapa nchini? *(Makofi).*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la nyongeza la dada yangu Mheshimiwa Mwanne Mchemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba uwepo wa Chuo cha Nyuki Tabora, unaweza ukasaidia sana kutoa elimu kwa wafugaji wa nyuki. Serikali ilishaanza ukarabati wa chuo hiki na tunategemea hadi mwisho wa mwaka huu tutaweza kuwa tumekamilisha na ninafikiri baada ya hapo matatizo yote yatakuwa yamekwisha. Kwa hivyo ni suala la *time frame,* matumaini yetu ni kwamba tutakamilisha katika mwaka huu wa fedha.

Na. 60

**Utata Kwenye Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa**

**MHE. WILLBROAD P. SLAA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika kifungu cha nne cha sheria ya mafao ya viongozi wa kisiasa kinatoa tafsiri ya viongozi wastaafu kwa maneno ya, "*aliyeshika nafasi" (Who held office)* na "aliyeacha kushika nafasi hiyo", *(Has ceased to hold that office),* tafsiri inayoacha utata jinsi muhusika anavyoacha uongozi yaani kwa kustaafu, kustaafishwa, kufukuzwa au kujiuzulu, mwenyewe; na Kwa kuwa, kwa mujibu wa sheria maneno hayo yanatofautiana hasa kuhusiana na malipo ya mafao:-

(a)Je, kwa mujibu wa sheria hiyo na kulingana na sheria nyingine zinazohusu mafao ya wastaafu wengine wa umma, ni tafsiri gani inayostahili malipo ya mafao kati ya hayo?

(b)Iwapo tafsiri haiko wazi. Je, viongozi walioacha kushika nafasi ya uongozi wao tangu sheria hiyo ilipoanza kutumika wamekuwa wakilipwa kwa utaratibu upi?

(c)Je, ni viongozi wangapi tangu mwaka 1999 hadi tarehe 31 Disemba, 2008 waliacha kushika nafasi zao kwa kila tafsiri zilizotajwa kwenye swali hili, kwa majina, vyeo na wamelipwa kiasi gani cha mafao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (JEREMIAH S. SUMARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Dr. Wilbroad Slaa, Mbunge wa Jimbo la Karatu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kuna tofauti ya jinsi ya kuhitimisha Utumishi wa Viongozi wa Kisiasa na wa Watumishi wa Umma na kwa hiyo kustahili mafao. Kustahili mafao kwa Viongozi wa Siasa ni kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa Na. 3 ya Mwaka 1999, kifungu cha 5:-

1. Anapomaliza kipindi chake cha uongozi wa kisiasa cha kuteuliwa au kuchaguliwa.

2. Akikoma uongozi kulingana na vifungu vilivyoko kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

3. Kwa kufutwa kwa ofisi ambayo aliteuliwa au kuchaguliwa.

4. Kukoma uongozi kwa ugonjwa.

5.Kukoma uongozi kwa kifo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Pensheni ya Mafao kwa Watumishi wa Umma Na. 2 ya 1999, Kifungu cha 16, inaainisha jinsi ya kustahili mafao ya kustaafu kama ifuatavyo:-

1. Kustaafu kwa hiyari baada ya kutimiza umri wa miaka 55.

2. Kustaafu kwa lazima baada ya kutimiza umri wa miaka 60.

3. Kustaafu kwa kufutwa kwa ofisi.

4. Kustaafu kwa ugonjwa.
5. Kustaafishwa kwa manufaa ya umma.

6. Kustaafu kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, tafsiri zinazodaiwa kuleta utata ni tafsiri mbili; ya kufukuzwa kazi na kujiuzulu, ambapo hazijafafanuliwa katika sheria hizo mbili za mafao na hivyo kuonekana kama kutotoa stahili ya malipo ya mafao.

Hatahivyo Viongozi wa kisiasa wanaojiuzulu wanastahili kulipwa mafao kama ilivyoainishwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(b) Mheshimiwa Spika, Viongozi wa kisiasa walioacha kushika nafasi ya uongozi tangu Sheria ilipoanza kutumika wamekuwa wakilipwa kulingana na Sheria hiyo Na. 3 ya mwaka 1999, kifungu cha 5, ikisomeka pamoja na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(c) Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 1999 hadi tarehe 31 Disemba, 2008, Viongozi walioacha kushika nafasi zao kwa kila tafsiri, kwa pamoja, zilizotajwa kwenye swali hili, walilipwa mafao kulingana na stahili zao. Viongozi hao ni kama ifuatavyo:-

1. Marehemu Makamu wa Rais wa Awamu ya Tatu.

2. Waziri Mkuu Mstaafu wa Awamu ya Tatu.

3.Waziri Mkuu Mstaafu wa Awamu ya Nne.

4.Spika wa Bunge Mstaafu wa Awamu ya Tatu.

5. Mawaziri na Naibu Mawaziri wa Awamu ya Tatu.

6. Naibu Mawaziri waliofariki katika kipindi cha Awamu ya Nne.

7.Wakuu wa Mikoa na Wilaya wa Awamu ya Tatu.

8.Wabunge wote wa kipindi kilichoishia Mwaka 2000.

9.Wabunge wote wa kipindi kilichoishia mwaka 2005.

**MHE. WILBROAD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize maswali madogo mawili ya nyongeza. Awali niseme tu kwamba kifungu cha (c) hakijajibiwa kikamilifu na hivyo malengo ya swali hayajakamilika. Pamoja na hoja hiyo, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri, amekiri kwamba kuna utata hasa kuhusu vipengele vya kufukuzwa lakini vilevile kuna vipengele vya kupigiwa kura ya kutokuwa na imani na kadhalika. Na kwa kuwa, viongozi waliotajwa ni wengi, na haitaji wanalipwa kwa

*formula* ipi. Je, Waziri atalieleza Bunge hili ni *formula* ipi inatumika kwa wale viongozi ambao hawajamaliza kipindi chao lakini wameondoka katikati? Na labda ikitokea pia kwa kufukuzwa au kwa kupigiwa kura ya kutokuwa na imani ni sheria ipi itatumika?

Je, Waziri yupo tayari kuleta sheria hiyo ifanyiwe marekebisho makubwa kwasababu kama tunavyoona idadi ya wahusika ni wengi, na kwa kuwa ni wengi wanaoacha katikati pia ni wengi na hizi ni fedha za Watanzania ambazo zinapaswa kufanya kazi nyingine. Kutokuwa na *formula* kunafanya fedha nyingi zitumike bila sababu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba nijibu maswali mengi ya Mheshimiwa Dr. Slaa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu kutojibu kwa ukamilifu swali lake (c). Ni kweli tumejibu kwa kutoa orodha ya makundi 10 ambayo yanastahili kulipwa mafao chini ya sheria ya mafao ya viongozi wa siasa. Lakini vilevile tumetoa na vyeo vyao. Swali (c) ilihitajika kwanza tuorodheshe viongozi wenyewe lakini tuorodheshe kwa majina. Vilevile tuorodheshe na vyeo vyao. Katika orodha hii ya mafungu 10 niliyotoa ni pamoja na wabunge waliomaliza muda wao mwaka wa 2000 na wabunge waliomaliza muda wao mwaka 2005 ni pamoja na wakuu wa wilya zaidi ya 130, ni pamoja na wakuu wa mikoa 21. Sasa sisi kwa busara zetu tukadhani kwamba kuja kuorodhesha hapa kwa muda ambao tunao wa kujibu hili swali haina tija, hiyo ni moja. Lakini kama Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Dr. Slaa, watahitaji tufanye hivyo na tutapewa muda, tutakuwa tayari kufanya hivyo. Pili muda unaohitajika ni kwa miaka 10, yaani mwaka1999 mpaka mwaka 2000. Tatu inahitajika, kwenye (c) hiyo hiyo, kutoa taarifa hizi kutokana na tafsiri nne; waliojiuzulu, waliofukuzwa, waliostaafu, waliostaafishwa. Vilevile tupo tayari kutoa hivyo.

Lakini la nne, ilitaka kujua ni kiasi gani cha mafao ambacho kinahitaji, sasa aina ya mafao kuna zaidi ya manne kuna pesheni, kuna *gratuity* kuna *winding up allowance* halafu kuna *Maintanance Allowance*. Sasa baada ya sisi Serikalini kutazama swali la Mheshimiwa Mbunge C, linataka habari zote hizi ukweli tumedhani kwamba Mbunge atakuwa na jambo maalum katika hii C, analohitaji basi alitamke na sisi tutamjibu. (*Makofi*)

Lakini B yake aliyosema ni kwamba nimekiri kwamba sheria yenyewe ina utata, nimesema inaonekana maana yake Mbunge kwenye swali ameanza na dibaji ndiyo akaenda kwenye maswali yake matatu. Sasa sheria sisi hatujaona utata wote kwa nini kwa sababu sheria yenyewe jina lake na naomba kunukuu *it is an Act to provide for the granting of benefit and services to leader upon see session of service in a political office* na neno hapa ni *upon.* Lakini la pili ukienda kwenye kifungu cha nne, ambacho amekitumia kuonyesha kwamba kuna utata, hakutaja vizuri kwa sababu kifungu cha nne tafsiri inasema *a person who has held office but* sasa yeye kachanganya kaweka na *but*

*has assist to hold that office* maana yake ni kwamba ili kupewa mafao haya ni lazima uwe umekuwa kwenye nafasi hizi lakini umeondoka.

Mheshimiwa Spika, la tatu nataka kusema ni kwamba nimesema kwamba sheria hii ya viongozi wa siasa inahitajika kusomeka pamoja na Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Kwa hiyo, ukisoma viwili hivi sheria yenyewe pamoja na Katiba linaloonekana kwamba lina utata linafutika, tatizo ni tafsiri ya kiingereza kwenda Kiswahili, kiingereza kigumu. (*Kicheko*)

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Mbunge yoyote anapohitaji taarifa anapouliza swali anatakiwa ajibiwe kikamilifu. Na kama Serikali inaona majibu yale ni marefu inatakiwa iambatanishe kwa maandishi yale mambo ambayo anahisi ni marefu. Kwa hiyo hayamzuii, hakuna sababu yoyote ya kusema maelezo haya ni marefu kama ni marefu unatoa majibu…

**SPIKA:** Mheshimiwa hilo sio swali la nyongeza.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ndiyo nataka kuuliza sasa ni kwanini Serikali baada ya kuona swali lile lina maelezo marefu wasilete kwa maandishi yale maelezo yanahitaji kujibiwa katika swali la Mheshimiwa Mbunge? (*Makofi*).

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge ngoja nitoe ufafanuzi ambao uta-guide pande zote mbili, mimi nadhani hapa Wizara ya Fedha na Uchumi imetumia hekima na busara kwa sababu kuorodhesha majina ya Wabunge 200 waliopoteza uchaguzi, 200 tena 2000 na una orodha ya majina 400 kweli inatija katika ma-*DC* wote mimi nina hakika swali lilikuwa ukilitazama kwa maudhui yake swali lililenga katika viongozi wakuu basi na kwa maana hiyo wale waliotajwa pale inatosheleza kwa vyeo vyao.

Lakini ni dhahiri Mbunge hazuiwi kwenda kuangalia majina ya Wabunge wote, ma-*DC* wote, wakuu wa mikoa ambao wamestaafu. Taomba Waheshimiwa Wabunge tuvumiliane katika hili inapokuwa sasa na sisi hapa 319 ukiorodhesha majina 1000 kwenye karatasi kuwagawia Wabunge 321 mimi sidhani kama hayo ni matumizi mazuri ya rasilimali ya nchi yetu. Kwa hiyo Serikali watakuwa *guided* na hilo kwamba pale ambapo jibu ni refu mno na rekodi iko ofisini basi anayetaka zaidi anaweza kufuata ofisini.

Na. 61

**Gharama za Matumizi ya Magari ya Kifahari**

**MHE. LUCY F. OWENYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, ghrama za matumizi ya magari ya kifahari (mashangingi) zimezidi kuwa mzigo kwa Serikali na wananchi kwa ujumla ambao ndio walipa kodi na Serikali inatambua hali hiyo:-

(a) Je, ni lini Serikali ilitambua hali hii na hatua zimechukuliwa?

(b) Je, ni kigezo gani kinatumika kununua magari haya kwa Wizara na Idara zake?

(c) Je, Serikali inasemaje kutokuwepo na tofauti ya magari yanayotumika Serikalini kufuatana na wadhifa wa kiongozi kwa mfano, *RC, DC, RAS, DAS,* Makatibu Wakuu na kadhalika.?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimia Spika, tangu kuanza kutumika kwa magari ya *Four Wheel Drive* (mashangingi) mwishoni mwa miaka ya themanini, Serikali imekuwa ikitathmini mwenendo wa gharama za matumuizi ya magari hayo na kubaini gharama kubwa za matumizi hususani magari hayo yanapoanza kuchakaa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbali mbali za kupunguza gharama za matumizi ya magari hayo ikiwa ni pamoja na kufuta magari yaliyochakaa kila baada ya miaka mitano na kuzuia matumizi yasiyo ya lazima kwa magari hayo kama vile kuelekeza magari hayo kuegeshwa wakati ambao hakuna shughuli za kikazi. Aidha, utaratibu wa kununua magari hayo umeanza kuandaliwa ili kupunguza wingi wa magari hayo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu minong’ono imekuwa ya sauti ya juu mno tusikilize jibu.

(b)Kigezo kinachotumika kununua magari ya aina ya *Four Wheel Drive* (mashangingi) kwa Wizara na Idara zake ni ubora, uimara na usalama wa magari hayo kuweza kuhimili safari ndefu katika barabara za vijijini ambako viongozi na watumishi wengine wa umma hulazimika kwenda kuwahudumia wananchi.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyogusia kwenye maelezo yangu na jibu la sehemu (a) ya swali hili, Wizara yangu hivi sasa inaandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri juu ya utaratibu wa matumizi ya magari ya Serikali kufuatana na wadhifa wa viongozi wa Serikali. Waraka huo ukishawasilishwa kwenye Baraza la Mawaziri na kukubalika, utaratibu huo utaanza kutumika ambapo nia yake itakuwa ni pamoja na kupunguza wingi wa magari ya aina ya mashangingi.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza, awali ya yote kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa

kusitisha ununuzi wa magari mapya kama mashangingi. Katika majibu ya Mheshimiwa Waziri amesema magari haya ni gharama kwa Serikali na bado kwenye Serikalli magari ya zamani yatakuwa bado yako Serikalini.

Je, Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka sasa kuuza magari yote ya Serikali tukabaki na machache ili fedha zile ziweze kutumika katika huduma za kijamii kama elimu, afya na kadhalika Maafisa hao kwa sababu wanaweza wakakopeshwa magari. Serikali iwakopeshe magari ili waweze kutumia magari yao binafsi.

Mheshimiwa Spika, swali la pili Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yake amesema kwamba watazuia matumizi yasiyo ya lazima. Madereva huwa wanapaki magari yao mbali na mabosi wao kwa mfano unakuta dereva anaishi Gongo la Mboto, bosi anaishi Mikocheni. Lakini inabidi amfuate bosi wake Mikocheni, halafu ampeleke ofisini na jioni amrudishe Mikocheni halafu aende akapaki gari lake huko Mbagala pengine kwenye ofisi za CCM au ofisi za Serikali.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka magari yale yatumike wakati wa *office hours* tu mabosi waje na magari yao, magari yaanze kutumika wakati wanapofika ofisini saa moja ofisini badala ya kutokea nyumbani na magari hayo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, hili la kwanza pendekezo la kwamba magari yote ya zamani yauzwe ili fedha hizo zitumike kwa shughuli nyingine za tija zaidi. Nataka niseme tu kwamba pamoja na mtazamo huu wa kutaka kupunguza matumizi ya magari katika idara na Wizara za Serikali lakini bado magari yatahitajika kuweza kuwahudumia viongozi pamoja na watumishi wa umma kuweza kuhudumia wananchi. Kwa sababu tukisema kwamba tuyauze yote yaliyochakaa kwa maana kwamba shughuli zingine za lazima za Serikali zitaathirika sana. Kwa hiyo, nimuwmbe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa hivi huu wakala ambao tunauandaa na maandalizi yote tunayoyafanya kwa kweli yanalenga katika adhima hiyo ya kupunguza matumizi ya Serikali. Kwa hiyo, nadhani tutakuwa makini sana kuhakikisha kwamba magari yatakayokuwa yananunuliwa ni yale yenye ulazima tu na kuhakikisha kwamba hilo pendekezo lake linazingatiwa kwa utaratibu.

Hili suala la kukopeshwa watumishi utaratibu huo ulikwishaanza, watumishi wa Serikali wanaendelea kukopeshwa magari na wanayatumia wanapokuja makazini kama alivyo dereva kwa suala lake hili la pili. Lakini swali la pili la kwamba magari yasiyo ya lazima madereva wasiwafuate mabosi wao majumbani nataka tu nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba si madereva wote ambao wanawafuata maofisa wao majumbani kwa sababu baadhi ya maofisa wana magari kama alivyokuwa amesema wanakuja na magari yao pale ofisini na magari hayo yanapokuja pale kazini yanatumika kwa kazi za ofisi pale. Lakini baada ya muda yanatakiwa yapakiwe kama nilivyokuwa nimeeleza katika jibu langu la msingi. *(Makofi)*

Na. 62

**Uvaaji wa Mavazi Vyuo**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa sasa kuna uhuru mkubwa wa mavazi katika Vyuo Vikuu ambapo wanafunzi huvaa mavazi wanayoyataka wenyewe; lakini wanachuo wa kike/wanawake walio wengi wanatumia uhuru huo vibaya pale wanapovaa nguo fupi kupita kiasi na zinazobana sana mwili:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa uhuru huo unatumika vibaya na hivyo ione haja ya kuweka sheria zitakazowataka wanachuo wavae mavazi ya heshima?

(b) Je, uongozi wa vyuo husika umeridhika na hali hiyo; na kama haukuridhika, umechukua hatua gani katika kudhibiti hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zambi, Mbunge wa Mbozi Maghariki, lenye sehemu a, b, na c kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hadi sasa Serikali haijatunga sheria inayohusu vazi rasmi au vazi la Kitaifa. Hata hivyo Serikali imetoa waraka wa mavazi kwa watumishi wa umma na baadhi ya vyuo vikuu kama vile MUHAS wanavaa vazi rasmi. Aidha, Serikali haipendezwi na tabia ya uvaaji wa mavazi mabaya yanayovaliwa na baadhi ya wanafunzi wa kike na wa kiume katika Vyuo Vikuu na jamii nzima kwa ujumla. Hata hivyo, neno vazi la heshima ni dhana inayojumuisha mambo mengi ikiwa ni pamoja na mila na desturi, imani za dini, utamaduni na makabila na sehemu wanazotoka.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu haina uthibitisho kuwa yupo Mhadhiri aliyeshindwa kufanya kazi za kufundisha kwa sababu ya mavazi ya wanafunzi au mwanafunzi wa kiume aliyeshindwa mtihani kwa sababu hiyo. Hata hivyo Serikali inakemea tabia ya uvaaji mbaya unaoweza kupelekea vishawishi kwa wahadhiri na wanafunzi wenyewe na inasisitiza kwamba wanafunzi wa vyuo vikuu wanatakiwa kuwa mfano bora kwa jamii katika uvaaji. (*Makofi*)

(c) Vyuo Vikuu vina sheria ndogo ndogo (*Students by Laws*) ambazo huongoza maisha ya kila siku ya mwanafunzi. Katika sheria hizo ndogo ndogo za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam "*Students by Laws*" za 1992 ziliyofanyiwa marekebisho mwezi Machi, 2005, kuna kifungu mahususi kinachomzuia mwanafunzi kudhihirisha mwili kwa namna isiyokubalika "*Indecent Exposure*". Sheria hizi ndogo ndogo, zikimtia mwanafunzi hatiani, humsababishia kupewa adhabu kulingana na kosa alilotenda. Wizara yangu inasisitiza kwamba uongozi wa vyuo vyote vikuu hapa nchini watumie hizi sheria ndogo ndogo kuwabana wanafunzi wanaovaa vibaya.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia inatoa wito kwa jamii nzima kutoa ushirikiano katika malezi na makuzi ya vijana ili kujenga taifa la vijana wenye nidhamu na maadili mema.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali madogo ya nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini ukweli ulio dhahiri kwamba wanafunzi wengi naomba niseme wengi sio wote katika vyuo vya elimu ya juu na vyuo vinginevyo wanavaa vibaya na kwa maana hiyo mavazi ambayo hayana heshima. (*Makofi)*

Pamoja na ukweli kwamba Mheshimiwa Waziri anasema wanavisisitizia vyuo hivyo viweze kutoa miongozo mizuri na kwa maana hiyo *by laws* zifuatwe. Lakini inaonekana utekelezaji ni tatizo kubwa. Waziri anatoa tamko gani rasmi kwa uongozi wa vyuo vikuu ili viweze kutekeleza *by laws* hizo na kwa maana hao wanafunzi waweze kuvaa vizuri? (*Makofi*)

Kwa kuwa, pia Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba hakuna sheria ya mavazi na mimi naelewa kwamba kuna baadhi ya nchi ambazo zina sheria za mavazi. Je, lini sasa Serikali itakuja na sheria ya mavazi kwa ajili ya Watanzania wote ili tuweze kupata heshima ambayo tunastahili mbele ya jamii ya kimataifa. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Spika, kuhusiana na tamko rasmi nimejibu katika swali la awali kwamba tumeagiza vyuo vikuu vyote vizingatie sheria ndogo ndogo walizojiweka kuhusiana na mavazi ambayo tunafikiri ndiyo ya heshima. Na tutawaandikia dokezo kuwakumbusha jambo hili. Kwa hiyo, hili tumeshawaeleza.

Sheria ya mavazi tumesema bado haijakuwepo lakini nimesema ofisi ya Rais Menejiment ya Utumishi wa Umma wametoa waraka kuhusiana na mavazi yanayohusiana na mavazi mazuri ambayo yanastahili kuvaliwa.

Kwa hiyo, tunawapa wito wanafunzi wetu pia wa vyuo vikuu waanze kuvaa mavazi ambayo tunafikiri ndiyo ya heshima, ili watakapokuwa wameingia katika Utumishi waUmma basi waendeleze mtindo huo wa kuvaa mavazi ambayo Mheshimiwa Zambi, pamoja na sisi wengine Watanzania tunafikiri ndiyo ya heshima. (*Makofi*)

Na. 63

**Kujenga Shule ya Kidato cha Tano na Sita Kilwa**

**MHE. HASNAIN G. DEWJI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Kilwa ni kubwa sana na haina shule ya Sekondari yenye kidato cha Tano na Sita:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga shule za aina hiyo katika wilaya ya Kilwa?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hasnain Gulamabbasi Dewji, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hivi sasa zipo Wilaya 40 ambazo hazina shule za sekondari zenye kidato cha Tano na Sita, hapa nchini, wilaya ya Kilwa ikiwa mojawapo. Serikali ina mpango wa kuhakikisha kwamba kila Wilaya ina kuwa na shule mbili za aina hiyo ifikapo mwaka 2010. Mpango huu ni endelevu lakini unategemea upatikanaji wa rasimali fedha na ushirikiano kati ya Serikali Kuu, Halmashauri na wananchi.

Mheshimiwa Spika, Uongozi wa Halmashauri ya Kilwa tayari imeanzisha shule ya Sekondari ya kutwa Kilwa na kuipa hadhi ya kuwa na kidato cha Tano na Sita ifikapo mwaka 2009. Hii ni hatua nzuri, ni wajibu wetu sote kuhakikisha kuwa shule hiyo inaimarishwa ili kuwa na sifa stahili za kuanzisha kidato cha 5 na cha 6.

**MHE. HASNAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri lakini nina maswali mawili madogo. Serikali ina mpango gani wa kupata walimu wenye sifa kwa ajili ya *High School* kwa wingi ili ikidhi mahitaji?

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais mwaka 2007 aliagiza kila tarafa iwe na *High School.* Je, mpango huo umefikia wapi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, Serikali inao mpango wa muda wa kati na muda mrefu kuhakikisha kwamba inapata walimu kwa ajili ya shule za sekondari na hususani za kidato cha Tano na Sita. Ifahamike kwamba walimu wa shule za *A level* ni lazima wawe wana sifa ya Shahada ya ualimu. Tunavitegemea sana vyuo vyetu vikuu ambavyo kwa ujumla wake vingi vimeshaanzisha *College of Education* ili waweze kutupatia walimu kwa shule hizo.

Mheshimiwa Spika, aidha, ili kuweza kupata hizi shule za kidato cha Tano na Sita kwa kila tarafa inabidi kuwe na mpango mkakati tena wa muda mrefu. Kwa kuanzia nimejibu kwa niaba ya Waziri wa Elimu kwamba tunaanza kila wilaya kupata shule mbili, shule hizi zinavigezo vyake zina umuhimu wake na mambo matatu makubwa lazima izingatiwe. Kwa hiyo, hatutaweza kwenda kwenye tarafa kabla hatujaenda kwenye wilaya. La kwanza lazima ziwe na maabara, kupatikane nyumba za walimu, kuwe na mabweni ili walimu watakaopangwa kwenda kwenye shule hizo wapate pa kuishi, wanafunzi wakazikute maabara na walimu wa kutosha wapatikane.

Mheshimiwa Spika, tunakwenda kwa hatua, iko siku tutafika kila tarafa kuwa na shule yake ya kidato cha Tano na Sita, ahsante.

**MHE. FATUMA MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nashukuru na nimekubali maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini tatizo la wilaya ya Kilwa sawa sawa na tatizo la wilaya ya Ruangwa. Wilaya ya Ruangwa tuliahidiwa tangu mwaka 2007 kuwa na *High School* katika shule ya Sekondari Ndekenyera. Nataka kufahamu Mheshimiwa Naibu Waziri kumetokea tatizo gani hadi leo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, kwa maelekezo yaliyotolewa na Wizara ni kwamba kila Halmashauri au Wilaya ibainishe shule ambayo wameitenga kuwa au wameipandisha hadhi ili iweze kupewa kidato cha tano na sita. Sifa hizo naomba kuzirudia, kwamba iwe na maabara tatu, iwe na nyumba za walimu zisizopungua tatu, iwe na mabweni yasiyopungua mawili kwa maana ya wasichana na wavulana.

Lakini pia kuwe na nyumba za walimu, ili ifahamike bila kukidhi vigezo hivyo hatuwezi tukatoa kibali. Wengi naomba kutoa masikitiko yangu wanaotuletea taarifa ya shule hizi wana madarasa na maabara nyumba za walimu hakuna. Inatuwia vigumu kutoa kibali shule hizi kuanza maana walimu ni binadamu kama siyo wanastahili hifadhi, wanastahili nyumba za kuishi wao na familia zao.

Ni vyema na wao tukawapa kipaumbele, kinyume chake taarifa yoyote itakayoletwa hata kama kuna maabara na mabweni hakuna nyumba za walimu, nasikitika hatutaweza kutoa kibali huku tutakuwa tunawadhalilisha walimu maana hakuna mipango mahususi inayoandaliwa kwa ajili ya walimu. Matokeo yake ukiwapeleka wanatanga tanga hawana pa kuishi wanakwenda kujibana tunawavunjia utu na heshima yao, wanapoteza ari ya kufanya kazi. (*Makofi*)

Na. 64

**Kuboresha Kilimo na Soko kwa Zao la Nyanya**

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi kijiji cha Chiwata jimbo la Lulindi wameonyesha mfano mzuri wa kilimo cha nyanya:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kuboresha miundombinu itakayochochea kilimo cha zao hilo kama vile barabara, kiwanda cha *juice* na soko la uhakika?

(b) Je, Waziri husika yupo tayari kufanya ziara katika kijiji hicho cha Chiwata – Chivya?

**WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchaya, Mbunge wa Lulindi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo inatekeleza Mipango ya Kilimo ya Wilaya *(DADPs)* katika Halmashauri zote nchini. Maandalizi ya *DADPs* huanzia katika maandalizi ya Mipango ya Kilimo ya Vijiji *(Village Agriculatural Development Plans (VADPS)* ambayo huandaliwa kwa kuwashirikisha wananchi katika vijiji vyao.

Kupitia Mipango huo wananchi wana uhuru wa kuchagua miradi ambayo itaongeza tija na uzalishaji ili kuwaongezea kipato. Aidha, wanaweza kutekeleza miradi ya viwanda vidogo vya kusindika mazao wanayoyazalisha ili kuongeza thamani ya mazao hayo na hivyo kujiongezea kipato.

Ili kuhakikisha wananchi wanakuwa na uwezo wa kuibua miradi hiyo, kuanzia mwaka 2005/2006, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ikishirikiana na Wizara nyingine za Sekta ya Kilimo yaani Wizara za Viwanda, Biashara na Masoko; Mifugo na Uvuvi na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imekuwa ikitoa mafunzo kwa timu za wawezeshaji katika ngazi ya Mikoa, Wilaya na Kata.

Hivyo, nashauri wananchi wa kijiji cha Chiwata ambao ni wakulima wa nyanya kushiriki kikamilifu katika uandaaji wa *VADP* kwa lengo la kuhakikisha vipaumbele vyao vinaingia katika *DADPs* ya Halmashauri yao pamoja na mipango ya Halmashauri hiyo kuhusu miradi ya ujenzi wa miundombinu kama barabara.

(b) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na mwaliko wa Mheshimiwa Mbunge wa kutembelea kijiji cha Chiwata na napenda kuchukua fursa hii kumshukuru kwa mwaliko huo. *(Makofi)*

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri yanayohusiana na eneo hili la Chiwata. Eneo hili la Chiwata mimi nalifahamu vizuri sana na kwa kuwa vijana wale ni wachapa kazi kweli kweli na ni mfano wa kuigwa nafikri Tanzania nzima. *(Makofi)*

Je, Waziri kwa namna ya pekee kwa nini asiwapendelee hawa vijana kwa kuanzisha kituo maalum cha utaalam kitakachoweza kusambaza utaalam huo wa upandaji wa mboga mboga, nyanya, vitunguu na kadhalika katika eneo hili la Chiwata pamoja na kuwapendelea kuwapa kituao ambacho malighafi pamoja na madawa yataweza kupatikana kwa urahisi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kupitia kwake niwapongeze hao vijana kwa kazi nzuri wanayofanya. Katika jibu la msingi nimesema hivi, tunao Mpango wa Maendeleo ya Kilimo ambao unashirikisha wilaya zote.

Kwa kweli kwa mahali kama pale ambapo vijana hao wanafanya kazi vizuri jambo kubwa ambalo ninaweza nikashauri ni kuishauri Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ielekeze nguvu kupitia mpango wa *DADPs* ili kuhakikisha kwamba vijana wale wanapata manufaa.

Kwanza wanapata utaalam ili waweze kuzalisha zaidi na hasa wanapofikia mahali pa kutaka kuanzisha kiwanda, basi wawe na malighafi ya kutosha inayotokana na uzalishaji unaojitosheleza pale kijijini.

Hilo ndilo ninaloweza kusema kwa sasa. Aidha wako vijana wengine vilevile katika maeneo mengine ya nchi yetu ambao wanafanya kazi hiyo na Wizara yangu inatilia mkazo sana uzalishaji wa mazao ya bustani na ningependa kuwaambia Waheshimiwa Wabunge kwamba tumeanza kwa wakulima wa bustani. Sasa wameanza kusafirisha mazao moja kwa moja kwenda kuuza nchi za nje hasa Ulaya, kitu ambacho kilikuwa huko nyuma hakifanyiki. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunawapa moyo na kama nilivyoalikwa nikipata muda nitakwenda kuwatembelea na kuwaona vijana hao na kuwapa moyo zaidi ili waongeze uzalishaji maradufu. *(Makofi)*

Na. 65

**Ugonjwa wa Embe**

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS** aliuliza:-

Kwa kuwa, ugonjwa unaoshambulia embe umeathiri sana usafirishaji wa zao hilo nchi za nje kwa muda mrefu sasa hivyo kulikosesha Taifa fedha za kigeni:-

Je, Serikali ina mpango gani na wenye matumaini ya kutokomeza ugonjwa huo ili embe za Tanzania ziendelee kukubalika kwenye masoko ya nje.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani kama ifuatavyo:-

Katika mwaka 2003, baada ya Wizara kupata malalamiko kutoka kwa wakulima juu ya uharibifu mkubwa usio wa kawaida wa zao la embe, Wizara iliwaagiza wataalam wake kufanya uchunguzi juu ya uharibifu huo na kugundua kuwa kuna nzi wa matunda

ambaye hakuwahi kuwepo nchini ndiye anayefanya uharibifu huo. Uchunguzi huo ulionesha kwamba nzi asipodhibitiwa anaweza kuharibu takriban asilimia 80 ya mazao ya mkulima na hivyo kusababisha hasara kubwa.

Ili kunusuru mazao ya matunda na soko la matunda Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ilichukua hatua za haraka kwa lengo la kupata mbinu za kukabiliana na mashambulizi ya nzi hao. Hatua hizo ni:-

(a) Ilifanya utafiti na kugundua kwamba wakulima wakitekeleza vigezo vya udhibiti husishi wa visumbufu vya mimea (*IPM*) hususan kwa kufanya usafi na kuondoa matunda yaliyodondoka ambayo ndiyo mazalio ya nzi hao. Aidha, iligundulika kwamba dawa aina ya *methyl eugenol* ina uwezo wa kuwavuta kwa wingi wadudu hao na hivyo kuwezesha kuwaangamiza kwa wingi. Baada ya ugunduzi huo, Serikali iliagiza dawa hiyo na kuisambaza kwa wakulima wa maembe. Dawa hiyo imetoa mchango mkubwa katika udhibiti wa nzi hao.

(b) Jumla ya wataalam 135 na wakulima 800 kutoka maeneo yanayozalisha zao la embe kwa wingi walipatiwa mafunzo juu ya mbinu za kukabiliana na nzi huyo. Aidha, hadi Disemba mwaka 2008, jumla ya mabango na vipeperushi 7,500 yaliandaliwa na kusambazwa kwa wakulima kwa lengo la kuwaelimisha.

(c) Wizara kwa kushirikiana na kituo cha utafiti cha *ICIPE* kilichoko Nairobi, Kenya imeagiza na kuwasambaza wadudu walawangi (*biological control agents*) kwa lengo la kuwatumia kuwala wadudu hao na hivyo kupunguza mashambulizi yao.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hadi sasa Serikali imeweka mkazo na ushawishi mkubwa juu ya kupanua kilimo cha embe na kwa kuwa wananchi wengi wameshawishika katika kuwekeza katika kilimo hiki cha embe na kwa kuwa, hadi sasa juhudi za Serikali kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri hazitaleta mafanikio yoyote ya kutokomeza ugonjwa huo. Je, Serikali ina mikakati gani ya ziada ya kutokomeza ugonjwa huu ili juhudi za wakulima wa embe zisikatishwe tamaa na hali halisi iliyopo ya ugonjwa huo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa baadhi ya wakulima wa embe wamebuni mbinu mbadala za kukabiliana na ugonjwa huu wa embe kwa kuzianika juani mara tu baada ya kuzivuna hivyo kuondoa uwezekano wowote wa wadudu hao kuleta uharibifu. Je, Serikali inaifahamu teknolojia hii ya wakulima na iko tayari kufanya utafiti wa kisayansi ili kuiboresha?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza sikusema kwamba hakuna fanikio lolote lililokwishapatikana, nilichosema ni kwamba tumechukua hatua na hatua ambazo tumezichukua zimepunguza kwa kiasi kikubwa uharibifu kwa sababu kama hatua hizo zisingekuwa zimechukuliwa nzi huyu angeweza akaharibu zaidi ya 80% ya zao zima la embe. Ni kweli nzi yule bado yupo na sasa hatua tuliyoichukua ni kuleta wadudu ambao wataangamiza nzi ili kukomesha kabisa tatizo hilo. Kwa hiyo, nafikiri hili suala linaendelea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kuanika embe kama njia mojawapo ya kudhibiti huo ugonjwa na kama Serikali tunaijua. Kwa kweli Serikali tunaweza kusema hatuijui kwa sababu hatujatafiti lakini kwa maelezo haya ya Mheshimiwa Khamis sasa tutavipa vituo vyetu vya utafiti ili tuone kama kuanika kule kunaweza kukazuia wale wadudu bila kuharibu ubora wa eneo lenyewe.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, swali linalofuata naliahirisha kwa sababu lilivyoifikia Wizara lilikuwa na sehemu A peke yake, kwa hiyo ndiyo iliyojibiwa. Lilivyojitokeza leo lina A na B, kwa hiyo tumelififikisha Wizarani na watakapokuwa tayari basi tutaliweka katika *Order paper*.

Kwa hiyo, sasa nimeongeza dakika chache tunamalizia swali ambalo linaelekezwa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi linaloulizwa na Mheshimiwa Fuya G. Kimbita wa Hai.

**Na. 66**

**Ujenzi wa Mabwawa kwa Ajili ya Mifugo**

*(Swali lililotajwa hapo juu liliondolewa na Spika)*

Na. 67

**Kutumia Mizani Katika Minada ya Mifugo**

**MHE. FUYA G. KIMBITA** aliuliza:-

Kwa kuwa, utaratibu uliopo hivi sasa katika minada yetu katika kuuza mifugo ni kukadiria kwa macho thamani ya mifugo:-

Je, ni lini utaratibu wa kutumia mizani katika minada utaanza?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fuya G. Kimbita Mbunge wa Hai kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kutumia mizani kupima uzito wa mifugo ya biashara ili kujua thamani yao ulikuwepo hata siku za nyuma wakati Serikali ilipokuwa inajihusisha na biashara ya mifugo kupitia kampuni zake za *Tanganyika Packers* na Kampuni ya Biashara ya Mifugo Tanzania (KIBIMITA). Utaratibu huu uliathirika baada ya Serikali kuiachia sekta binafsi jukumu hili la biashara ya mifugo na hivyo kufanya hata baadhi ya mizani iliyokuwepo kuharibika. Hata hivyo, kwa kuzingatia umuhimu wa kufanya biashara ya mifugo kwa kigezo cha uzito, Wizara yangu imekuwa ikiweka miundombinu hii muhimu ya mizani minadani ili kuwezesha kufanyika kwa biashara ya haki na kutoa uwiano mzuri kimapato kati ya muuzaji na mnunuzi.

Mheshimiwa Spika, hapa nchini, tunayo minada zaidi ya 300 ikiwemo ya Awali, Upili na Mpakani. Wakati minada ya Upili na Mpakani inasimamiwa na Wizara, ile ya Awali ipo chini ya usimamizi wa Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa mizani ipo katika minada mbalimbali ikiwemo ya Pugu (Ilala), Korogwe (Korogwe), Themi (Arusha), Weruweru (Moshi), Mererani (Arusha), Lukole (Karagwe), Murusagamba (Ngara), Ushirika (Nzega), Buzirayombo (Chato), Nyamatara (Misungwi), Sengerema (Sengerema), Kasamwa (Geita), Shanwa (Maswa), Sekenke (Manyoni), Bungurwa (Kwimba), Igunga (Igunga), Iboregelo (Igunga) na Ipuli (Tabora).

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwekwa kwa mizani katika minada, mingi ya mizani hiyo haifanyi kazi na kutokana na kukaa kwa muda mrefu bila kutumika mizani hiyo imechakaa na mingine kuharibiwa kwa makusudi kwa kuondoa baadhi ya vifaa kama vyuma chakavu. Lakini hata pale ambapo mizani inafanya kazi, lipo tatizo la kutotumika kutokana na upotoshaji unaofanywa na wafanyabiashara wa kati (Magaragaja) kwa lengo la kujinufaisha zaidi kibiashara.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua athari za kutotumika kwa mizani katika biashara ya mifugo, Wizara yangu inafanya mapitio ya Kanuni za miongozo inayosimamia uendeshaji wa biashara ya mifugo katika minada itakayotoa msisitizo zaidi katika matumizi ya mizani kwa lengo la kuleta ufanisi katika biashara hiyo ya mifugo. Aidha, natoa wito kwa Halmashauri zote za Wilaya waweke mizani kwenye minada ya Awali isiyo na mizani iliyopo kwenye maeneo yao kwa lengo la kuwezesha kufanyika kwa biashara ya mifugo ya haki na hivyo kuwafanya wafugaji wanufaike na mifugo yao.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri lakini naomba nimwulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, uuzaji wa mifugo pasipo kutumia mizani ni sawasawa na ile biashara ya mazao kufanyika kwa njia ya lumbesa na Serikali imejitahidi sana na inajitahidi sana na napenda kuipongeza kwa kupiga vita biashara ya lumbesa. Je, Wizara yake itakuwa na mikakati gani ya haraka ya kuhakikisha mizani inafanya kazi katika minada yote ili kutokuwapunja wafugaji wetu?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli nimetembelea sehemu nyingi za minadani hata ule wa Pugu

na huu wa Dodoma na kukuta mizani ipo na haitumiki. Kama nilivyosema katika jibu la msingi ni kwamba tutaandaa miongozo ambayo itakuwa ni lazima katika kila mnada kuwe na mizani.

Kwa upande wa Wizara naamini kwamba tutaweka mizani ambayo iko katika minada michache ambayo tunayo na ile ambayo imeharibika tutaitengeneza, lakini kwa upande wa Halmashauri naomba kupitia katika minada mradi wa *DADPs* wananchi waweze kuibua miradi na tutahakikisha kwamba minada iliyopo huko inapatiwa mizani ili mifugo iweze kununuliwa kwa uzito na kuacha wananchi wasidhulumiwe na wafanyakazi wa katikati. Naamini kwamba ili kutoa haki ni lazima hii mizani iwepo na tutahakikisha kwamba tumefanya mapitio ya mwongozo na kusititiza kwamba, kwa ambaye hatafuata uuzaji wa ng'ombe kufuatia uzito atakuwa anavunja Sheria na Sheria itachukua mkondo wake.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umepita na ukiacha lile ambalo tumeahirisha basi maswali yamekwisha. Sasa ni matangazo, naanza na wageni:

Mgeni wa kwanza ni mgeni wa Mheshimiwa James D. Lembeli na Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti. Yeye ni Bwana Rajab Muhembe ambaye ni Mwenyekiti wa Chama Cha Ushirika cha Msingi Tujitegemee cha Mjini Kahama. Ahsante na karibu sana. (*Makofi*)

Wapo wageni kutoka Chama cha Waganga wa Tiba asilia, vipi mnaogopa? Pia na Wakunga wa Jadi ambao ni Bwana Mita Magombego, Katibu Mkuu Taifa. Ahsante sana na karibu sana. Bi Fatma Machangwa Katibu Mwenezi Taifa; Bwana Issa Mdoe, Mwenyekiti wa Waganga wa Tiba Asilia Mkoa wa Dodoma; naona ndiye mwenyeji wao. Mwenyeji hayupo? Labda ametoa udhuru kidogo au pengine haonekani kwa macho kwa sababu hawa jamaa…, basi Bwana Mdoe kama upo karibu. (*Kicheko/Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, pia yupo Bwana Salum Misanya, Katibu Mkoa wa Dodoma, eeeh! Nina hakika wapo tu hawa, karibuni sana. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge sasa ni matangazo ya kazi, kuhusu taarifa za mikutano. Ninawaarifu Wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi tutakuwa na Kikao Saa 5.30 asubuhi kwenye Ukumbi wa Spika. Kamati ya Uongozi hiki ni kikao muhimu sana, kwa hiyo, ningesihi basi kwa sababu naona matangazo yanayofuata ni Wenyeviti wa Kamati wanaita Wajumbe wao katika vikao vya Kamati, pale ambapo ni lazima kabisa Mwenyekiti ubaki katika kikao cha Kamati yako basi tafadhali mtume Makamu Mwenyekiti aje kwenye Kamati ya Uongozi. Kwa tahadhari hiyo basi, naendelea na matangazo kama ifuatavyo: Mheshimiwa Wilson Mutagaywa Masilingi, Mwenyekiti wa Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo mkutane saa 5.00 leo katika Ukumbi namba 231.

Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Bora anawatangazia Wajumbe wote wakutane mara baada ya kipindi hiki cha maswali katika Ukumbi namba 227.

Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu anahitaji Wajumbe wote wa Kamati ya Miundombinu mkutane leo saa 6.00 mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Mheshimiwa Dr. Wilbrod Peter Slaa, anahitaji Wajumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa *LAAC* wakutane saa 5.00 asubuhi katika Ukumbi namba 219 na mwisho, Mheshimiwa Elietta Namdumpe Switi amenituma nitangaze kwamba Wabunge wote Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi wakutane leo saa 7.00 Mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo mwisho wa matangazo. Ili kuweza kuandaa mkutano wa Kamati ya Uongozi, basi namwita Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mwenyekiti aweze kuja ili aendeleze shughuli zinazosalia. (*Makofi*)

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Zubeir Ali Maulid) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori wa Mwaka 2008
### *[The Wildlife Conservation Bill, 2008]*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo na atafuatiwa na Mheshimiwa Felister A. Bura na Mheshimiwa Said Amour Arfi ajiandae.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia Muswada huu uliopo mbele yetu wa Uhifadhi wa Wanyamapori 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Shamsa Selengia Mwangunga pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige na watalaam waliohusika kuandaa Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Liwale ina eneo lipatalo 38, 000 *square kilometres*, 53% ya eneo hilo ni hifadhi ya wanyamapori ambayo inatumika kwa uwindaji wa kitalii. La kushangaza vijiji vinavyozunguka hifadhi hiyo havifaidiki na chochote na havinufaiki kimaendeleo. Siyo hivyo tu, badala yake vinaathirika kutokana na wanyamapori hao.

Kuna watu wanapoteza maisha yao, mazao yanaharibiwa na pia kuna wengine wanajeruhiwa kiasi kwamba wanakuwa na ulemavu wa kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza kwa kuwa hawa wanyamapori hawajui mipaka yao, hivyo unakuta wanakwenda nje ya vijiji ambavyo vimeainishwa kwa ajili ya wanyamapori, wanazagaa Liwale nzima na matokeo yake ni kwamba hii imekuwa tishio kwa usalama wa wana Liwale kwa ujumla katika Wilaya ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 8 cha Muswada huu inaelezea taratibu ambazo zimewekwa ili kuweza kutoa kifuta machozi kwa ajili ya watakaopoteza maisha au mazao yao yataharibiwa au wale watakaojeruhiwa. Ukiangalia jinsi ilivyo, Serikali haiwajibiki vyovyote pale, haina ulazima wa kutoa kifuta machozi kwa kuwa imesema tu Waziri atazungumza na Waziri wa Maliasili. Kweli! Lini wataonana na Waziri wa Fedha ili waweze kuzungumza na hakuna *time frame* baada ya kutokea tukio, kwamba ikitokea tukio basi kama ni fidia au kama ni kifuta machozi kitatolewa baada ya muda fulani. Kwa hiyo, inaonekana maisha ya binadamu hapa hayajaliwi kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaashiria kwamba yale maisha bora yanayozungumzwa ni kwa wanyamapori na siyo kwa binadamu ambao wanatupigia kura, inasikitisha sana. Sielewi katika kufanya hivi, hii ni hulka ya utawala bora tuliyonayo au vipi, kwa nini tunafanya hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi niko katika hali ya kumuunga mkono Mbunge wa Tunduru Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura kwa kutokuunga mkono Muswada huu. Hii ni kutokana na kwamba hali ngumu tunayopata sisi katika Vijiji vyetu, sisi hatukuomba kukaa na wanyamapori na wanyamapori hao tumewakuta tu katika mazingira hayo, walikuwepo kabla ya ukoloni na hata baada ya ukoloni. Lakini wakoloni walikuwa wana utaratibu mzuri mpaka baada ya kupata uhuru na kulikuwa na *Games Scouts* katika Liwale siyo chini ya 50 na walikuwa wanajua nini kinachoendelea na matatizo haya yanayojitokeza sasa hivi yalikuwa ni aghalabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasoma, natoka katika Kijiji changu cha Kipelele kwenda Liwale kuanza shule ya msingi kwa kuwa shule za msingi zilikuwa chache. Nililetewa *Game Scout* wa kufuatana naye kwa miguu, alikuwa hana viatu nami sina viatu na wale walikuwa ni darasa na nne au hawakusoma. Nimetembea naye kwa muda wa kilomita 60 siku mbili tumelala kufika Liwale kwenda kuanza Shule. Sasa palikuwa na utaratibu mzuri sana lakini sasa hivi utaratibu uliopo wa kuwalinda wanyama hawa sijui ni wa aina gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi hapa tumeambiwa kwamba Askari au kadri itakavyokuwa watumishi wako wachache, hiyo ina maana kwamba wanyamapori hao sasa wanalindwa na wananchi wetu sasa vipi wasithaminiwe maisha yao wanapokuwa hatarini? Hili linatakiwa liangaliwe kwa karibu sana. Sio kwamba sisi tunanung’unika bure, kuna vigezo na pia kuna matatizo ambayo yametupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi kilichopita tu kabla ya mwaka jana haukwisha kilichotokea ni kwamba katika Kijiji cha Kimambi, mwananchi mmoja kwa jina la Jamal Ngalondola, huyu alikuwa amekwenda shambani kwake, alivyoanza kulima, kukaa kidogo akakutana na Simba, alichokifanya mwananchi huyu ni kukimbilia mti akapanda mpaka juu, sijui alifikaje huko juu lakini alikwenda juu. Simba akaja akakaa chini ya mti ule kumsubiri pamoja na mwanaye, yule jamaa alikuwa anasikia sauti za kutoka vijijini akajaribu kupiga mayowe ili wanakijiji wamsikie kwa bahati mbaya upepo ulikuwa unavuma kutoka kule kijijini kuja kwake kwa hiyo sauti yake haikumsaidia kitu kwa siku ile, alilala juu ya mti mpaka siku ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanakijiji walipoona hajarudi, ikabidi wamfuate mpaka kule shambani. Walipokaribia kule kwenye mti yule jamaa akasema kwamba jamani kama hamna silaha rudini kwanza nyumbani mkachukue silaha hapo chini kuna Simba na mwanaye wananisubiri. Kwa hiyo, wakaenda wakajiandaa wakaja wakamsaka yule Simba wakamuua na yule Bwana akashuka chini ya mti. Sio hiyo tu matukio haya yako mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kijiji cha Mkundi, kijiji ambacho kiko nje ya Selous kilichotokea ni kwamba, mkulima amekwenda shambani, baada ya kurudi akapita kwenye mto kuosha jembe lake aanze kurudi nyumbani. Akavamiwa na Chui, akapigana naye kiasi cha kwamba alifanikiwa kumuua lakini akaishia hospitali ambako nimemuacha amelazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kijiji kingine cha Lilombe ambacho nacho kiko nje ya Selous hali ikawa ni hiyo hiyo. Mkulima amekwenda kufukuza nyani, matokeo yake kukawa na simba, simba akawaacha wale nyani, akamshambulia mwananchi, wakapigana kiasi kwamba yule simba akakimbia. Huyu mtu pia nimemwacha hospitali Liwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matukio chungu nzima ya aina hiyo, kuna watu kama sita hivi mpaka 2008 wameshapoteza maisha na siyo hivyo tu zaidi ya watu 10 wamejeruhiwa. Sasa leo hii tunasema kwamba suala hili atakapofikiria Mheshimiwa Waziri na Waziri wa Fedha ataona jinsi ya kufanya. Jamani hii ni kweli jamani? Naamini kabisa hapa hatuwatendei haki wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwa masuala kama haya tuwajibike, kitu ambacho tungeweza kufanya ni pamoja na kutafuta au kubuni utaratibu ambao wananchi hawa watapata *Insurance* au Bima hiyo inawezekana kwa kuwa Sekta ya Utalii inapata mchango mkubwa sana kutokana na utalii wa uwindaji. Naomba kitu hicho kifikiriwe.

Sio hivyo tu, pia kuna matukio ya watu kupoteza maisha, mazao yao kuliwa hovyo na kujeruhiwa na kupata ulemavu wa kudumu yanatokea mara kwa mara. Serikali inawajibika vipi? kwa nini Waziri mhusika, Katibu Mkuu, Mkurugenzi mhusika wasijiuzuru kwa kushindwa kuhifadhi wanyamapori? Ni lazima tufanye kazi lakini kama

hivi tu tunakwenda kwenye mikutano Marekani tunarudi, tunatunga sheria ambazo zinaathiri wananchi wetu itakuwa kazi kubwa sana, itakuwa hatuwatendei haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio hivyo tu pia kuna utaratibu mwingine ambao tungeweza kuufanya. Kwa nini basi tusiitumie Mahakama katika kutoa kifuta machozi? Kwa kuwa, sina uhakika kama wakati mwananchi wangu atakapoathirika na wanyamapori kweli Waziri wa Maliasili atakuwepo nchini au Mkurugenzi wake atakuwa nchini, kwa nini tusitumie utaratibu wa Mahakama wa mtu kwenda kudai chochote tu ambacho kitakuwa ni haki yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu ingekuwa vizuri sana ukaletwa mbele yetu baada ya Serikali kutimiza baadhi ya ahadi ambazo iliweka kwa wananchi wetu wakati wanazunguka vijijini kwa mfano Liwale, au kwa jamiii zote. Kilichotokea ni kwamba tuliahidiwa tutapata 25% kutokana na uwindaji. Upatikanaji wa pesa hizi kusema kweli ni mgumu na hauna mtiririko mzuri hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Liwale ilipata milioni 16 tu na hakuna maelezo ya ziada kwa suala hilo na siyo hivyo tu utakuta miaka kama 2004/2005 na 2005/2006 hatukupata kabisa. Sasa mnategemea wananchi hawa wataendelezwa vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio hivyo tu, kwa Liwale walituahidi kwamba barabara kutoka Ndapata kwenda Ulanga itafufuliwa ambayo ilifungwa kutokana na wanyamapori na kwamba watashirikiana na Miundombinu, lakini hadi leo hii hakuna kilichofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hayo tu nina mambo mengine kadhaa. Kwa mfano, kuna boma la Liwale la Mjerumani, boma hilo waliahidi kabisa kwamba watasaidia kulifufua *by instalment*, kazi ile ilitakiwa ifanywe na *GTZ*. *GTZ* ilivyotoka Wizara iliahidi kabisa kwamba itatoa milioni nane kama walivyoahidi *GTZ* ianze kukarabatiwa awamu kwa awamu lakini mpaka leo pesa hizo hazipo. Sasa wananchi hao unavyoletwa Muswada huu wanaelewa nini kinachoendelea? Si wanajua kama wanavurugwa tu. Kama mimi siwezi kuelewa nini kinachoendelea, je, wananchi wangu unategemea wataelewa kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni tu tulikuwa na matatizo, palikuwa na wimbi la ng'ombe kuzidi, hii ilitokana na wafugaji kutoweza kufanya *family planning* kwa mifugo yao. Matokeo yake ng'ombe hao wakapelekwa kule Kusini na tunashukuru wapo wanatupa adha. Sasa kwa nini basi wataalam tunao kama akina Mheshimiwa Job Y. Ndugai na kadhalika wale Simba waliopo kule Liwale tusiwachote pamoja na Tembo wakaja huku? Wengine wakakaa Kongwa pale na wengine wakapelekwa Dar es Salaam wakasaidia kuwapokea watalii.

Kuhusu ujangili, suala la ujangili kusema kweli ni suala ambalo ni nyeti kwa kuwa ujangili umezidi kutokana na Wizara yenyewe husika, vyombo vya ulinzi havifanyi kazi yake vizuri, matokeo yake ndiyo haya, hebu niambie mwanakijiji kutoka Liwale ataua tembo achukue meno atakwenda kumuuzia nani? Ninyi ndiyo mnajua soko na mnajua bei. Lakini kinachotokea ni kwamba, inatokea *operation* na imewahi kutokea

katika Jimbo langu la Liwale, wakati huo mambo yamezidi wanafanya *operation* na kabla hawajafanya *operation* Maafisa wao wanahamishwa, matokeo wanakwenda kuteswa wananchi. Hivi jamani tunawatendea haki wananchi hawa wakati ninyi wenyewe wakiumizwa hamwathamini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kweli sitaunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nashukuru kwa kunipa nafasi na kwa kuzingatia amri ya Mheshimiwa Spika, kwamba Wenyeviti lazima twende kwenye Kikao saa 5.30, kwa hiyo nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutoa mchango wangu juu ya Muswada ambao upo mbele yetu. Naupa uzito sana Muswada huu kwa sababu Muswada huu unaashiria kwamba ardhi tuliyopewa na Mwenyezi Mungu inatubidi tuwaachie wanyamapori ili waweze kulindwa kwa sheria na kwa ajili ya kupata faida kutokana na lindo hilo la wanyamapori kwa ajili yetu sasa hivi na kwa baadaye. Kwa hiyo, huu ni Muswada muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho nataka kusema ni kwamba sheria nyingi tunazitunga za kuwalinda wanyama. Lakini ninavyoona sasa hivi katika nchi yetu kuna upendeleo mkubwa sana kuwalinda wanyamapori kuliko kuwalinda wanyama ambao wananchi tunao kama vile ng'ombe. Ninavyozungumza hivi sasa ni kama vile Serikali hii ya Awamu ya Nne imetangaza vita kati ya Serikali na ng'ombe. Hivi ninavyozungumza Kilosa kuna ng'ombe zaidi ya 2500 ambao wamekamatwa na Serikali kwa amri ya *DC* hawajalishwa siku nne na wale ambao wanawafuga wanaambiwa walipe milioni 75 ili wawachukue wale wanyama wao, sio kwa kuwatembeza kwa magari na hawajui wawapeleke wapi. Ukiwaweka kwenye magari wanapotoka Kilosa wanauliza wanakwenda wapi na wasipojibu lile swali wanaambiwa warudi kule walikotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo inaonyesha upendeleo ambao tunauweka zaidi kwa wanyamapori kuliko kwa wanyama tunalionao. Sasa najiuliza hivi kura tunazopigia hii Serikali zinapigwa na wanyamapori au zinapigwa na wafugaji? Hili ni jambo muhimu ambalo hivi sasa ni lazima tujiulize maana yake hili jambo liko Tanga, liko Urambo, liko Kilosa na hakuna ufumbuzi wowote ambao unatokea. Natoa wito kwamba, naomba Serikali tunapotengeneza sheria tutengeneze sheria ambazo zinaleta usawa mahali pote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili jambo la Kilosa Mheshimiwa Waziri Mkuu, ananisikiliza sasa hivi naomba hawa ng'ombe waachiwe mara moja kama utaratibu wa kuwahamisha haujawa kamili ili wananchi hawa wasijione kwamba wenyewe ni wakimbizi katika Taifa lao wakati Serikali inawalinda wao pamoja na mali zao ambazo kwa sasa hivi ni ng'ombe. La sivyo hatutawaelewa na zaidi inapokuwa kwamba hawa wananchi ni wa kabila moja na zaidi ni Wasukuma na wachache ndiyo Wamasai. Sasa hatuwezi kuwa nchi ambao inabagua watu na huku tuna Katiba inasema watu wote wako

sawa kwa sheria. Kwa hiyo, nasema hii sheria basi iwe mfano kwa wote na siyo kwa wanyamapori peke yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ukisoma sheria hii katika *Part* ya 4 inazungumza kwamba Rais anaweza akatangaza mahali popote kuwa ni mahali pa hifadhi *game reserve, national park* na mambo kama hayo. Sasa najiuliza hivi mpaka wake uko wapi? Dunia hii tunakokwenda haijulikani tutakuwa na Marais wa namna gani, tunaweza kuwa na Rais ambaye anapendelea zaidi wanyama kuliko binadamu na akaamua kwa mfano Sukuma land yote iwe *game reserve*, ndiyo sheria inampa madaraka hayo je, ukomo wake uko wapi?  Waziri anaweza kuamua hii *area* ndiyo mahali ambapo watapitia wanyama watu wote hameni, ukomo uko wapi? Ukiangalia madaraka ambayo yamewekwa kwa *Director* wa *Wildlife* ni makubwa sana. Nafikiri ni vizuri sasa tukaanza sasa kuiga baadhi ya nchi zingine, maamuzi ambayo ni makubwa yaletwe kwenye Bunge, isiwe kuwa Rais anaweza kutoa 1000 *square kilometre* kwa mwekezaji mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kama mwekezaji wa *Gulumeti Reserve* ana 1000 *square kilometre*. 1000 *square kilometre* ni karibu Wilaya nzima. Wilaya nzima imetolewa kwa mwekezaji mmoja na mwekezaji mmoja huyu ni ambaye ana wivu sana na wengine anataka akae peke yake tu. Hataki mtu mwingine aweke hoteli katika *game reserve,* hata hataki mtu mwingine apite kwenye barabara ambayo imo ndani ya *game reserve,* ni dunia yake tu peke yake. Sasa nashangaa kama sisi ambao ni majirani zake tukimwambia na yeye hatutaki magari yake yaingie katika vijiji vingine atakuwa anatoka kwenye *Gulumeti Reserve* anakwenda juu au atakwenda namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni tabia ya wapi?  Sisi tumeachiwa na wazee wetu waliotengeneza nchi hii kwamba uhusiano uwe mzuri bila ubaguzi, bila kuoneana kati ya majirani na kati ya watu. Hata Mwenyezi Mungu alipotengeneza hawa wanyama kuna simba, tembo,  swala wadogo, lakini wote wanaishi kwa pamoja bila kubaguana. Huu mtindo sasa ambao unaingizwa Tanzania kwamba tunatoa rasilimali ya Tanzania kwa mwekezaji mmoja na tunampa *exclusivity* matumizi yake yeye binafsi peke yake na wageni, hii tabia imetoka wapi? Imezaliwa na nani? Sisi hatujakuzwa hivyo na Mwalimu Nyerere. Hata Mwenyezi Mungu anasema pamoja na simba, pamoja na nini muishi pamoja. Kwa nini sheria hii inatoa mwanya kama huo ambapo mwekezaji akipewa mahali tena anapewa kuwinda anaamua siwindi, nitafuga lakini hapa ni mahali pangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri hii sheria haitoi haki kwa matumizi ya rasilimali tulizopewa na Mwenyezi Mungu. Kama ni *game reserve* iwe ruhusa kwa mtu yeyote ambaye anakwenda kuangalia wanyama na kupiga picha iwe ruhusa kwa watu wote ambao walio na makampuni ya kutembeza watalii na pasiwe hata kidogo na *exclusivity* ya mtu mwingine yeyote. *Hunting blocks* nafikiri tumezungumza hapa na Bunge hili linapofika kwenye *hunting blocks* linagawanyika. Hivi ni kwa nini tunagawanywa kwa kitu kidogo kama hiki?

Kwanza ukiangalia mapato hata ya utalii mwaka jana karibu bilioni 53 *hunting block area* ni hela kidogo sana. Halafu ukiangalia kusema kweli pasingekuwa na sheria inayokubalia watu wafanye *hunting* isipokuwa labda *hunting* kwa sababu ya kitoweo.

Kwa sababu ukizungumza juu ya *hunting* au unazungumzia juu ya kuua wanyama haendani sasa na *conservation* kama tumetaka kuhifadhi kwa nini tunaua, kama tunataka kuhifadhi kwa nini tunatengeneza utaratibu wa kwamba simba 30 tuwauze, tembo sasa hivi hawaendi. Lakini pundamilia kadhaa wauawe. Kama tumeamua kuhifadhi, tuhifadhi. Mambo ya kusema kwamba tunapewa fedha tu na tuthamini fedha kuliko uhifadhi na ukiangalia watu wenyewe wanaokuja kuomba kuwinda *actually* wanapatumia pale mahali kama mahali pa kuvuna tu kwa ajili yao. Ukiangalia mapato wala siyo mapato ambayo kweli yanaweza yakaifanya nchi hii iharibiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yangu kama ningekuwa na uwezo wa ku-*convince* Bunge hili ningesema tufute kabisa uwindaji wa kitalii na watu wote waweze kuruhusiwa kwenda kwa ajili ya utalii wa kuweza kupiga picha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamaliza nataka kuzungumzia juu ya *Wildlife Management Area*. Hii ninavyoona ni vizuri kwamba tuna *national park*, tuna *game reserves*, tuna *open areas* lakini na yenyewe sasa imetengeneza *Wild Management Area* kisingizio kwamba na ninyi wananchi muweze kuvuna. Lakini ukweli jinsi inavyotengenezwa kumbe ni njia ya kuwapa wawekezaji tena *area* kubwa zaidi. Huu mfano uko tayari, *Wild Management Area* ya Gurumenti, mwekezaji ndiyo ambaye amepewa mamlaka ya kumiliki pale mahali. Kwa hali hii tunafanya nini sasa? Kwa hiyo, mafao yote yale yanakwenda zaidi kwa mwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, hao watu ambao wanapelekwa katika hizi *exclusive areas* wanapewa na mamlaka ya kulinda. Hii mamlaka ya kulinda inakuwa ni kubwa zaidi. Kule kwangu Longalomboto, kule Ng’waswale, kule kwangu Bariadi hawa wawekezaji wanapigana na wananchi. Juzi Mwaswalo wamekamata ng’ombe 200, wamerusha risasi, baadaye wametoa amri lazima tulipe 100,000 kwa kila ng’ombe. Hawa wanakuwa pia wenyewe ni walinzi, wakati huo huo ni Mahakimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itoe amri kabisa, ukipewa kitalu huna mamlaka ya kujichukulia sheria mkononi, kama mtu anakuja mahali apelekwe Mahakamani na siyo kwa hali ambayo inakwenda hivi sasa. Kwa hiyo, ukiangalia jinsi ambavyo tunaendesha Idara hii ya Wanyamapori, zaidi inakuwa ni bughudha kwa wananchi na siyo msaada kwa wananchi. Kama tunataka wanyamapori wasigusane na ng’ombe basi tuweke *fence* kila mahali. Wanyamapori kule na sisi wananchi tuwe huku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi wamezungumzia juu ya fidia na inavyoonekana hapa ni kiini macho. Sheria hii inathamini zaidi mnyamapori kuliko ng’ombe, kuliko mazao ya wananchi. Hali hii haiwezi ikakubalika kwa Watanzania ambao wengi ni wakulima, wengi ni wafugaji. Tunataka sheria ihuishe namna itakavyoweza kuwalinda hawa wananchi. Hayo mambo ya kusema kifuta machozi futa kabisa, katika sheria hakuna cha kifuta machozi, hiyo ni *compensation* yaani ulipe kabisa fidia ya mazao yote, ulipe fidia kama umenivunjia nyumba na vitu kama hivyo. Sheria hii haijakaa vizuri ili kuweza kushabihiana na maisha halisi ambayo tunayo kwa sasa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, natoa wito, tusije tukaifikisha nchi hii mahali ambapo wananchi wakapigana kwa sababu ya wanyamapori au wanapigana kwa sababu wamebanwa. Huo ndiyo wito wangu. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cheyo tunashukuru sana kwa mchango wako.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika Bunge hili. Kwanza, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kusimama. Vilevile nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Ezekiel Maige, Katibu Mkuu wa Wizara hii Dr. Komba pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa maandalizi mazuri ya Muswada huu ambao umeletwa mbele yetu na unaoendelea kujadiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu una mambo mengi mazuri ambayo yataendeleza wanyamapori na wanyamapori ni zawadi tuliyopewa na Mwenyezi Mungu, kwa hiyo, tunatakiwa kuwalinda na kuwatunza. Tukiwalinda na kuwatunza tutafaidi kutokana na wanyamapori tulionao na tuna bahati kwa sababu nchi zingine hawakujaliwa na Mwenyezi Mungu bahati hii ya kuwa na wanyamapori na ndiyo maana wanakuja Tanzania kuwawinda na kuvuna na kupiga nao picha na kutokana na utalii huo tunapata mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mapato tunayoyapata, uendeshaji wa wanyamapori ni gharama, unahitaji fedha na siyo fedha kidogo, ni fedha nyingi. Fedha zinazotokana na uwindaji wa kitalii ndizo zinazosaidia katika uendeshaji na uendelezaji wa wanyamapori katika mapori yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara haitaki siasa, tukubaliane kwamba biashara haitaki siasa na biashara ya uwindaji wa kitalii ni biashara ya Kimataifa na tukubaliane kwamba Serikali lazima iwe na msimamo katika kufanya biashara ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Idara ya Wanyamapori kwa mwaka huu wa fedha ilikuwa shilingi bilioni 12, shilingi bilioni 6 zilikuwa zinatokana na uwindaji wa kitalii, na shilingi bilioni 6 zilitoka Wizara ya Fedha. Lakini cha ajabu ni kwamba Idara hii imepewa bilioni moja tu kutoka Hazina. Kwa maana hiyo, bila uwindaji wa kitalii Idara hii itakufa na haitatekeleza majukumu yake. Kwa hiyo, ukiua uwindaji wa kitalii ina maana uendelezaji wa wanyamapori utakwisha. Kwa hiyo, naomba Wizara au Serikali kuijipanga vizuri kukabiliana na athari zitakazotokana na maamuzi ya kisiasa ambayo yalitolewa muda siyo mrefu na Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchangia kifungu cha 9(1) kinachomruhusu Mheshimiwa Waziri kuunda kikosi maalum cha kupambana na ujangili. Ni wazo zuri na nampongeza Waziri kwa maamuzi hayo kwa sababu wanyama wanatakiwa kulindwa, tusipowalinda watakwisha maporini huko waliko kwa kuuawa na

majangili. Kwa hiyo wanahitaji kulindwa kwa sababu wakimalizika kwa kuuawa na majangili majangili mapato tunayotegemea kuyapata kutokana na uwindaji hatutayapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kitu ambacho nakitahadharisha ni hali waliyonayo Maaskari wetu au wafanyakazi katika maeneo ya wanyamapori. Nilitembelea eneo la Selous muda siyo mrefu, nikakuta wanadamu wanaishi na wanyama kule, tembo wanatembea kwenye mazingira ya binadamu, ngiri wanakaa milangoni kwa Maafisa wa Wanyamapori kule, wanatafuta maji na Maafisa wanaoishi kule hawafungi madirisha, ukifunga dirisha tembo anakuja anavunja dirisha akitafuta maji. Hebu fikiria mazingira hayo wanayoishi Maaskari wa wanyamapori, wanaishi maisha magumu, wanachangia maji na wanyamapori. Kwa hiyo, kama Serikali haitaweka mazingira mazuri kwa hicho kikosi kinachopambana na ujangili hao Maaskari hawatawapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa niliyonayo ni kwamba, Maaskari hao walikuwa wengi zaidi ya 800, lakini wamepungua kutokana na mishahara midogo wanayopewa na hali ngumu wanayoishi. Naishauri Serikali, pamoja na nia nzuri ya kuanzisha kikosi hiki, lakini waangalie namna ya kuwapa motisha hawa Maaskari ambao wanaishi katika maisha magumu kule maporini waliko, wapate usafiri, wapate maji na wapate nyumba nzuri za kuishi. Kwa sababu ya ufinyu wa bajeti, hao watu katika maeneo mengine hawana hata maji ya kunywa na maji wanayochimba katika mitalo tembo sijui ndovu akienda kule anafukia au wanawafukuza binadamu kwa ajili ya kupata maji.

Kwa hiyo, hebu waangalie namna ya kuwapa motisha hawa watu, kuishi porini siyo kazi ndogo, kuishi porini ni kazi kubwa. Lakini nia ni nzuri na lengo ni zuri, tuwapate vijana wakafanye kazi kule. Waliopo ni wazee ambao wanakaribia kustaafu, watakapostaafu hao waliopo wanyama wetu watalindwa na watu gani kama mishahara na motisha haitaboreshwa kwa hao ambao wapo kwa sasa na kwa watakaoajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie tena katika Kifungu 91 kinachohusu kuundwa kwa Bodi ya Wadhamini. Bodi hii imepewa madaraka makubwa, imepewa madaraka ya kisheria, *legal personality*. Bodi hii ina uwezo wa kuingia mikataba mbalimbali, Bodi hii ina uwezo wa kuwekeza vitega uchumi, Bodi hii inaweza kushtaki au kushtakiwa, Bodi hii pia itakuwa na nembo yake na Bodi hii imepewa madaraka ya kutunza mahesabu na kuhakikisha kwamba mahesabu yake yapo sahihi na yanakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali yaani *CAG*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nia ni nzuri na lengo ni zuri na madaraka waliyopewa wakiyatumia vizuri tunategemea kwamba Idara hii ya Wanyamapori itafanikiwa kwa hali ya juu sana. Lakini kitu ambacho nimekiona kwamba kina upungufu kidogo katika Bodi hii. Bodi hii haikupewa mamlaka ya kuajiri, haina mamlaka ya kuajiri pamoja na madaraka makubwa iliyopewa, wanaweza kushtaki au kushtakiwa, wanaweza kuingia mikataba ya vitega uchumi, wana nembo yao, wana mambo mengi sana kama mhimili wa Idara hii ya Wanyamapori, lakini hawakupewa mamlaka ya kuajiri.

Mheshimiwa Spika, sasa kama hawakupewa mamlaka ya kuajiri hesabu hizi zitakamilishwaje zikawa sahihi na zikakaguliwa na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali na akapelekewa Waziri wa Maliasili na Utalii na Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii atakayaleta Bungeni yakiwa mahesabu sahihi na kama huyu ambaye ni Mhasibu wa Idara kama atakosea atawajibika kwa nani kwa sababu hawajibiki kwa Bodi ya Wadhamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Idara hii itakosa watumishi ambao ni wataalam wanaohitajika kwa muda huo, hebu tuulizane Bodi hii itafanyaje kuwapata waajiriwa hao? Au ni mpaka waombe Serikalini na kama Serikali itakuwa imesitisha ajira kwa kipindi hicho ina maana Idara ya Wanyamapori itaendelea kukaa bila watumishi ambao wana uwezo wa kufanya kazi katika Idara mpaka hapo Serikali itakapoamua. Naomba sasa au nashauri Serikali itoe madaraka kamili kwa Bodi hii ili iweze kuajiri, iweze kuadhibu na iweze kufanya yote kama ilivyopewa mamlaka mengine ya utendaji kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia na niseme kwamba naunga mkono Muswada huu. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niungane na wenzangu kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Muswada huu ambao upo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda niishukuru Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kuwasilisha Muswada huu ambao binafsi sina uhakika sana kama Muswada huu utakidhi changamoto zilizopo sasa hivi kwa sekta ya maliasili na hasa wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita sana katika kutoa mifano katika Wilaya yangu ya Mpanda. Wilaya ya Mpanda eneo lake ni zaidi ya Mkoa wa Kilimanjaro na Tanga kwa pamoja. Lakini Wilaya ya Mpanda asilimia 63 ni misitu. Ndani ya misitu hiyo kuna maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya wanyamapori kama *game controlled areas*, *game reserve* na pia hifadhi ya Taifa ya Katavi. Kwa hiyo, sisi ni wadau wakubwa sana katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusudio ya sheria hii yangekuwa na maana sana kama sheria ingetamka bayana kabisa wananchi wananufaika vipi kutokana na hawa wanyamapori. Kama sheria haiwezi kutamka bayana na ikaacha mamlaka hayo kwa Waziri tu ambaye anapanga kanuni za namna ya kugawa mapato yatokanayo na wanyamapori bado wananchi tutakuwa hatujawatendea haki hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana sana na Waheshimiwa wenzangu ambao wamesisitiza umuhimu wa kuanzishwa mamlaka ya wanyamapori. Ziko faida nyingi ambazo tutapata kwa kuanzisha mamlaka hii ya wanyamapori. Nikitolea mfano kutokana na takwimu za Kiserikali kwamba *TANAPA* wanatumia karibu Dola 1100 na kidogo kwa ajili ya uhifadhi wa wanyama kwa kila *square kilometre* moja wakati Idara ya Wanyamapori inatumia Dola 24. Kwa hiyo, ni dhahiri kabisa tukiwa na mamlaka itatenga fedha za kutosha katika kuhifadhi wanyama kama wanavyofanya Shirika la Hifadhi ya

Taifa (*TANAPA*). Kwa hiyo, nadhani ipo sababu ambayo inatupelekea kwa nini tunaitaka Serikali ianzishe mamlaka ya wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukitazama Muswada huu umelenga sana katika kuhifadhi wanyamapori. Hebu tutazame, ni kweli tunahifadhi wanyamapori au tu ni kuendeleza kuwa na sheria zinazotamka kuhusu kuhifadhi. Nina mashaka sana kama kweli tuna dhamira ya kweli kweli katika kuhifadhi hawa wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu wakati tunapata uhuru tulikuwa na Hifadhi za Taifa tatu, leo tuna hifadhi karibu 16 hivi. Lakini tutazame kweli maana ya kuhifadhi ipo. Nichukulie mfano hifadhi ya Katavi, Hifadhi ya Katavi ina eneo karibu *square kilometre* 4417 hivi, lakini ina Askari wasiofika 70 wapo kati ya 60 na 65 hivi. Kwa maana hiyo kila Askari mmoja kule Katavi anawajibika kulinda eneo la *square kilometre* 60800. Sasa hiyo basi ni afadhali katika Hifadhi ya Taifa. Hebu tazama pori la Rungwa Lukwati *game reserve* ambayo ina eneo karibu mara mbili ya ukubwa wa Hifadhi ya Katavi, karibu *square kilometre* 7000 ina Askari 35. Ni kweli tuna dhamira ya kutaka kulinda na kuhifadhi wanyama hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa undani kabisa, kwa mfano, unapotazama matatizo ya Rungwa Lukwati inasikitisha sana. Kwanza wale Askari wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Baada ya ule mradi uliokuwepo wa Katavi, Rukwa *conservation development problem* kwisha mwaka 2006 watumishi wale wanaishi katika hali ngumu sana. Hawana vitendea kazi, mradi ule ulijenga majengo mazuri sana kule Mlele lakini hayatumiki, hakuna Askari, hakuna huduma za kijamii na ni mbali kutoka Mpanda Mjini ambapo wanapata huduma zao za msingi za kibinadam. Watu hawa kwa sababu kule hakuna shule, hakuna zahanati wanalazimika kuweka familia zao mjini. Kwa hiyo wana gharama za kutunza familia zao ambazo zimebaki mjini na kujitunza wenyewe wakati wakiwa kule porini. Mishahara haitoshelezi kukidhi hali hiyo ambayo inalazimishwa na mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni lazima tuangalie maslahi ya hawa watumishi wanaojitolea kufanya kazi za uhifadhi kwa sababu wanafanya kazi katika mazingira magumu, hawana namna nyingine yoyote ya kujiongezea kipato chao zaidi ya mshahara. Kule Mlele hawezi kufungua *grocery*, hawezi kufuga kuku wala ng'ombe wa maziwa, anachotegemea ni mshahara tu. Kwa hiyo watumishi hawa wanaishi katika mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata magari ya kufanyia kazi hawana. Pori kubwa kama hilo ambalo limechukua Wilaya ya Mpanda na Chunya, kutoka Mlele mpaka ufike Chunya ni zaidi ya kilomita 400. Watu hawa wana gari moja halafu nyinyi mnakaa mnasema tunahifadhi, tunahifadhi kitu gani? Ujangili katika eneo hilo ni mkubwa sana, eneo hilo wakati huu wa masika halipitiki. Sasa ni lazima tuangalie tunawekeza kiasi gani katika uhifadhi wa wanyama ili dhamira ya kuhifadhi iweze kutimia. Vinginevyo tutakuwa tunapiga hadithi tu na tunaandika maneno mazuri ya kupendeza, mtu akisoma kitabu anaona kweli tuna dhamira wakati tunashindwa kutekeleza yale tunayokusudia kuyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wa Idara ya Wanyamapori wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Nimeeleza waliopo pale Katavi na waliopo katika Mradi wa Rukwa Lukwati lakini ukiitazama Idara yenyewe katika Wilaya nzima ya Mpanda ina Askari wa Wanyamapori 11 ambao wanaangalia *controlled areas* karibu 9 ambazo ziko pale. Kuna Mlele, Msima, Ugalla ni nyingi Askari wako 11, wanafanyaje kazi hao? Katika maeneo ambayo ukiachilia mbali *game reserve* na *National Park* maeneo mengine tu ya wanyama ni zaidi ya *square kilometres* 12,000 katika Wilaya ya Mpanda. Wale Askari 11 pale Wilayani hawana gari wanategemea waende wakaombe, Mkurugenzi atazame gari ya elimu au maji wawape waende kufanya doria. Kwa hali hiyo, hatuwezi kufika katika malengo tuliyokusudia katika kuhifadhi wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na hilo kuna vitalu vya kuwindia kule Mpanda. Lakini tukijiuliza kwamba tunafaidika vipi watu wa Mpanda na uwindaji wa kitalii hatuna majibu kuhusu hilo. Hakuna mtu yeyote anayeona faida ya moja kwa moja wanayoipata wananchi wa Mpanda kutokana na uwindaji wa kitalii. Pamoja na kwamba takwimu zinaonesha kuongezeka sana kwa ukuaji wa uwindaji wa kitalii ukiangalia kwa mfano mwaka 2005 tulipata zaidi ya dola 250,000 na leo mwaka 2008 ni karibu dola 750,000. Lakini tunanufaika vipi watu wa Mpanda kutokana na uwindaji huu wa kitalii? Hiyo asilimia 25 hatuipati, haifiki na kama ikifika basi inafika pungufu. Kwa hiyo, inafikia mahali wananchi hawaoni faida wanayopata kutokana na kuwepo kwa hao wanyamapori na hata leo mkisema mnafuta uwindaji wa kitalii kwa watu wa Mpanda watashangilia kwa sababu hawaoni manufaa ya kuwepo uwindaji huo wa kitalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia pia katika eneo hilo hilo la kitalii kuna zaidi ya Makampuni matano yanayofanya kazi kule Mpanda, lakini katika hayo Makampuni matano, ni moja tu ya Saidi Kawawa ndiyo Mtanzania, Makampuni yote ya wageni. Kwa bahati mbaya sana ni mgeni huyo huyo mmoja anasajili Makampuni matatu katika nchi hii. Mtu huyo huyo mmoja anasajili Makampuni matatu kwa majina tofauti na anapewa vitalu na anawinda, tunakwenda wapi jamani? Ni lazima eneo hili tuliangalie na nashauri kama inawezekana hiki kipindi cha mpito basi kiongezwe hata kifikie miaka mitano ili tuweze kujipanga vizuri tuone kama tunanufaika na uwindaji wa kitalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kenya hawawindishi, Uganda hawawindishi, sisi tuna lazima gani ya kuwindisha. Ni lazima tuangalie ni namna gani sasa tutakuza utalii wa kupiga picha. Simba mmoja anaweza kupigwa picha na watalii 50 mpaka 100 au zaidi lakini simba mmoja atauawa na mwindaji mmoja. Hata kama tunapata mapato kidogo kwenye utalii wa kupiga picha, tukitengeneza mazingira mazuri ya kuvutia tunaweza tukafidia pengo tutakalolipata kutokana na kuwaua hawa wanyama. Nadhani ni lazima tujiangalie katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, Serikali isiyabane sana haya Mashirika yetu ili yaweze kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa na hasa Shirika la Hifadhi za Taifa kwa maana ya *TANAPA*. *TANAPA* inalipa kodi Serikalini, mwaka jana imelipa karibu bilioni nne, lakini bado unakuta huyu *TANAPA* analazimishwa kulipa gharama nyingine ambazo si za kwake. Juzi Serikali ilifanya maamuzi mazuri, nayapongeza sana ya

Hifadhi ya Usangu, lakini *TANAPA* wamelazimishwa kulipa fidia, kwa nini *TANAPA* ilipe fidia? *TANAPA* ina majukumu yake ya kufanya katika hifadhi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake leo wanashindwa, wanapunguza bajeti katika hifadhi zao, watumishi katika hifadhi wanaishi katika mazingira magumu sana. Vitendea kazi vya kutosha hakuna kwa sababu Serikali inaendelea kulitwisha mzigo Shirika hili la *TANAPA*. Haya Mashirika na Mamlaka tutakazozianzisha zipewe uhuru wa kufanya kazi na maamuzi yao. Pale Serikali inapohitaji kodi kama inastahiki kulipa kodi zilipe kodi na zisiongezewe tena mizigo mingine ili waweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, nitakuwa sikutenda haki kama sikuzungumzia *WMA*. Mradi ule wa *KRDC* ulikuwa na mpango wa kuanzisha *WMA* nne kule Mpanda katika eneo la Mradi. Mpaka sasa hivi *WMA* mbili ya Mpwimbe na Ubende mpaka leo zimeshindwa kufanya kazi wala hazina *user's right* kwa sababu ya urasimu katika Wizara ya Maliasili. Watu hawa wanahitaji kusaidiwa, watu wa Mpimbwe, Inyonga, Stalike ambao wanazungusha hifadhi wapewe msaada ili hizi *WMA* zao ziweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa yale niyaonayo yanafaa katika Muswada huu ulio mbele yetu. Kwanza, napenda kuwapongeza Waziri wa Maliasili, Naibu Waziri wake pamoja na Katibu Mkuu kwa kuuleta Muswada huu na katika hili nataka kuwaambia toka mwanzo kabisa kwamba nauunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umesubiriwa kwa siku nyingi kwa sisi tunaoufahamu kwa undani wake kwa kweli umeandaliwa kwa miaka mingi sana na sasa tunashukuru kwamba ni Muswada mmoja ambao kama ukiusoma sawa sawa utauona kabisa ni wa Kimapinduzi. Nitasimulia kidogo uanamapinduzi huo lakini ningeomba kwanza maana wanasema *charity begins at home*. Katika kuchangia kwangu, kwanza naomba Wizara ifanye utaratibu wa kuanzisha Hifadhi ya Taifa kule Kusini. Pale tunayo mapori mawili ya akiba *game reserve*. Moja iko Lukwika, Nanyumbu na nyingine Msanjesi katika Wilaya ya Masasi. Ni mbuga kubwa lakini kwa bahati mbaya mpaka sasa hivi hakuna hata mbuga moja iliyopandishwa daraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi majuzi katika kikao cha *RCC* cha Mkoa wa Mtwara tulizungumzia jambo hili na Mkoa ulipendekeza kwamba mbuga ya Msanjesi ipandishwe iwe *National Park* yaani tuiombe Wizara ya Maliasili iipandishe hadhi mbuga ile ili iwe *National Park.* Tunasema hivi kwa sababu katika Mikoa ile ya Kusini kusema kweli tuna utalii mkubwa zaidi wa fukwe na pia utalii wa mambo ya kale. Sasa kama tungeweka pia *National Park* ambayo watalii hawa baada ya kutoka *beach* wangeweza kwenda kupumzika kule kwa kweli lingekuwa ni jambo la busara sana. Naona wakati tunavyopitisha sheria hii na ili tuitumie vyema basi Waziri utangaze kwamba Msanjesi itakuwa nayo ni *National Park. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine kwa sababu kule Kusini hatuna hifadhi yoyote ya Taifa kuna baadhi ya maendeleo yanayokwenda kwa haraka sana hasa ujenzi wa miundombinu na kadhalika. Kwa hivi sasa barabara ndio zinafikafika Mtwara, magari mengi yanafika kwa wakati, watalii nao wanakuja. Tuna Kampuni hii ya *ARTMUS,* kusema kweli nashukuru *ARTMUS* wamefikia mahali pazuri pa kupeleka umeme kwenda Masasi na tunategemea mwaka huu bila shaka umeme utawaka vizuri pale Masasi na sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika pendekezo langu la kufanya Msanjesi iwe Hifadhi ya Taifa, nilikuwa naomba kwamba *TANAPA* basi ijiandae kuwaomba *ARTMUS* wapeleke umeme mpaka Msanjesi. Kwa sababu kama Msanjesi itakuwa *National Park* lazima kutakuwa na mahoteli mengi na kadhalika. Kwa hiyo umeme huu unaokwenda sasa hivi Masasi basi njia zake zifike mpaka Msanjesi ili tuweze kupata faida hiyo. Kwa wakati huo huo, wakati tunakwenda Msanjesi basi wenzetu wa Mbonde, Namkungwi, Namajani, Namatutwe, Chingulungulu mpaka Msanjesi wenyewe wote wapate umeme. Kwa hiyo vijiji hivi navyo vitaamka kitaliitalii. Kwa hiyo hayo mambo ndiyo ya kimaendeleo tunayotegemea kwamba lazima Wizara itatusaidia. Kwa hili kwa kweli tunasema sisi mbuga tunazo na wanyama wapo, kilichobaki ni taratibu tu, tutengenezeeni *National Park* ili maendeleo hayo yawepo katika Mikoa ya Kusini na watalii waweze kuhitimisha safari zao kwa kwenda kuwaona wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ebu sasa nigeukie kwenye Muswada huu ulio mbele yetu na nitoe *comments* zangu katika mambo machache ambayo nimeyaona zaidi. Lipo suala la fidia au *compensation,* kwa bahati nzuri hili lipo katika Muswada. Lakini ningewasihi Wabunge wenzangu tukiweka kiasi cha fedha ambacho kitaonekana katika sheria hii haitatusaidia sana kwa sababu kadri muda unavyopita thamani ya shilingi inapungua. Kwa mfano, zamani ilikuwa kwamba mtu akiuawa na simba au ndovu anapata kifuta machozi cha shilingi 50,000. Shilingi 50,000 miaka ya 1980 ilikuwa ni fedha nyingi sana, lakini leo shilingi 50,000 si kitu si chochote. Kwa hiyo, kuweka hii katika sheria naona haitaweza kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha maana ambacho tukiweke ni kwamba iwepo kwenye *regulations* kwa sababu kanuni huwa zinabadilika kila wakati, hapo ndio tukijite kwamba katika kanuni atakazotengeneza Waziri ni lazima kuwepo ama fidia ama kifuta machozi na hiki kiwe kinabadilika kwa miaka kadhaa kadri hali ya uchumi inavyoendelea na kadri Tanzania inavyoendelea pia. Tusijifunge sasa hivi kwa kuonyesha kwamba tunataka kiwekwe kiasi fulani. Kwa hiyo, ningeomba sana Wabunge wenzangu tukubaliane katika hili kwamba iwepo kwenye *regulations.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nililotaka kulizungumzia ni kuhusu suala la uwindaji wa kitalii. Kwa bahati nzuri nipo katika Bodi ya Utalii, kwa hiyo nina bahati ya ufahamu mkubwa zaidi katika suala hili na wakati huo huo ni lazima ni-*declare interest* kwamba nipo pia katika Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii pamoja na Mazingira. Hili limeletwa kama hoja binafsi iliyoletwa vizuri sana na mtoa hoja na baadaye hatimaye Bunge likakubali. Kwanza katika hili nimpe pole Mheshimiwa

Waziri kwa dhoruba iliyotokea wakati hoja hii inaletwa na pia baadaye kwenye magazeti kwa jinsi yalivyoandika na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tu kwamba katika siasa haya ni kama mawimbi yaliyopo kwenye chai hasa chai ile ya Kitaliano inayoitwa *cappuccino* ikiwekwa inakuwa na dhoruba hasa. Sasa dhoruba ile isikukatishe tamaa, maji yale yananyweka ni chai. Sasa yale yaliyotokea siku ile basi yachukuliwe tu ni kama sawa na kwamba kulikuwa na dhoruba iliyotokea kwenye chai ambayo inanyweka tu na sasa tuinywe vizuri tena bila wasiwasi wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili nafahamu kwamba ili biashara ya uwindaji wa utalii iweze kwenda vizuri mtu anahitaji sio chini ya vitalu vinne. Kwa kweli ni ghali na kwa Watanzania wengi si rahisi, ndiyo maana hivi sasa tunayo Makampuni 13 ya kigeni na kati ya hayo nafikiri ni manne ndiyo ya Waswahili wenzetu. Kwa kweli tulihitaji muda wa mpito na kwa sababu tumepitisha kwamba iwe miaka miwili sijui jinsi Waziri atakavyofanya, labda atatueleza baadaye wakati ana *summarise* kwamba jinsi gani atafanya, lakini kwa kweli kipindi cha miaka miwili kitakuwa ni kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kuna madhara ambayo nayaona na ambayo nafikiri Bunge hili lifahamu. Kwanza ninachokiona ni kwamba, Kampuni zilizoingia Mkataba na Serikali kwa vyovyote vile huenda watasusia kuingia mikataba mipya na huenda hata Kampuni hizo zikaleta *court injunction* kwa Serikali kwa sababu kuna mikataba iliyokuwa inaendelea, sasa hii ni hatari, inaweza ikachelewesha mambo mengi kwa muda mrefu. Kwa hiyo, naomba Waziri ujiandae kwa sababu kama wakileta hizi *court injunction* maana yake shughuli zile za uwindaji wa kitalii hazitakuwa zinafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo ni lazima tutegemee kutakuwa na upungufu wa mapato kutoka Serikalini. Kama wenzangu walivyosema mpaka hivi sasa Idara yetu ya Wanyamapori ilikuwa inajiendesha yenyewe kutokana na uwindaji huu wa kitalii. Sasa kama usipoendelea vizuri kwa vyovyote vile Serikali ijiandae kuhakikisha kwamba inatoa au inapanga fedha kwa ajili ya kuendesha Idara ya Wanyamapori ambayo hapo zamani ilikuwa inaweza kujiendesha yenyewe na pia Serikali ijiandae hata kushtakiwa Mahakamani na hivyo kutoa mabilioni ya fedha kwa sababu ya uvunjaji wa ile mikataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba kwamba wimbi hili lisimamiwe vizuri na naliomba Bunge baada ya kupitisha Maazimio yake iiachie sasa Idara pamoja na Wizara iweze kutekeleza mambo mbalimbali. Ikiwa sisi tutakwenda mpaka jikoni kule kuwaelekeza sijui namna gani watengeneze kanuni, taratibu na kadhalika kwa vyovyote vile hili linaweza kuwa na madhara ambayo niliona kwamba afadhali yajulikane katika Bunge hili. Tusipoangalia vizuri hata ujangili unaweza kurudi kwa sababu Makampuni haya mengi yalikuwa yanafanya kazi nzuri ya kuzuia ujangili. Sasa majangili watakavyoona kwamba uwindaji ule wa utalii haupo wanaweza wakarudi kwa nguvu katika *game reserve* zetu na hasa katika Hifadhi za Taifa. Sasa hili nalo naomba Waziri baadaye labda wakati anamalizia hotuba yake atuelezee ni mipango gani itakayofanyika ili kuhakikisha kwamba mambo haya hayaiathiri nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa niseme tu kwamba nawapa pongezi, hongera kwa kazi nzuri, Muswada huu tuutetee na upite bila ya wasiwasi na kama nilivyosema, nauunga mkono. (*Makofi*)

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Muswada huu ambao uko mbele yetu. Naungana na wenzangu kwanza kuipongeza Wizara kwa kuweza kufanya marekebisho na hatimaye kuuleta Muswada mbele ya Bunge lako Tukufu. Naamini baada ya kusikia michango mingi ambayo Wajumbe wa Kamati walisema na kupitia vifungu kwa vifungu wenzetu wameuchambua Muswada huu kwa makini na nipongeze kwa kazi ambayo wameifanya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita zaidi kwenye mapato ambayo yanatokana na Idara hii ya wanyamapori kwa maana ya *game reserve*. Nasema nina uzoefu kwa sababu kwenye Wilaya yangu kumekuwa na vitalu vya uwindishaji kwa muda mrefu na sasa naondokana huko baada ya dharura ambayo ilitokea. Serikali iliona kwamba lile pori la hifadhi sasa lipandishwe kutoka kwenye *game reserve* kwenda kwenye Hifadhi ya Taifa kwa maana ya *National Park.* Lakini nina masikitiko makubwa sana kwamba, hii sheria inaonekana sasa imeweka nguvu zaidi kwamba tutakusanya mapato kwa wingi na kwa maana hiyo asilimia 25 tunayoizungumzia sasa itakuwa kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema hapo mwanzo kuwa tumekuwa na vitalu tangu sheria inaanza mwaka 1974, Mbarali tumekuwa na uwindishaji vitalu vya uendeshaji lakini kama wenzangu wanavyolalamika hapa kiwango kikubwa sana ambacho wamekipata ni shilingi 16. Sasa labda Waziri atueleze inawezekana wengi hatuelewi hiyo asilimia 25 inatokana na nini, tunatofautiana kwenye Wilaya ambazo kuna vitalu vya uendeshaji au hiyo asilimia 25 inatokana kwenye vitalu ambako mapato yanayokusanywa kwa mwaka halafu ndiyo unapata hiyo asilimia 25 ili tuweze kujua kwamba ni kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukipitia kwenye Kamati zetu za Hesabu, unakuta Idara ya Wanyamapori imekuwa ikilalamika kwamba mapato mengi yakienda Wizarani au Serikalini hayarudi kwa ajili ya kuhudumia Idara yenyewe kwa maana ya wafanyakazi wao na nina uzoefu huo ambao mwenzangu hapa amesema kwamba kule tunahitaji Askari wa wanyamapori ambao wanazunguka na kulinda majangili, lakini utashangaa sana kazi wanayoifanya ni kazi ambayo ni kama ya kinyama. Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza haya kwa uchungu sana kwamba kutokana na kipato kidogo wanachopata Askari. Wakikaa kwenye hifadhi, akipita mwananchi yeyote kwa bahati mbaya au labda ni mtu ambaye ni jangili sheria imewekwa kwamba kuna adhabu, kuna kifungu kuna pesa ya kutoa lakini wamekuwa wakijichukulia sheria zao mikononi, maana yake mtu akishikwa kama ameshikwa na samaki atalishwa samaki mbichi, yaani wanakuwa na hasira. Sasa kama kipato kingekuwa kinarudi kule Idara ya Wanyamapori na wale Askari wa wanyamapori wakalipwa vizuri wakawa na maisha mazuri naamini huu ukatili usingekuwepo. Adhabu zile Waziri kama hana habari kwa kweli ni kali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wengi hawajapata hiyo elimu, wanasema nikaokote kuni, nikavue samaki, nikafanye nini, lakini madhara yake wanayoyapata ni makubwa sana. Kwa hiyo, hilo nalo lizingatiwe na nilitaka niulize kwamba, je, ukiweka ekta 5,000 kwa ajili ya wanyamapori na ukaacha lile pori likawa kwa ajili ya mifugo utapata shilingi milioni nane? Sasa kwa faida hii kweli Serikali iko makini katika kufuatilia na kuona haya mapato yanapatikana. Hii hifadhi ni kwa ajili ya manufaa ya kwetu sisi Watanzania au kwa ajili ya wenzetu wa nje ambao wamepewa hivyo vitalu? Sasa Mheshimiwa Waziri hii ni *challenge* umetuletea, hii sheria umeweka mambo mazito, tunaamini sasa faida yake ni kuona mapato ya vitalu hivi yanaongezeka mara mbili au zaidi kuliko yalivyokuwa hapo mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipitia hii sheria, kuna baadhi ya vifungu ambavyo ningependa nizungumzie. Inaonekana sasa Serikali imeelekea zaidi kwenye kulinda wanyama kuliko hata wananchi wanaozunguuka mazingira yale na hatukuangalia hali halisi ya maisha ya Watanzania ambao wanaishi kwenye hivyo vitalu. Kwa mfano, nilikuwa naangalia hiki kifungu cha 74 kinachozungumza kwamba kwa bahati mbaya unataka kujihami mwananchi akamuumiza mnyama, yeye ataonekana ni mhalifu na atachukuliwa adhabu ile ile kama mtu ambaye alikuwa amekwenda kama jangili kwenye hifadhi ya wanyamapori. Kweli kwa maisha ya sasa kwa Watanzania na sisi wengine ambao ni Wabunge hapa tunaotoka kwenye maeneo hayo yenye vitalu au yenye hifadhi ya wanyamapori tunajua jinsi watu wetu walivyo, huenda wakaingia pale na bahati mbaya akakutana na mnyama pale akasema nijihami, sasa anapata adhabu ya kuumizwa na mnyama na yeye akijikinga atakwenda jela sawa na wale wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna kifungu cha, kifuta machozi, kinazungumzia utapewa tu kama utakuwa umeumizwa na mnyama ambaye ni hatari. Maana yake unasema *dangerous animal* na wameweka kwenye s*chedule* namba nne. Sasa ukisoma ile *schedule* wale wanyama ni wachache sana, naamini wanyama wengi ni wa hatari. Ukisema hata duma, mbwamwitu ni hatari lakini sasa wanyama waliotajwa pale ni wachache. Labda Mheshimiwa Waziri atuambie je, kutakuwa na *regulation* huko itakayozingatia kwamba utakuwa unatangaza kila wakati ni mnyama gani tena anaongezwa kwenye orodha ya *schedule* ya wanyama ambao ni hatari ambao atapaswa mwananchi akiingia kwenye hilo eneo kwa bahati mbaya akaumizwa atapewa fidia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalotaka kuchangia ni kama ambalo ameongelea Mheshimiwa Mtutura hapa, la mnyama au wanyama wakienda kuharibu shamba. Tunaelewa mashamba ya wananchi wetu, akiharibu eka 10 au 20 lakini atapewa fidia ya ekari tano tu, kweli ni hali halisi hiyo? Si unyanyasaji huo. Kwa nini hatuthamini wale wakulima au wananchi wanaokuwa wametoa ile sehemu kwa moyo wa dhati kabisa kwa ajili ya manufaa ya nchi nzima au kwa ajili ya watu wote? Leo bahati mbaya ndovu wameingia wamevuruga mahindi eka 10 au 20 unamwambia utakuwa *entitled for* kulipwa eka tano tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba tupate maelezo, inawezekana labda hatujaelewa vizuri au iko kwenye *regulation,* sisi tukiipitisha hii sheria angalau tujue tunapitisha kitu ambacho kitakuwa na manufaa kwa sisi wote na kuleta *harmony* kwa

wananchi wetu na manufaa kwa sisi wote na kuleta *harmony* kwa wananchi wetu ambao wanazunguka sehemu hizo za uendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalotaka kuzungumzia hapa ni kwamba, Wizara ya Maliasili na Utalii wenzetu sisi ni wakulima na wafugaji na hiyo Wizara ni ya kwetu, ifike wakati sasa wasiwe na uhuru tu wa kuongeza maeneo kwa sababu wanasheria, naona kama Kilimo, Mifugo hawana Sheria, kwa hiyo wanaweza wakahamishwa wafugaji wakaletwa Wanyamapori, wakahamishwa wakulima wakaletwa wanyamapori. Kwa hiyo, tuhakikishe kwamba hivi vitu vinakwenda sawa, kwa mfano, wanyamapori, kilimo na mifugo kama ng'ombe ni vitu ambavyo vinategemea kuleta uchumi katika nchi hii na vinaondoa umaskini kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Mbarali tumeongeza lile eneo vizuri lakini *compensation* ya wananchi ni ndogo sana. Wafugaji wameondolewa, wakulima wameondolewa kwa eneo kubwa sana. Eneo la hekta 400 ukatoa 5000 ni eneo kubwa sana, ni karibu asilimia 30 ya Wilaya nzima ya Mbalali. Ukija kwenye fidia ambayo mwananchi amepewa, ni kidogo sana. Leo unamwambia hata mazao yake kama yakiharibiwa bado atapewa fidia kwa kiwango kidogo sana. Kweli atakuwa na amani ya kutunza eneo hilo? Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri la kwanza ambalo limenifanya nichangie hapa kikubwa zaidi nafikiri ni wakati muafaka kwa Wizara yako kuleta *regulations* au kubadili Sheria ya viwango vya fidia sasa. Fidia kwa ajili ya kupisha Hifadhi za Taifa na fidia ya kupisha vitalu kwa sababu mtazidi kutafuta maeneo mbalimbali. Sasa tuwe na viwango vipya ambavyo vitakidhi haja ya hali halisi ya Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna kilio ambacho ni kikubwa tu kule Mbarali kuhusu fidia walizopewa watu, wengine wamepewa shilingi 50,000/-, unaacha Mji wako, unaacha shamba lako unapisha kitu ambacho unasema ni faida kwa nchi hii, lakini kilio hicho mpaka sasa hakijafikishwa mbali na wale Watanzania bado hawajasikilizwa. Kwa hiyo, ninachomwomba Mheshimiwa Waziri sasa, fidia kwa ajili ya kuwahamisha watu wanaopisha hizo hifadhi iongezwe na iletwe hiyo Sheria. Pili, fidia kwa ajili ambayo umeizungumza kwenye *regulation* utakapoleta kwa asilimia kama alivyosema Mheshimiwa Mrope si kwa kiwango, ni kwa asilimia kwamba ni asilimia ngapi huyu mtu apewe kama fidia na si kifuta machozi ambapo na mfiwa atafarijika kwa kiasi ambacho amepewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka niseme ni kwa upande wa uwindishaji wa vitalu. Hivi hawa tunaowapa vitalu wanaokuja kuwinda, hesabu zake kwamba amewinda wanyama wangapi, amelipa kiasi gani, kuna mkakati gani umewekwa? Kama tumemwambia awinde tembo mmoja au nyati mmoja, ni kweli anawinda tembo mmoja na nyati mmoja si zaidi. Huo mkakati ni upi ambao utafanywa? Hawa Askari watakaokuwa wanasimamia je, Serikali itajikita vipi kwa maana ya Idara ya Wanyamapori? Naona majukumu makubwa sana amepewa Mkurugenzi wa Wanyamapori katika kusimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri atupe mkakati kwa hili kwa sababu ndiyo kilio kikubwa. Watu wanachowinda ni kikubwa zaidi, wanasafirisha nyara kwenda nje kwa kiwango kikubwa lakini sisi Watanzania tumekuwa kama watazamaji. Kwa hiyo kelele zetu zote na kilio chetu ni kuhakikisha kwamba rasilimali ya nchi yetu tuliyonayo inabaki hapa na tunanufaika kwa asilimia kubwa. Kwa sasa tunapata asilimia 25 tu. Kwa hiyo, hili ni *challenge* kwake Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, napenda kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba, Wizara aliyonayo ni ngumu sana na ndiyo maana *turnover* ya Mawaziri inaonekana ni kubwa. Kwa hiyo, lazima akubali kupambana na mambo mazito na bahati mbaya sana Wabunge wengi tuliomo humu tumetoka kwenye maeneo hayo. Kwa hiyo, watu wanafahamu nini kinachoendelea, kwa nini hatupati mapato yanayotakiwa, kama hawa watu wanatuzunguka, basi tusiwape hiyo nafasi. Kama kuna mtandao wa wenzetu wanaowinda na kumiliki vitalu kwa ajili ya kutuhujumu sisi, tunaomba wenzetu mliopewa dhamana, basi ifike mahali tuwaweke wazi na kuwanyima kabisa kuwapa vitalu ili kusudi wasiiharibie heshima Wizara na nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hizi ndizo kelele zetu wala hatuna tatizo na lingine ni kuhakikisha kwamba tunalinda uchumi wetu, tunalinda maliasili yetu na watu wanaojitolea kwa moyo wa dhati sehemu za mashamba yao, sehemu za uwekezaji wao kupisha uhifadhi ili waweze kunufaika kwa faida ambayo inatokana na uhifadhi wa wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na hilo na nilitaka kwa dhati kabisa nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba bado anadeni kubwa la kuhakikisha kwamba analeta marekebisho ya viwango vyote ili kuleta faida na manufaa kwa wananchi wote ambao watapisha maeneo na wananchi wote ambao watakuwa ni walinzi wakubwa wa Hifadhi zilizopo kwetu Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. JOHN P. LWANJI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami ili nichangie juu ya Muswada huu. Nichukue nafasi hii kwanza niwapongeze wenzetu waliowasilisha Muswada huu japokuwa sina uhakika kama nauunga mkono. Lakini kwa juhudi walioionyesha katika maeneo yangu nadhani kuna mwelekeo mzuri na watu wa Rungwa, watu wa Mgandu, watu wa Doroto walikuwa wanausubiri sana Muswada huu. Labda niwasilishe tu kwa Mawaziri hapo, Waziri na Naibu wake salaam za Doroto jinsi walivyoshughulikia tatizo la mpaka, pia tatizo la mpaka kati ya hifadhi pamoja na wananchi. Sasa hivi wananchi wanakaa salama matatizo yamepungua, wananchi Watanzania hawana tatizo sana kama matatizo yanarekebishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nililalamika sana kuhusu tatizo la simba msimu uliopita na bahati nzuri malalamiko yale yalipatiwa ufumbuzi. Wataalam wa kuwawinda walipatikana, wamewaondoa, wengine waliuawa, wengine wakakamatwa na mitego na sasa wananchi wanakaa kwa usalama na ndicho hicho tulichokuwa tunataka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi tajiri sana kwa upande huo wa rasilimali hizi tunazozizungumza hapa za wanyamapori, nadhani ni nchi ya kwanza duniani. Tuna *National Parks* 14, *Game Reserves 17*, ni utajiri wa wa hali ya juu sana. Lakini linapokuja suala hili la kuwaona wananchi kwa maana ya kuwashirikisha waweze kunufaika tunasuasua. Kuna wakati fulani walikuwa wanasema kwamba labda twende Botswana tukaangalia wenzetu wanafanya vipi, labda sijui twende wapi; wakati sisi ndio tunaongoza duniani kwa rasilimali hii. Sasa tunataka watu wengine waje watutengenezee, sasa ni kitu cha ajabu sana. Tukamwangalie nani ili aje atuainishie kwamba jamani rasilimali yenu hii mgawane hivi, wananchi wapate hivi, hakuna; ni sisi wenyewe. Kwa hiyo, ninavyouangalia Muswaada huu bado kuna mapungufu, umejikita zaidi kwenye masuala ya udhibiti na masuala ya uhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti iliyopita nilishawishiwa sana mpaka nikaunga mkono. Lakini hoja yangu niliyoiwasilisha wakati ule ilikuwa inasema juu ya sera ya fidia kwamba iboreshwe. Sasa jibu nililolipata linasema hivi, taratibu za kulipa fidia ni mzigo mkubwa kwa Serikali. Sasa sijui ni tani ngapi? Hata hivyo, Wizara yangu inaliangalia kwa kina suala la kifuta machozi katika Sheria mpya ya Wanyamapori ambayo itawasilishwa Bungeni mwezi Agosti 2008. Ni Muswada huu, wakati ule haukuwasilishwa ndiyo umewasilishwa sasa hivi kwa kina. Lakini Sura ya Nane sidhani kama kuna *seriousness* na sidhani kama kuna ukina wowote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani nimepata mashaka zaidi, tulisafiri na Mheshimiwa Naibu Waziri tukaenda mpaka maeneo hayo. Kwangu nina mbuga tatu; Rungwa *Square Kilometre 9,000*. Kizigo *Square Km 2,000* na Muheze ni *Square Km 1,000* na *Open Area* za Chaya. Anapofika Waziri hata akiwa ni Waziri wa Kilimo au wa Maji hawezi kukosa kuulizwa suala hili la wanyamapori na hasa suala hili la fidia. Kwa sababu hakuna kijiji ambacho mtu hajawa *affected* kuumwa na fisi, simba au tembo. Lakini tuliambiwa na tukawaeleza wananchi kwamba jamani subirini Muswada unakuja. Sasa Muswada huu umekuja *there is nothing tangible* na kwa kweli wamekwepa suala hili. Wanasema itafuata *regulations* na kulingana na mazungumzo ya leo kwenye *TBC*, Mheshimiwa Ndugai ameligusia hilo, anasema ni shilingi 200,000/ ni hiyo hiyo. Mwananchi apate nini tunapomwacha katika hali hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sidhani kama kuna mtu anaweza kujianika barabarani aweze kukamatwa na simba au tembo. Hizi ni ajali. Ikitengwa shilingi bilioni 1.0/- kwenye masuala haya ya fidia kuna tatizo gani? Sasa wanasema Muswada ni mzuri labda tunaovaa masuti, tunalala kwenye mahoteli, labda ni mzuri kwetu sisi. Lakini kwa mwananchi wa Rungwa, mzuri vipi Muswada huu? Sidhani hata kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hata mzoga haruhusiwi, kuna kakifungu hapa kanasema hivi: "*except in accordance with any license or wildlife user right, nothing in this section shall be deemed to transfer to any person the ownership of any protected animal found dead or dying.*" Sasa kama Bwana Nyama hayupo hapo mwananchi wa kawaida hata kitoweo, kwa hiyo akimuona huyo amwache. Basi

wangeelezwa katika kifungu hiki kwamba ni mali ya fisi sio ya binadamu wala siyo ya nani. Mara nyingi digididigi wamekanyagwa haruhusiwi mtu kuchukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia suala la nyara halikutafsiriwa vizuri, ingewekwa *definition* ya nyara. Nina watu wangu ambao wamekamatwa kwa sababu wamekutwa na gamba la kiboko. Pale Itigi waliua kiboko watu wa *Game,* wakaruhusu wananchi wapate kitoweo. Wakajichukulia wakakata mapande sidhani kama kiboko ana ngozi sijui au tembo. Maana unaunganisha nyama na ngozi huwezi ukachuna ukasema hii ngozi, hii nyama. Sasa amekwenda nayo nyumbani, amekula nyama gamba lile yeye katika kuamini kwake amekwenda kutumia kwenye shughuli zake, ameweka kwenye lambo la maji akiamini pale ng'ombe wanapokunywa watanenepa kama kiboko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hiyo ilikuwa ni imani yake na kwa kweli ng'ombe aliwatunza vizuri wakawa wamenenepa msimu huo. Sasa watu wakasema mnaona, wakaenda kumchongea, wakamkamata, wakamweka lupango. Wala haikupita muda wakaja wakafilisi tena Polisi na kesi hii hadi Wizara nilishawaeleza. Sasa ni mateso wanayoyapata wananchi, ndiyo maana sisi Watanzania kwa ujumla tulio wengi hatuna utamaduni wa masuala ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu toka mwanzo anajua kabisa kwamba yeye na wanyama na Serikali ni adui. Ukikutwa na kipande cha mbao wewe ni lwako. Sasa tunaambiwa kwamba kinaundwa kikosi kingine ambacho kitakuwa na idhini tena ya Mkuu wa Nchi, sijui wanaruhusiwa kubeba na silaha kukabiliana na majangili. Hivi vikosi vilivyoko vimeshindwa nini? Tumeeleza sana kwamba vimeshindwa kwa sababu havina nyenzo za kazi na ni wachache. Sasa tunaleta tena kikosi kingine chenye nguvu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala ya *mistaken identity,* tumewahi kuona nchi hii mtu amepigwa risasi wakasema tulifikiri ni jambazi lakini mtu ameshakufa. Sasa kuna hicho kikosi ambacho ukikisoma utakuta ni sawa na Polisi. Ni kazi ya Polisi sasa na wanapokuwa kule porini anaweza kutambua vipi huyu ni jangili na huyu ni mwananchi. Nadhani na hapa napo kungeweza kuangaliwa waweze kuona ni jinsi gani wanaweza kufanya kazi na kwa nini hivi vikosi vingine vimeshindwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia waainishe maeneo ya *Game Reserves* ambazo kuna machimbo. Kwa mfano pale Mgandu kwa upande wa *Game Reserves,* kuna machimbo ya *lithium* na wananchi hawaruhusiwi kwa sababu wanaambiwa kwamba ni maeneo ya hifadhi, hamruhusiwi kwenda. Kwa hiyo, nadhani hapa napo tungeweza kuona. Sasa wanasema usimamizi wa mapori ya akiba uwe chini ya Mkurugenzi wa Wanyamapori, sasa *role* ya Halmashauri za Wilaya hizo ambazo hayo mapori ya akiba yapo huko itakuwa nini? Sasa hivi kuna mtu wa maliasili halafu kuna *KDU.* Huyu *KDU* anaripoti kwa Mkurugenzi wa Wanyamapori, huyu wa Maliasili anaripoti kwa *DED.* Lakini pale kumekuwa na *friction* kila mara na pesa unakuta mara nyingi wanapeleka kwa *KDU,* wanawaacha hawa na ndiyo wasimamizi wa hao wafanyakazi, sasa unakuta matatizo kibao. Huyu naye wa *KDU* ana maeneo makubwa. Kwa hiyo naomba sana

Wizara hii itusaidie, isisubiri kazi ya zimamoto, ifanye kazi. Iwape vifaa na iwape motisha ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kusema ada ni nafuu lakini mimi naona kwa mwananchi wa kawaida bado ada ziko juu kiasi. Ni utaratibu si suala la ada tu lakini ni utaratibu. Sasa kuwinda kanga kuna ada yake lakini idadi ya kanga unaambiwa mwisho watatu na kwa kipindi cha muda mfupi. Sasa vitu kama hivi havisaidii badala yake vinaongeza uwindaji haramu. Naomba Wizara hii iwe *serious* na ijaribu kuangalia. Nimejikita zaidi kwenye Sura ya Nane ya Muswada huu. Ndugu zangu hakuna mtu anayeweza kuja kutufanyia mambo yetu, ni sisi wenyewe. Sasa unapokuta wachache wamepewa dhamana hiyo, basi unakuta wanasema tunafanya kwa niaba ya Taifa lakini waliowengi hawanufaiki *then* inakuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana kama si sasa hivi, basi katika muda ujao siamini kama *regulation* zitasaidia na kuachia Waziri na kuongea na Waziri mwenzake. Toka lini Waziri wa Fedha atamwambia Waziri wa Maliasili kuna pesa za kutosha, hakuna. Toka tumeanza ni nakisi, nakisi kila mahali. Kwa hiyo haiwezekani. Kwa hiyo hakuna nyongeza yoyote kwa upande ule na hakuna suala la fidia, bali ni kifuta machozi. Machozi ya nani, ya aliyekufa na machozi ya nini, ni machozi wakati anamkimbia mnyama kabla hajamkamata au vipi? Maana haijulikani hiki kifuta machozi, machozi ya nani? Mtu anazikwa kichwa kimeliwa na samba, watoto na mama unawaambia nini? Kwanza hizo za mwaka juzi watuambie wamelipa?  (*Makofi*/*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.  (*Makofi*)

**MHE. ALOYCE B. KIMARO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na nipate kuchangia Muswada huu wa maliasili. Naomba wananchi na Bunge hili waelewe kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 63(2), Toleo la 2002 inasema ya kuwa:  "Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndicho chombo kikuu chenye madaraka kamili kwa niaba ya wananchi wa Tanzania ya kusimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na vyombo vyake vyote katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku".

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa mujibu wa Katiba hiyo hiyo lengo kuu la Serikali litakuwa ni ustawi wa wananchi na Ibara ya 9(c) inasema kwamba: "Shughuli zote za Serikali zitatekelezwa kwa njia ambazo zitahakikisha utajiri wa Taifa unaendelezwa kwa njia ambazo zitahakikisha utajiri wa Taifa unahifadhiwa na kwa njia ambazo utahakikisha kwamba utajiri wa Taifa unatumiwa kwa manufaa ya wananchi wote kwa jumla na pia kuzuia mtu yoyote kumnyonya mtu mwingine na kwamba maendeleo ya uchumi wa Taifa yatakuzwa na kupangwa kwa uangalifu kwa pamoja". Tunapopanga hapa Bungeni maana yake ni wananchi wanapanga. Kwa kuwa wananchi kwa makini kabisa walichagua Wabunge na Wabunge makini ndiyo hapa wanapanga kwa niaba ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili la Tisa la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania halitakubali hata kidogo kuona utajiri wa nchi yetu unatafunwa na wageni

wachache huku Watanzania wakiendelea kubakia kati ya nchi 25 zilizo maskini duniani na huku hili ni Bunge la Tisa. Zaidi ya miaka 45 ya uhuru leo hii unasikia Watanzania wenzetu wanasema bado Watanzania hawawezi kumiliki kitalu cha uwindaji. Maneno haya hayawatendei haki Watanzania. Watanzania wapo tena wengi kabisa na wanaweza. Leo hii mwakilishi wa Tanzania anasema bado hawawezi, nashangaa sana. Bunge hili ni Bunge makini tena nawahakikishia wananchi Bunge hili ni Bunge la viwango vilevile. Kwa hiyo tunafanya kazi kwa viwango wala hatufanyi kazi kwa kusukumwa na wala hatufanyi kazi kwa kutumwa na mtu yoyote, tunatumwa na wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maliasili na Utalii ina uwezo kabisa wa kuongeza pato la Tanzania kutoka lile ambalo inachangia *percent* 18 mpaka kufikia *percent* 50 kama watakuwa ni Wazalendo na watakuwa wanafanya kazi kwa kutumwa na Watanzania. Nasema hivi kwa kuwa Idara za Maliasili na Utalii na hasa Idara ya Wanyamapori inafanya kazi kwa kusukumwa na wafanyabiashara hasa wageni. Leo hii unaposema kwamba Mtanzania hawezi kufanya biashara ya uwindaji, kwanza hawa watu wanapokuja kuwinda wala si wawekezaji. Hawa wanakuja kuvuna, ni wavunaji wa maliasili zetu, si wawekezaji. Mtanzania atashindwa kununua *tent*, atashindwa kununua bunduki, atashindwa kununua *fridge*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wapo wengi ambao wana uwezo huo, lakini nawashangaa maofisa ambao tunawatuma wafanye kazi hizo wanakwenda kufanya kazi kwa maslahi yao na maslahi ya wafanyabiashara wachache, tena wageni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano hiki kitendo cha Wizara hii kukubali barua walioandika wawindaji kuomba waongezewe muda wa kuwinda. Barua imeandikwa tarehe 5 Novemba, nyingine ikaandikwa tarehe 5 Januari, kikao kikaitishwa haraka haraka Wajumbe wa Kamati ya Ardhi na Maliasili wakakutana haraka haraka kwa dharura tarehe 12 siku ya Mapinduzi, wakaacha kusheherekea, Mapinduzi wakaenda kukutana, wakasema tunabariki hili. Lakini ndugu zangu hakuna mwenye uwezo wa kukiuka maagizo ya Bunge. Haya yangepaswa yarudi Bungeni yakubaliwe, haraka haraka tarehe 16 wawindaji wakaandikiwa tumekubaliana na yale matakwa yenu. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge samahani nadhani hoja kuhusiana na barua ilishaamuliwa na imekamilika nenda kwenye mchango.

**MHE. ALYOCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndiyo mchango wenyewe. Barua hiyo nimeitaja kuonyesha kwamba idara hii ni kwamba inatumwa na wafanyabiashara. Mimi naiwekea msisitizo ili waache. Tena naongezea tarehe 16 baada ya barua hiyo wakaondoka wakaenda Marekani kwenda kuwasaidia wafanyabiasha hawa hawa kutangaza vitalu vyao. Sasa najiuliza huku sisi tunasema vitalu visitishwe huku watu hao hao ndio wanakwenda kuwaambia wale waongeze. Maana yake ni kwamba, nasisitiza kusema kwamba, hawafanyi kazi tunazowatuma. Kwa hiyo naomba tu waache tabia hiyo. Waswahili wanasema ukimwona panya anamdhihaki paka maana yake kuna shimo karibu sana la kukimbilia.

Mheshimiwa Spika, lakini nakwambia hakuna Serikali yoyote duniani ambayo inaweza kudhihaki maamuzi ya Bunge na hakutakuwa na shimo la kukimbilia lililoko karibu. Kwa hiyo, wale wanaokiuka maagizo, wakifika hapa Bungeni tayari wanakuwa presha zinapanda, presha zinashuka, presha zinapanda, presha zinashuka kwa kuwa wanajua wameshakosea. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake wanaomba uhisani wa Bunge lakini kwa kuwa Bunge hili ni makini halitakubali. Kwa hiyo nawasihi sana viongozi wote wenye nia njema ya kuwaondoa Watanzania kutoka kwenye umaskini, watekeleze maamuzi yote yanayoamuliwa hapa Bungeni na Mungu awabariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maliasili na Utalii ina uwezo kabisa. Nitatoa mfano wa maeneo ambayo mapato yanapotea. Kwa mfano, masuala ya utalii, utalii ni eneo ambalo linaweza kuingiza mapato mengi ndani ya Tanzania, lakini unakuta anapewa mwekezaji. Eneo la kujenga hoteli, anajenga hoteli, ardhi ile si mali yake ndani ya hifadhi ya Taifa, hatengenezi barabara, haangalii wanyama, kazi yake ni wageni kuingia na kuona wanyama lakini anamchaji mgeni dola 1,000, yeye anacholipa kwa Serikali ni chini ya dola 10. Tena anatembelea barabara zinazotengenezwa na Serikali ndani ya Hifadhi, anaangalia wanyama wanaotunzwa na Serikali na wananchi ndani ya hifadhi, lakini mapato yale ya dola 1000 kinachochukuliwa na Serikali ni chini ya dola 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ukienda katika eneo lingine ambalo nasema hawa wanapotunga kanuni na tukiwaachia, juzi nilikuwa naongea na mmojawapo wa wataalam nikamwambia uwindaji si uhifadhi endelevu kwa wakati huu. Dunia nzima inataka kuondokana na uwindaji iende kwenye uhifadhi, watalii wapige picha mnyama, mtaalam yule akasema nyie Wabunge tuacheni tufanye utaalam wetu nyie kafanyeni siasa zenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa jeuri ya namna hiyo ndiyo maana tunasema hawa lazima tukabiliane nao. Ndio wanaokwenda kutunga Kanuni ambazo wanaambiwa na hawa wafanyabiashara. Kwa mfano kanuni ya kusema kwamba lazima kuwe na *grace period* ya miaka miwili ya kujitayarisha kuwinda. Unajitayarisha nini vitalu vinajulikana dunia nzima na kwamba kama una kitalu ukitangaza kwenye *internet* mwezi mmoja au miwili wawindaji wanavifahamu vyote watakuja. Lakini unaweka kwenye kanuni ili kubana tu wale ambao wanataka kusogeasogea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, wanaweka kwenye kanuni kwamba ukishapewa kitalu hakuna mtu yeyote atakayeingia kwenye kitalu hicho. Matokeo yake kule Serengeti kuna mwekezaji amepewa vitalu vitatu Grumeti, Ikorongo na *open area* yote. Ana-*square kilometre* 1000, maana yake ana Serengeti yake hapo pembeni, lakini hawindi, ana wageni wake ndiyo wanatembea kwenye hilo eneo. Wakienda wageni wengine anaweka Askari, anasema huku si kwenu, kwenu ni huko Serengeti *National Park*. Kwa hiyo, yeye anabaki na Serengeti yake pembeni. Hatuwezi kukubali ndani ya Bunge hili, Bunge la viwango, mambo haya yaendelee na yanatokea wakati wa kuweka Kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kengele ya pili naomba kwa nusu nusu niunge mkono hoja lakini kwenye Kanuni tuwasimamie vizuri kanuni zile zifuate Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia. Labda nianze kwa kuweka mambo sawa, inawezekana kukatokea upotoshwaji halafu ikaonekana kama vile ndiyo sehemu ya ukweli, kwa sababu kuna Mbunge mmoja wakati anachangia, kazungumzia masuala ya kesi, kwa sababu hawa wawekezaji wanaweza wakakasirika. Kwa utaratibu uliopo ni kwamba, tunafahamu mwaka 2009, kisheria ndio ulikuwa mwisho wao wa kuwa na haki ya kumiliki vitalu. Kwa hiyo, tusije tukatengeneza uoga ambao mwisho wa siku ukawa hauna ukweli wowote. Hilo lilikuwa ni angalizo langu la kwanza, vilevile kumtoa wasi wasi Mheshimiwa Mrope aliyekuwa akichangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nianze tu moja kwa moja, kwa kuungana na *concern* ya Wabunge, kuhusiana na kipengele cha 70 juu ya suala zima la mkono wa pole. Hakika inasikitisha kuona kwamba, imefikia kipindi mnyama anakuwa anathaminiwa zaidi kuliko binadamu. Mimi ninadhani, tatizo hasa lipo kwenye Sera yenyewe, kwa sababu Sera ya Wanyamapori haitambui kitu chochote kinachoitwa fidia, ndio maana sasa Waheshimiwa hapa wanakuwa wanajitahidi kutafuta neno ambalo litaweza kujifananisha na fidia lakini siyo fidia. Kwa hiyo, ninadhani kuna umuhimu wa kuwa na Sera ambayo inatambua uhalali wa Watanzania ambao watapata madhara yoyote kutokana na maeneo yao kuvamiwa na wanyama. Hii ni changamoto kwa Serikali, kwa sababu wana jukumu la kutafuta askari ambao watakuwa wana jukumu la kulinda maeneo. Sasa badala ya kurushia mzigo kwa wananchi ni muhimu Serikali iwajibike kwa kiasi kikubwa sana, kuhakikisha kwamba, kunakuwa na walinzi wa kutosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea na mchango wangu, niende kwenye Muswada ambao tunaujadili. Ukiangalia kwenye huu Muswada, kipengele cha 37, Mkurugenzi wa Wanyamapori alipokuwa na mamlaka ya kugawa vitalu *as an individual*, ilizua utata na nadhani ndio matokeo yake, sasa hivi tuna hivi vitalu ambavyo vinahodhiwa na watu wachache. Sasa fikra ilikuwa ni kwamba, labda sheria hii itatoa jibu, lakini matokeo yake, kwa mtazamo wangu, ninaona sheria imekuwa mbaya zaidi. Kwa nini ninasema sheria imekuwa mbaya zaidi?

Ukiangalia kipengele cha 37(6), haya mamlaka amepewa Waziri. Waziri ni mwanasiasa na tunajua maamuzi ya kisiasa ambayo yameshatokea; tuliona kwenye madini, tumeona juzi hapa Mheshimiwa Shamsa Mwangunga jinsi Bunge lilivyompeleka mpeleka kidogo, tumeona masuala anayosemwa Mheshimiwa Masha, tunaona jinsi ambavyo wanasiasa labda kutokana na kutokuwa *probably* na ufahamu wa sekta husika, wanajikuta wanafanya *decisions* ambazo si sahihi. Kwa hiyo, niungane na Waheshimiwa Wabunge ambao walipendekeza kwamba, iundwe Mamlaka ya Wataalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii ya *Hunting Block Allocation Advisory Committee*, *content* yake kungekuwa kuna mamlaka ambayo ina watu wa aina hii;

ingekuwa ni rahisi sana na ingefanikisha vizuri sana suala hili zima la ugawaji wa vitalu kwa haki na pasipokuwa na *political intrest,* kwa namna moja au nyingine. Vilevile cha kushangaza zaidi, ukiangalia kipengele cha 37(13), kinasema kwamba, wakati tunaambiwa kwamba, Waziri mwenye dhamana ya Wizara husika ndio ana mamlaka ya kugawa vitalu, huku tunaambiwa tena mtu ambaye hataridhika na uamuzi wa Waziri husika, aende tena akakate rufaa kwa Waziri kwa kitu kinachoitwa *Administrative Review*.

Sasa haiingii akilini, mimi ndio nina mamlaka ya kugawa na ndio nina mamlaka ya kupitia kwa dhana ya *Administrative Review, in some sort of Appeal* na kwamba, uamuzi wangu ndio utakuwa wa mwisho, *unless* kama kutakuwa kuna mtu ambaye atataka kwenda Mahakama Kuu. Sasa hapa ni kuweka mianya ya rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuwe *realistic*, tumeona watendaji wetu ambao tunawapa dhamana wanavyofanya. Kwa hiyo, tusijaribu kutengeneza mazingira ambayo yatakuwa yana-*entertain* masuala mazima ya rushwa. Vilevile nikiendelea kwenye vipengele vingine, unakuta sheria hii inazungumzia suala zima la ajira. Inatamka bayana kwamba, *minimum requirement* ya makampuni haya ya utalii, inatakiwa iwe mzalendo mmoja na mgeni mmoja. Sasa wakati tunazungumzia dhana nzima ya kusaidia vijana wetu wapate ajira, haiingii akilini pale ambapo tunaweka usawa mgeni na mwenyeji katika soko la ajira. Tukiangalia vilevile suala la sera nzima hii ya wanyamapori, inaeleza jukumu lake au madhumuni yake ni ku-*promote* ajira kwa Watanzania. Sasa sheria tena inapotamka bayana, kwa sababu nilitegemea labda inaweza hata ikawa kwenye kanuni, lakini sio katika *formula* hii. Sasa unapokuwa unaweka masharti ya idadi ya Watanzania watakaoajiriwa na idadi ya wageni watakaoajiriwa kuwa sawa, inakuwa haitusaidii ila inakuwa inawarudisha nyuma Watanzania. Kwa hiyo, ninatarajia kwamba, kutakuwa kuna mabadiliko katika hili, isiwe *fifty fifty, at least* kwa kuwa labda tunasema bado soko letu linakuwa la ajira na wataalam wa ku-*hunt;* ni muhimu hata iwe moja kwa tatu lakini isiwe *fifty fifty*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nikija katika suala zima la hali ilivyo katika Wizara hii na changamoto zilizopo, ni kweli kwamba, tumeona kama alivyo-*observe* Mheshimiwa Kilasi kwamba, inaonekana hii Wizara ni ya moto kidogo, kwa sababu kila Waziri anayekwenda pale, anajaribu kufanya *reform* anaondolewa. Kwa hiyo, inavyoonekana ama hao watu ambao wanahusika na masuala ya uwindaji, wana nguvu kubwa sana kuliko ambavyo sisi tunaiona. Wana uwezo kwa kiasi kikubwa sana ku-*influence the whole system,* kiasi kwamba yeyote ambaye anaonekana kama anakuja mbele kuweza kuwabana hao, kama ambavyo tuliona Mheshimiwa Maghembe hapa alizungumza kwa makeke sana tutaongeza ada, lakini matokeo yake akarudi, hata hakuja kutoa *feedback*! Kumbe kule aliambiwa bwana wewe sisi tunataka kiasi hiki na ndivyo ilivyo hadi hivi sasa. Kwa hiyo, kuna tatizo la msingi ambalo inabidi tuliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kupitia taarifa kuhusiana na watu ambao wanahodhi hivi vitalu, hasa hasa Ripoti ya Mheshimiwa Mzindakaya. Nimeona kwamba, katika vitalu 73 ambavyo vipo kwenye mapori yale yaliyoshiba, ambayo yana wanyama

wengi, yanamilikiwa na makampuni ya kigeni 12. Vitalu vipo 73, makampuni ya kigeni 12 yanamikili vitalu 57.

Kwa mantiki hiyo, asilimia 78 ya vitalu vyote vilivyoshiba vinamilikiwa na wageni. Sasa hili ni tatizo na mimi ninaamini kabisa kwamba, huo mchakato au hiyo *transition period* ambayo Wizara ilipewa juzi, ikija basi tutaona kama kweli tuna dhamira ya kweli ya kuhakikisha kwamba, hawa Watanzania tunawatoa kutoka hatua moja au nyingine, hii 78% lazima ipungue, *unless* kama tunakuwa hatuimaanishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna kitu kimoja nilikigundua; unakuta kuna makampuni labda matatu, ambapo makampuni mawili kati ya hayo wana uhusiano na mwenye kampuni moja. Nitatoa mfano; kuna huyu mtu wa *Gerald Pasan's Safari Corporation*, yeye tunaambiwa ana vitalu vinane, lakini ukiangalia huyu *Ballet Safari Corporation* ambaye ana vitalu vinane, *within* Ballet kuna familia ya *Pasan's*. Sasa hili ni tatizo. Kwa hiyo, unakuta kumbe ni mtu mmoja amejisambaza kwenye makampuni mengi, matokeo yake Watanzania wanakuwa wanakosa fursa ya kuweza kuwekeza katika hili suala zima la utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kumekuwa kuna malalamiko sana kutoka kwa hunters wa Kitanzania, wanasema kwamba, wao wanapewa masharti magumu sana. Kwanza, wanasema mitihani yenyewe, *modality* yake, mbali na kwamba ni ngumu, hata wale wachache basi wanaofanikiwa kuweza kuifaulu, masharti yanakuwa ni magumu sana, ambayo yanawafanya wao washidwe kwenda kuingia kwenye soko lenyewe. Kwa mfano, wanasema baada ya kufaulu, ili hata upate leseni ya muda, unatakiwa utoe dola elfu moja. Sasa lazima tujiulize huyu mtoto wa mkulima anatoa wapi dola elfu moja baada ya kumaliza Chuo kwa mfano cha Mweka?

Vile vile ili uweze basi kuonyesha kwamba, unaweza kuendesha hii biashara ya kitalii, unatakiwa sijui uwe na *Landcruiser* tano, sijui uwe na majenereta ambayo ukiangalia ni karibu milioni mia tatu. Kwa hiyo, ninadhani kuna umuhimu Serikali yetu kuhakikisha kwamba, tunafanya masuala ama maamuzi ambayo yanawanufaisha watu wetu. Vilevile tuangalie nchi za wenzetu walivyofanya; Zimbabwe na Botswana kuna *mechanism* ya kuhakikisha kwamba, *hunters* wa kizalendo ama wa nyumbani wanapewa mazingira muafaka ya kuweza kufanya kazi, hatimaye tukuze ajira kama tunavyofanya. Isije kuwa tunasema tuna dhamira ya kuwawezesha Watanzania, lakini hatuifanyi dhamira hii kivitendo. Ninashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima, ahsante sana. Sasa ninamwita Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, aweze kuchangia kama mchangiaji wa mwisho mchana wa leo.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia yangu machache ambayo nimeyaona katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasahau, nitaanzia kwenye tatizo la sheria; kifungu cha 99(1) kinazungumzia *burden of proof*. Sheria hii imekuwa ngumu na haitawatendei haki wananchi. Ninazungumza hivi kwa sababu upo uwezekano wa mtu kuchomekewa kwa maana kwamba, inawezekana hakufanya kosa au hakukutwa na nyara, lakini mtu akaenda akamuwekea na akashindwa kujitetea, mahakama ikachukua uamuzi wake bila ya yeye kupata haki yake. Hii sheria ninaomba iangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu vilevile katika mazungumzo ambayo yamepitishwa kuhusu Idara hii, kulikuwa na mapendekezo ya kuundwa kwa Mamlaka itakayosimamia mapori yote, lakini mpaka leo hatujapata majibu; hatujui hiyo Mamlaka itaundwa lini na itakuwa na majukumu gani? Kwa hiyo, hilo pia tungependa tulifahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumza vilevile kuhusu maeneo yetu ambayo tunaishi. Mimi ninatoka Mkoa wa Lindi, Wilaya ya Kilwa. Mkoa huu una utajiri wa mapori yaliyozungumzwa hapa na kuna vitalu vya uwindaji, lakini imekuwa ni shida sana kwa wananchi kunufaika na vitalu hivyo. Sheria imezungumza hapa, lakini utekelezaji wake ni mgumu. Nafikiri wenzangu waliotangulia wamezungumza vya kutosha, kuhusu hizo sheria za kuwalinda wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wa Wilaya za Kilwa na Liwale Mkoani Lindi na hata wa Wilaya ya Nanyumbu Mkoani Mtwara, wanakabiliwa na matatizo makubwa sana ya kupambana na wanyama ambao ni waharibifu, wakali na wanaowaumiza binadamu. Sheria hii kwa vifungu ambavyo vimetajwa kama walivyozungumza wenzangu, kweli inawalinda wanyama badala ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni nilitembelea Wilaya ya Nanyumbu ambako nilikuta Ndovu kwa siku moja amepita vijiji vitatu na ameua watu watatu, lakini hakuna chochote kinachotokea. *Game* mmoja ambaye alitamani kuingia kumuua yule mnyama, alionekana kwamba anatenda vibaya kwa sababu ya kusadia wananchi, ilibidi asiifanye hiyo kazi. Kwa kweli hii sheria iangaliwe pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba wanasema kuna fidia, lakini hizi fidia mimi naona ni kama kiinimacho, kwa sababu hivi leo mwananchi anapoliwa mimea yake shamba zima, fidia haifanani na mimea iliyoliwa. Vilevile mpaka hiyo fidia itakapokuja kutolewa, huyu mwananchi anaishije na anakula nini? Kwa hiyo, bado hapa panatakiwa paangaliwe kwa nguvu zote. Hiki kifungu cha 70, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anaangalia hizi sheria, akiangalie na hiki pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hii habari ya asilimia 25, ambayo inatolewa kwa vijiji. Kuna vijiji kadhaa ambavyo kuna wawekezaji, mfano, kwa kule Kilwa kuna hii *Coast Wildlife Hunting Company* na kuna *Tanzania Club Limited*. Haya makampuni wakati yanaenda kupata hiyo *hunting block allocation*, kuna *letter of offer* ambayo inamwelekeza mwekezaji aende kwa wananchi na anapewa masharti na hata anapomaliza zile shughuli zake, anatakiwa alipe fedha, lakini haya kampuni inakuwa ni ngumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii sheria ni nzuri, lakini utekelezaji wake unakuwa ni mgumu. Hawa wawekezaji wengi wamekuwa na viburi, hawataki kutekeleza yale ambayo yapo kwenye mkataba; matokeo yake, kijiji kinapotaka kupata zile haki hazipatikani. Kwanza, kijiji kinataka kipate zile fedha kitumie kwa kipaumbele chake ambacho kimepanga, lakini hawa hawatoi. Muda mwingine kwa mfano, nitachukulia Njinjo; mwekezaji ambaye anawekeza katika Kijiji cha Njinjo na maeneo yanayozunguka eneo hilo, wananchi wanataka fedha wafanyie vipaumbele vyao ambavyo wanavihitaji, lakini yeye anasema siwezi kuwapa pesa nitawajengea Kituo cha Polisi.

Hapa pana utata, ina maana kwamba, mwekezaji ana mamlaka; ile sheria ambayo anapewa wakati anapewa *hunting block allocation*, anaiweka pembeni kwa sababu hakuna mtu ambaye anaweza akamsimamia au kumlazimisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wanakijiji wanakuwa hawana uwezo wa kudai hivi vitu. Kwa hiyo, hizi sheria zimetungwa hapa na sote tunaziona ni nzuri, lakini utekelezaji wake ni mgumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makampuni ya kitalii ya nje yamehodhi vitalu vyote vikubwa. Wanavuna wanyama wanavyotaka bila ya huruma na hawalipi kitu chochote pale wanapohitajika kulipa kwenye eneo linalotakiwa, yaani hawatoi *social support*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo yamekuwa ni matatizo; hivi sasa kwa upande wa Kilwa, kuna Mradi unaoendeshwa na Wabelgiji *(Eastern Selous)*, unaoendeshwa katika vijiji tisa, unawasaidia wananchi kwenye kulinda maeneo yale na imepeleka mafunzoni hata wananchi wa kijiji kile ili waweze kulinda pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ni nzuri, lakini ninaiomba Serikali, licha ya hivi vijiji tisa, Mradi huu uende vijiji vyote kwa sababu tatizo la wanyama wakali na waharibifu kwa mazao limekuwa ni la kitaifa, ilichukulie hili kitaifa ili kunusuru maisha ya wananchi ambao wanaliwa na inusuru mazao ambayo yanaliwa kwa wananchi wa maeneo husika wanaozunguka mbuga hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia kuhusu takwimu za nyara. Kwa upande huu ninataka kuzungumza kwamba, kunapokuwa na miradi yoyote katika Halmashauri za Wilaya au ukusanyaji wa mapato yoyote, Serikali inafuatilia kama *Controller and Auditor General* anafanya kazi ya kuangalia yaliyopo pale. Nina swali ambalo ningependa kuiuliza Serikali; nyara ambazo zinakamatwa zinawekwa kwenye Halmashauri na ambazo zinapelekwa Makao Makuu, takwimu zake kwa kipindi cha miezi mpaka mwaka ni nani anazionyesha?

Je, mapato baada nyara hizi kupatikana, fedha zake nani anazi-*audit*? Ningependa kujua hilo kwa sababu sehemu yoyote inayoingia mapato, lazima kuwepo na uangalifu. Nyara ambazo zinapatikana zinahifadhiwa, sisi hatujui kama ziko maghalani zimejaa au zimeuzwa na kama zimeuzwa ni kiasi gani kinapatikana? Tunapokagua mahesabu ya maeneo haya, hatuoni fedha ambazo zinatumika au zimepatikana kwa takwimu za nyara zinazopatikana katika nchi hii. Kwa hiyo, ningependa hilo pia nilijue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kuzungumzia asilimia 25. Tumekuwa tunaambiwa asilimia 25, lakini imekuwa ngumu kupatikana. Vijiji vyote vinaambiwa asilimia 25, utakuta wanapewa shilingi 500,000, unaambiwa hiyo ndiyo asilimia 25 kwa mwaka. Wanapewa shilingi milioni tatu, mgawane vijiji vinne asilimia 25 kwa mwaka. Hii pia kama wanavyokagua mahesabu mengine, tungependa tujue ni wanyama wangapi wamewindwa katika maeneo hayo na kila mnyama analipa kiasi gani na zinapatikana kiasi gani ili tuweze kuijua hii asilimia 25 wanayopewa wanakijiji kama ni halali au la.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaona maelezo yangu yanaishia hapo; ningependa kuieleza Serikali, iangalie mapori ya Mkoa wa Lindi ni makubwa na Serikali inashindwa kuyasimamia. Mapori ambayo ni utajiri mkubwa kwa maeneo hayo. Kwa hiyo, ninatoa ushauri kwa Serikali na ninaiomba iende ikayaone ili Wananchi wa Mkoa wa Lindi na Mtwara, waweze kupata haki zao kutokana na rasilimali zilizopo katika nchi yao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanawetu, ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kwa mchangiaji huyo na muda tuliobakiwa nao, tutakuwa hatuwezi kumpata mtu mwingine yeyote kuweza kuchangia, utakuwa hautoshi. Kwa hiyo, ninapenda kuchukua nafasi hii kwanza, kusema kwamba, hii hoja itahitimishwa leo, lakini pamoja na hivyo, jioni watapata wachangiaji wachache. Ninapenda niwataje wawili tu ili waweze kujiandaa. Mchangiaji wa mwanzo atakuwa Mheshimiwa Dkt. Charles Ogesa Mlingwa, ambaye atafutiwa na Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro na wengine ambao watakuja kuamuliwa na Kiti hapo saa kumi na moja jioni.

Ninachukua nafasi hii sasa kulisitisha Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.55 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea juu ya Muswada wa Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori wa Mwaka 2008 *(The Wildlife Conservation Bill, 2008).* Kwa mujibu wa maelezo ya Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati anasitisha shughuli za Bunge, wachangiaji wetu wa mwanzo katika kipindi hiki cha jioni ya leo tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Charles Mlingwa, atafuatia Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka.

**MHE. DKT. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie kwenye Muswada huu. Mimi ni mdau wa Muswada huu kwa sababu ni mtaalam wa masuala ya wanyamapori. Siwezi kukosa mengi ya kuongea, isipokuwa kwa sababu ya muda ni vizuri kusema machache tu yale ambayo angalau ninaweza kusema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Wanyamapori kwa ujumla huwa naichukulia katika *set* moja na mifugo, kama dhahabu tulizonazo juu ya ardhi, kiasi kwamba, tukijipanga vizuri kuitumia tunaweza kuleta maendeleo makubwa zaidi kuliko hapa tulipo. Kwa kuwa tunao, hatimaye ninaamini tutafika tu huko. Kwa hiyo, hakuna kitu kilichozaliwa na kuweza kutembea au kukimbia kwa siku moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkurugenzi wa Wanyamapori na Watumishi wote wa Idara ya Wanyamapori. Ninaijua kazi kubwa sana ambayo wamekuwa wakiifanya na hata kwenye utayarishaji wa Muswada huu wameifanya kwa muda mrefu sana; kwa hiyo, tunawapongeza sana. Ninafahamu hata katika hatua za mwisho kukamilisha Muswada huu, Mkurugenzi wa sasa amejitahidi sana kuhakikisha kuwa, masuala ambayo wengine tuliyapigania huko nyuma wakati tukiwa kwenye Taasisi ya Utafiti ya Wanyamapori, yalikuwa hayakuingizwa lakini Ndugu Tarimo ameweza kuhakikisha kuwa taasisi kama *TAWIRI* na Chuo cha Mweka, vinaingizwa hususan kwenye suala ambalo nitalisema baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja, kwa sababu utekelezaji wa Muswada huu hata Wananchi wangu wa Shinyanga Mjini na Mkoa wa Shinyanga kwa ujumla watafaidika. Ninafahamu harakati za Serikali katika kuuboresha Uwanja wa Ndege wa Shinyanga, ambapo wawindaji wa kitalii wataweza kuutumia kwenda kwenye Mapori ya Akiba ya Maswa na Kigosi, kwa ajili ya uwindaji wa kitalii. Pili, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, kwa hiyo ni sehemu yamaandalizi haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu nyingine za kuunga mkono Muswada huu ni kama zifuatazo: Madhumuni makuu na sahihi ya Muswada huu ni kuimarisha uhifadhi wa wanyamapori na maeneo yao na kuboresha mapato yatokanayo na matumizi ya wanyamapori hawa. Kwa hiyo, tunazungumzia Muswada ambao ni sarafu moja; upande mmoja uhifadhi wa wanyamapori na upande wa pili ni mapato yatokanayo na matumizi ya wanyamapori hao. Ndiyo maana wakati mwingine kunakuwa na mijadala mikali sana ya kuona pengine tunavyofanya, kuna watu wanafanya makusudi kuona kuwa rasilimali hii inatumiwa vibaya. Mimi binafsi niseme kuwa, siamini kama kuna watu wanaofanya makusudi kabisa, kuhakikisha kunakuwa na hujuma kwenye matumizi ya maliasili hii, isipokuwa tu ni suala la uelewa wetu wa kufanya kazi au kuelewa namna usimamizi huo unavyoendeshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifano mahususi nikieleza kwenye Muswada wenyewe ni kwamba, Muswada huu umezungumzia kuanzishwa kwa Mamlaka itakayosimamia wanyapori katika maeneo nje ya Hifadhi za Taifa na Ngorongoro, yale yanayosimamiwa na *TANAPA* na Mamlaka ya Ngorongoro tukiangalia kwenye kifungu namba 7(8).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ina maana kuwa, baada ya *TANAPA* na Mamlaka ya Ngorongoro kuwa ni Taasisi za Umma hapa nchini, zinazofanya kazi kwa ufanisi, tutakuwa na mamlaka nyingine. Watu waliopo kwenye Idara ya Wanyamapori, kwa sehemu kubwa ndiyo wataunda Mamlaka hii na wataiweza kazi hii kwa sababu wana

uzoefu. Vilevile hawa *TANAPA* na Ngorongoro, wengi walitokana na idara yenyewe, kwa hiyo, sina wasiwasi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kingine ni kuwekwa madaraja ya vitalu vya uwindaji; hiki ni kifungu cha 37(9), ambapo naamini baada ya vitalu vya uwindaji kuwekwa kwenye madaraja, hata tozo zake zitazingatia madaraja hayo kuliko sasa hivi ambapo tozo za vitalu vya uwindaji zinafanana bila kujali ubora wa maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi zaidi ya uwindaji kwenye vitalu hivi vya uwindaji wa kitalii, yataruhusiwa kwa mujibu wa kifungu namba 53. Upande mwingine kuna uwindaji wa kitalii, kipindi ambacho si cha uwindaji. Wanyama hawa na maeneo haya yatumiwe ili tuweze kupata mapato zaidi na ule upande wa pili wa sarafu wa mapato uweze kuzingatiwa vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu namba 30 mpaka 32 cha Muswada huu ni kwamba, wananchi kwa mara ya kwanza, wanashirikishwa katika uhifadhi wa wanyamapori na kupewa uwezo si tu wa kusimamia ni pamoja na kukusanya mapato yatokanayo na wanyamapori wanaowasimamia kwenye maeneo ya ardhi ya vijiji. Kwa hiyo, ningependa niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge, ambao wamekuwa wakionesha wasiwasi sana kuhusu hatima ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *WMA* zitakapoanzishwa, zitasimamiwa na wananchi wenyewe. Kwa uelewa wangu wa Muswada huu, mapato watayakusanya wao wenyewe. Kwa hiyo si suala la kugawiwa tena na kwa jinsi hiyo, kama mnavyofahamu nchi yetu ilivyo na wanyamapori wengi, litakuwa ni suala tu la wanyamapori wenyewe tuwasaidie kuchangamka kuhakikisha kuwa, wanaanzisha hizo hifadhi za jamii ili waweze kuzisimamia na waweze kukusanya mapato kwa faida yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaamini hatimaye tukifanya vizuri, hawa nao wakishakusanya vya kutosha, watakuwa walipa kodi wazuri kwa Serikali Kuu. Kwa hiyo, hii ni fursa ya pekee ambayo hatujawahi kuwa nayo na ukichukulia hii pamoja na *TANAPA*, Ngorongoro na Mamlaka itakayoanzishwa, mfumo wa nne utakuwa ni wananchi wenyewe kusimamia rasilimali hii, ikiwa ni pamoja na mapato watakayoyakusanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazidi kuunga mkono hoja kwa sababu Mamlaka za Wanyamapori zilizopo, kwa mujibu wa kifungu namba 98, zinatakiwa kuwa zinachangia kwenye gharama za mafunzo, pamoja na utafiti. Taasisi zitakazofaidika ni Taasisi ya wanyamapori Tanzania na Chuo chetu cha Wanyamapori cha Mweka. Haya ni mapinduzi makubwa, kwa sababu huko nyuma tukumbuke wanyamapori wanaleta pesa, lakini taasisi inayotengeneza wataalam na taasisi inayofanya utafiti na baadaye matokeo haya kuzipa hizi mamlaka, zilikuwa hazipati pesa kutoka kwenye mamlaka hizi zinazokusanya. Mnaona mahusiano mazuri ambayo Serikali imeyaona na kuyaweka pamoja ili seti moja iwe imekamilika kuwa una hifadhi, unafanya utafiti na wataalam

unawatengeneza, ikiwa ni pamoja na wawindaji na wawindishaji *(Professional Hunters*), kupewa mafunzo kwenye taasisi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, baadhi ya matatizo ambayo tumekuwa tukiyazungumza hapa, kuhusu ushiriki wa Watanzania ni namna gani ufanyike usipokuwa na wataalam wanaoweza kuwindisha? Utasemaje unawazuia wageni kuja kama huna wataalam? Muswada huu kwa makusudi kabisa, umehakikisha kuwa si tu kwamba tunazingatia hili kinadharia, lakini kisheria haya ni mapinduzi makubwa sana katika usimamizi wa rasilimali yetu ya wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naendelea kutoa mifano ya namna Muswada huu unavyotaka tuunge mkono kwamba; kwa mujibu wa kifungu cha 38(3), kimeboresha ushiriki wa Watanzania katika biashara ya uwindaji wa kitalii. Hoja hapa si kuwakataa wageni, bali ni kuweka mfumo utakaohakikisha tunaboresha uhifadhi, lakini pia tunaboresha mapato tunayoyapata kutokana na wanyamapori hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hapa siyo kuona tunawafukuze wageni hapana; unaweza ukawafukuza na bado hiyo rasilimali usifaidike nayo. Kwa hiyo, kelele za kusema wanyama hawa wanatusaidia nini zinapata nguvu. Kwa hiyo, tuone mantiki ya kifungu hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kihistoria, wenzetu wa kutoka nje, ndiyo wamekuwa washiriki wakubwa. Kwa makusudi kabisa na sisi ni lazima tujitahidi, watu wetu waingie. Hatuwezi kusema tuwaondoe leo hapana, mambo yanaenda kwa nyakati na ndiyo maana ushauri wangu ni kuwa, kwanza, kwenye ushiriki ambao tumekuwa tukiupigia kelele wa Watanzania kwenye uwindaji wa kitalii; si vizuri tuanze kunyosheana vidole kuwa Kamati mlifanya hivi , mnaanza kuhoji na kadhalika. Mimi ninaijua biashara ya uwindaji wa kitalii, ninaamini bado tunahitaji muda zaidi wa kuweza kuielewa ili sisi Wabunge tuweze kujipanga vizuri zaidi, tuimarishe uhifadhi na tuweze kuinua mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine ninaoweza kuutoa ni kwamba, Mamlaka hiyo inayotarajiwa kuanzishwa, ianzishwe haraka ili tuweze kuimarisha uhifadhi wa wanyamapori nje ya hayo maeneo. Tukielekea huko, Serikali iwaangalie Watumishi wa Idara ya Wanyamapori, iweze kuwapa hela za kutosha. Ninajua wanafanya kazi kwenye mazingira magumu sana, mimi nilishawahi kuifanya kazi hiyo, wafanye kazi katika mazingira ambayo yanaridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, kama muda unairuhusu, kifungu cha 38(4), mimi siridhishwi na maandishi hayo; ninanukuu: "*The Minister shall make regulations prescribing fees and modalities of transferring hunting blocks from one person to another*." Ningeshauri isomeke hivi; "*The Minister shall make regulations prescribing fees and modalities of transferring hunting blocks sharehold from one person to another,*" kwa sababu ilivyoandikwa hapa ni kwamba, *blocks* zinahamishika wakati si kweli na wala huwezi ukasema tubadilishe neno iwe ni *ownership*, hata *ownership* ya *person* haipo. Kwa mujibu wa Muswada huu, vitalu vitamilikiwa na kampuni ambapo

kutakuwa na watu wa aina mbalimbali, isipokuwa mtu ndani ya kampuni anaweza akaamua kuuza *shares* zake akaingia mtu mwingine na akaenda kufuta *BRELA* na kuleta jina la mtu mwingine likaingia. Ninadhani hii ndiyo mantiki ya kifungu hiki, lakini kwa sasa hivi maneno yalivyowekwa hayako sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza na mimi nichukue nafasi ya kuchangia Muswada huu wa Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori jioni ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kuwapongeza na kuwashukuru sana, Wananchi wa Mbeya Vijijini, kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuhakikisha kwamba, Jimbo lile lililokuwa katika mikono ya kada wetu wa Chama cha Mapinduzi, ambaye Mungu amemwita mbele ya kiti cha haki, linaendelea kubaki ndani ya mikono ya Chama chetu cha CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wa Mbeya Vijijini, wameendelea kuwathibitishia Watanzania na dunia kwa ujumla kwamba, mpaka sasa katika mwaka wa nne wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi, tunakwenda vizuri na imani ya Wananchi kwa Serikali ya Rais Jakaya Kikwete, bado ni kubwa sana kwa kiwango ambacho kimedhihirishwa Mbeya Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mwizi wa fadhila, kama sitachukua nafasi hii, kuwapongeza makada wetu wawili; Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuonesha busara ya hali ya juu, ukomavu wa uongozi katika suala zima la kushughulikia Muswada huu ambao upo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ninasema hivyo? Muswada pekee niliowahi kuutamka tangu nimekuwa Mbunge kwamba, mwanzoni ulikuwa unaonekana kuwa na dhamira ovu, ulikuwa ni Muswada huu kabla ya maoni ya wadau kutolewa. Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, iliyokuwa ikiongozwa na Mheshimiwa Job Ndugai, kwa ushirikiano na Wizara ya Maliasili, walipokea maoni ya wadau na wakayazingatia kwa kiwango cha kupigiwa mfano. Kwa mantiki hiyo, ninataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Mwenyekiti wa Kamati, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo na Mkurugenzi wa Wanyamapori. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona niseme hayo bayana, kwa sababu Waswahili wanasema chanda chema huvishwa pete na si stahiki ya kichwa cha jogoo kuvishwa kilemba. Lingine ni dhana yetu nzima ya kujisahihisha kwamba, kukiri upungufu si dalili ya kushindwa bali ni ishara ya kujiimarisha. Kwa hiyo, ninaendelea kumpa moyo Waziri, aendelee kuchapa kazi wala asione tatizo na vidhoruba vidogo ilimradi ni suala la kujisahihisha na tuweze kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kujielekeza katika kuchangia Muswada uliopo mbele yetu ni kuzungumzia suala la mgogoro uliopo kati ya Pori la Akiba la *Mkungunero Game Reserve* na Wananchi wa Wilaya mbili. Tangazo la Serikali Namba 307 mwaka 1996, lililosainiwa na Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, liliunda na kutangaza mipaka ya Pori la Akiba la *Mkungunero Game Reserve,* ambalo katika suala la mipaka, limebainisha wazi kwamba, pori hilo litakuwa ndani ya ardhi ya Wilaya ya Kondoa, ndani ya Mkoa wa Dodoma. Kwa masikitiko makubwa, kana kwamba wataalam waliokwenda kuweka mipaka ya *Mkungunero Game Reserve* hawakuwa wanajua mipaka, walivuka mipaka ya Wilaya ya Kondoa na kumega maeneo mengine ya Wilaya ya Kiteto na Wilaya ya Simanjiro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tangazo Namba 65 la Mwaka 1961, lililosainiwa na Mwalimu Julius Nyerere la kuundwa kwa iliyokuwa Wilaya ya Monduli na iliyokuwa Wilaya ya Kondoa, lilibainisha mipaka bayana ya Wilaya hizo mbili na mikoa hii miwili baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanya hivyo vitongoji vitatu vya Mkoa wa Manyara, viwili vya Wilaya ya Kiteto, Kitongoji cha Lombeneki na Kitongoji cha Maasasi; Kijiji cha Irkiushioibor kilichopo katika Wilaya ya Kiteto kimemegwa na Pori la *Mkungunero Game Reserve* na Kitongoji cha Arkasupai katika Kijiji cha Kimotoro, Kata ya Loiborsiret. Wilaya ya Simanjiro, imemegwa na *Mkungunero Game Reserve* kinyume na Tangazo la Serikali, ningetaka nimwombe Waziri wakati anafanya majumuisho yake na kujibu hoja zetu, ajielekeze kuwaeleza Watanzania walioko huko kwamba, Tangazo Namba 307 litaheshimiwa na kwamba litabaki katika mipaka ya Kondoa, kama tangazo lenyewe lilivyotangazwa.

Mgogoro uliopo sasa, uliopelekea vifo vya watu wapatao saba katika mpaka wa maeneo haya ya Kijiji cha Kiushibo kati ya mpaka wa Wilaya ya Kondoa na Wilaya ya Kiteto, kwa kiasi kikubwa ni lazima tukiri kwamba, udhaifu huo wa wataalam wetu katika kuweka mipaka hii, umechangia kwa kiasi kikubwa. Tusingependa kuona Serikali yetu ikihusishwa na kashfa za aina hiyo, kutokana na uzembe wa wataalam wachache ambao wameshindwa kutimiza wajibu wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo, ningependa kuchukua nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa William Lukuvi, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma na Mheshimiwa Shekiffu, kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuunda Tume ya Wataalam na wadau mbalimbali katika Sekta ya Maliasili. Wataalam hawa walifanya utafiti na kubainisha upungufu niliokuwa ninausema na kuendelea kumwomba Waziri sasa azingatie busara za vikao vya wadau, ambavyo vimetaka Tangazo hilo Namba 307 liheshimiwe kama lilivyokuwa. Vilevile pasiwepo njama za kusema mnakuja kutuomba tena tuwamegee maeneo mengine ya kuhifadhi kutoka katika Vitongoji hivyo vya Lombeneki, Maasasi na Arkasupai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa najielekeza zaidi kuitendea haki ajenda iliyopo mbele yetu, nayo ni Muswada huu uliopo hapa wa Uhifadhi wa

Wanyamapori. Uzoefu unaonesha kwamba, Hifadhi za Taifa na Mapori ya Akiba, hayawezi peke yake yakakidhi mahitaji na matakwa ya wanyamapori na hivyo kuwafanya wanyamapori waendelee kubaki katika hifadhi zetu za Taifa bila kuondoka na kuvuka mipaka hiyo. Wanyama wanaondoka katika hifadhi hizo na katika mapori haya ya akiba kufuata malisho, maji na wakati mwingine kupata maeneo ya wazi ya kuzalia na maeneo ya kumpumzikia kama ilivyo katika Mbuga za Simanjiro au kwa maana ya *Simanjiro Pleins*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanyama hao wanapotoka katika Hifadhi ya Taifa ya Tarangire katika vijiji vipatavyo 12 vya Wilaya ya *Simanjiro Pleins*, wanaleta madhara makubwa sana kwa upande wa wananchi wanaokutwa pale. Kwanza, mazao yao yanaharibiwa kwa sababu ni kipindi cha kilimo, lakini ni dhahiri pia kwamba, mifugo iliyopo pale inaachiwa magonjwa mengi zaidi; kwa mfano, mifugo inapata matatizo ya ugonjwa wa *Foot and Mouth Disease (FMD)*, lakini pia Ugonjwa wa *MC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhara haya pamoja na mengine, ambayo siwezi kuyataja kutokana na muda, yanaendelea kutuacha sisi baada ya msimu wa wanyama wale kurejea katika eneo la Hifadhi ya Tarangine, tukiwa hatuna malisho ya mifugo, tukiwa na maradhi, lakini mazao yetu yakiwa yameharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matarajio yangu kwamba, sheria itakayopitishwa na Bunge hili Tukufu, itaweka utaratibu utakaotoa fidia kwa mazao yanayoharibika, kuanzia mazao ya shambani na mifugo. Kwa masikitiko makubwa sana, sheria yenyewe inazungumzia fidia kwa mazao ya shambani, lakini haizungumzii fidia kwa mifugo, imeamua kuleta *schedule of amendment* ili mwishoni kifungu hicho kinachotaja mazao, kiweze kujumuisha na mifugo ambayo mara nyingi inauawa au kuliwa na wanyamapori kama simba na chui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kuwashawishi Wabunge wa Bunge lako Tukufu, waunge mkono marekebisho niliyoyawasilisha kwenye Meza yako ili yaweze kufanyiwa marekebisho. Kwa maana hiyo, kuufanya Muswada huu uweze kukidhi matarajio ya wadau, kama walivyokuwa wamefanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika kifungu kidogo cha 15(4), yapo maeneo ambayo yamekuwa yakitumika kama *relevant authorities*. Nilikuwa naliomba Bunge kwamba, baadaye liendelee kumshawishi Waziri na Wataalam wetu wa Sheria, waweze kutoa *definition* ya *Relevant Authorities* ili pale ambapo itahusu maeneo ya ardhi ya vijiji, basi *relevant authority* iendelee kuonekana ni Halmashauri za Vijiji na Mikutano Mikuu ya Vijiji, kwa mujibu wa Sheria Namba Tano ya mwaka 1999.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefarikjika kuona Serikali na hasa Waziri mwenye dhamana, amekubaliana na pendekezo la wadau na kuona kwamba, *game controlled area* sasa yatakuwa nje ya ardhi ya vijiji. Ningetaka kuishawishi Serikali iendelee na msimamo huo, kama ilivyobainishwa katika moja kati ya vifungu vya sheria hii, lakini iangalie sana kifungu cha mwisho cha 121, ambacho kinaendelea kusisitiza pamoja na mambo mengine, kuheshimiwa kwa *regulations* na sheria zilizokuwepo au maamuzi yale.

Katika kipindi hicho cha *transition* ni vizuri basi Waziri baada ya miezi hiyo 12, zile *regulations* zilizokuwepo mwanzo ziweze kufutwa.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kulishauri Bunge letu na kuishauri Serikali kwamba, wakati wa kutenga maeneo yale ya Ushoroba, Mazalio na maeneo ya Mtawanyiko, kwa upande wa wanyama basi kwa kuwa ardhi hiyo inakuwa katika ardhi za vijiji, basi mikutano ya Serikali za Vijiji na Mikutano Mikuu ya Vijiji ishirikishwe ili iweze kupata *concern* ya wale ambao wanamiliki maeneo hayo kisheria.

Mhehsimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa sana kulisisitiza ni suala la vitalu vya uwindaji.  Inasikitisha sana kuona Muswada huu bado unapeleka madaraka kule Dar es Salaam Makao Makuu; kwamba, uwindaji unafanywa katika ardhi za vijiji, lakini hakuna maoni ya uongozi au mamlaka za vijiji hawapewi fursa ya kuweza kutoa maoni yao.  Inapendeza sana kwamba, yule ambaye anakusudiwa kutoa nafasi ya kuwinda katika kijiji A, na B basi aweze kupata maoni ya mikutano mikuu ya vijiji hivyo na itawafanya hawa wanaopewa *hunting blocks* hizo waendelee kuwaheshimu hawa wananchi wasiendelee kuwa *loyal* tu kwa Mkurugenzi wa Wanyamapori, Katibu Mkuu na kwa Waziri mwenye dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu ambao wapo kwenye Wilaya yangu, sitaki kuwataja majina leo, kwa sababu hawatapata fursa ya kujitetea; lakini ninataka kusema kwamba, wananchi wangu wamewachoka, hawawaoni waliko.  Mimi nilikwenda kwenye maofisi yao ili wachangie Miradi ya Maendeleo katika maeneo wanayowindia, sijawaona mpaka leo; kama mimi Mbunge imenichukua miaka mitatu na nusu kuwatafuta na siwapati, sasa Mwenyekiti wa Kijiji na Serikali ya Kijiji watawapata wapi?  *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wanafanya hivyo kwa sababu wanajua Serikali za Vijiji na Mikutano Mikuu ya Vijiji haihusishwi katika ugawaji wa vitalu hivyo. Yaondoeni madaraka kutoka Dar es Salaam, yarejesheni sasa kwa wale wanaowafanya wale wanyama wawepo na ambao ni Mikutano Mikuu ya Vijiji na ndiyo wenye ardhi zao.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimependekeza hilo la mifugo kuongezwa katika maeneo yatakayotolewa fidia, lakini suala la fidia kuendelea kuonekana kama ni kifuta machozi, nimeleta marekebisho ili hii ionekane kwamba ni haki; ng’ombe wangu wameliwa, mazao yangu ya shambani yameliwa halafu wewe unaniambia unanipa kifuta machozi.

Nimeleta marekebisho ili tuweze kupewa *compensation*, ambayo inalingana na thamani halisi ya madhara yaliyosababishwa na wanyama wale.  Mkiuona mzigo huo ni mkubwa, rejesheni mamlaka ya wanyama hao kwa vijiji vyetu, tutawalinda na tutavulimia uharibifu wao, lakini tutafaidika nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa maeneo ambayo pia nilikuwa nimeomba marekebisho ni eneo hili linalihitaji fidia.  Mimi nimeiweka kama *damages* au *compensation* badala ya kubaki kama *consolation*, ambayo ipo katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo ningependa kuligusia kama muda wangu utaruhusu ni wafugaji kuendelea kuonekana kama Watanzania daraja la pili. Ukienda Morogoro kule Kilosa, mauaji yanayofanyika na taarifa zinazoripotiwa kwenye vyombo vya habari, inaonekana kama wafugaji ni kundi moja lililozuka la ajabu ajabu linaloharibu mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja, baada ya marekebisho ambayo nimeyaleta mezani. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nilishtuka kidogo nilidhani unataka kuniruka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye hoja yenyewe, kwa sababu muda wenyewe ni mfupi na nina mambo matatu ambayo nilitaka niyazungumze. Kwanza, kabla ya yote, ninaomba ni- *declare interest,* nimefanya kazi katika Wizara hii kwa kipindi cha miaka tisa huko nyuma, nikiwa kama Afisa Mafunzo. Kwa hiyo, naielewa kwa kiasi kikubwa tena vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja, kwenye niliyotaka kuyasema, mwishoni nitaeleza nayaunganishaje na Muswada huu. Kilindi tunayo *game controlled area*, tuna mbuga ambayo na Wizara ina taarifa nayo; ambamo ndani kuna vijiji vya wafugaji takriban vitongoji viwili na kitalu kimoja cha wawindaji. Halmashauri ilikuwa na mtaalam mmoja aliyemaliza SUA mambo ya *wildlife management,* lakini alipokwenda masomoni alikuwa peke yake. Tulipewa ikama kwa ajili ya kuajiri watu wanne, ikasemekana wamekosekana watu wenye sifa, kwa hiyo, mpaka sasa hatujaajiri. Sasa hivi tumepata *ranger* mmoja kutoka Handeni, ambaye ndiyo anafanya kazi hiyo. Utashangaa sehemu kama hiyo kuwa na *ranger* mmoja, ambaye hata vitendea kazi hana na Mbuga haina hata *post* moja!

Niliomba fedha Wizarani kwa kushirikiana na Halmashauri yangu, tuliahidiwa lakini baadaye tukakuta tumekatwa. Baada ya mjadala mgumu, nadhani tumerudishiwa japo fedha hazijafika. Imani yangu ni kwamba, Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wananisikia na wataweza kusimamia angalau hizo fedha ziweze kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji wa kitalu hicho wana matatizo sana; watu ambao wamekuwa wakiingia, wana matatizo yao binafsi ya kiutendaji na wanawinda pale bila utaratibu. Hali kadhalika, mapato yamekuwa madogo sana kiasi kwamba, kwa mfano, mwaka jana ile asilimia 25 kwa vile vijiji tisa vinavyozunguka, wamepewa milioni mbili na kitu, ambayo ni kama hakuna. Wala hakuna huduma zozote za jamii ambazo zimetolewa na watu hao. Nitaeleza baadaye, kwa nini ninawaunganisha na Muswada huu.

Ukurasa wa 18 nimeweka zaidi *concentration* yangu, kwenye hivi vifungu ambavyo vinahusu watu wangu. Katika kifungu cha 18 ukurasa wa 23(2)(b), nadhani ni *typing error,* pale ambapo inasema *impose a fine of not less than 300 shillings but not*

*exceeding 500 shillings*. Nadhani mnaongelea 5,000. Nadhani mnaongelea *300,000/= not exceeding 500,000/=,* naomba basi mrekebishe ili isomeke vizuri, baadaye tusije tukashikana kwa vifungu hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye hivi vipengele vya 18, 19, na 20, japo wengi wamezungumza, lakini nalilazimika kusimama na kuyasemea, kwani yananitia wasiwasi sana kwa sababu Muswada ukishapita ina maana imekuwa sheria. Sisi hatujaanzisha *WMA*, nina wanakijiji wangu wanakaa mle ndani, yale yote ambayo yameandikwa kama *restrictions* ndiyo yanayoendelea kwa wakati huu. Sasa najiuliza; itakuwaje kwa zile jamii zangu za wafugaji, isije ikawa mshikemshike, masuala haya tunaanza kusumbuana kisiasa kuweza kuwatoa watu. Nilikuwa naomba nijue kabla ya hiyo *WMA*, maana ukiangalia sisi hatuna wataalam, hatuna ujuzi. Sasa hapa ningependa Waziri anieleze kitatokea nini kabla ya kipindi hicho au hawa watu wataendelea kukaa hata kama sheria imepitishwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao skauti wengi, lakini tunaambiwa hawana sifa za kuweza kuajiriwa. Sasa nilikuwa naomba kwa Wilaya ya Kilindi, tupewe kibali tuwaajiri hawa kwa muda mpaka hapo watakapokuja wataalam ambao tunasema wanafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme hapa, kuna tatizo kubwa Wizarani. Mheshimiwa Waziri, anapata tatizo na hata juzi nilisikitika sana; tatizo ni kwamba, ushauri anaopata nadhani uko chini ya kiwango. Kuna tatizo kubwa sana Wizara hii hususan kwa Idara hii ya Wanyamapori, ambayo naifahamu naisemea hiyo. Wapo watu wenye uzoefu wamewekwa benchi, mtanisamehe lakini inaumiza. Kuna mtu anaitwa Charles Mdoe, huyu amefikia mpaka kukaimu Ukurugenzi; a Maafisa Wanyamapori nchi nzima wanamfahamu. Tume ya Mzindakaya ameshughulika nayo na wametoa mapendekezo ambayo hayakuzingatiwa, baadaye Waziri akaelezwa kitu kingine cha ajabu, ndiyo hicho kimemletea aibu juzi; huyu mtu kakaa benchi eti kahamishwa pale kwenye idara akaletwa TAMISEMI, TAMISEMI hawajui wampeleke wapi *over qualified*, wakampeleka Morogoro, Morogoro wakasema tumfanye nini, mtu ana karibu mwaka yuko nyumbani!

Hii ni kamusi ya wanyamapori, sisi tulikuwa tunawatumia hawa watu na kazi zilikuwa zinakwenda, ameachwa tu amebwagwa. Mama Tibanyenda, *very senior* yuko TAMISEMI amekaa, utamkuta anasoma magazeti mara moja ikitokea sijui kozi gani aende kule kama *resource person* au akasikilize. Bwana Gamasi, Mkuu wa Chuo cha Mweka, amebwagwa pale Wizarani, kazi anazofanya hazieleweki; hawa ni watu wanaojua sekta ya wanyamapori na wanafahamu kila kitu. Hizi taarifa sisi tulikuwa tunaambiwa takwimu hazipo, kwa kweli nilimsikiliza kwa sababu Waziri anakuwa *misled.*

Idara ya Wanyamapori takwimu zote za wanyama zinafahamika, ukienda TAWIRI utazipata siyo kitu cha kupoteza muda. Kama sisi tunawaweka benchi watu wenye uwezo tunategemea nini? Kama waliobaki ni watu wenye uwezo, basi mshaurini Waziri kinachoeleweka, inatuuma sisi kama wanawake; wanawake tunataka kuonyesha

tunaweza, tunafanya kazi na kweli tunaweza, lakini utokana na ushauri, kwa sababu yeye Waziri hawezi kufanya kila kitu, lazima a-*delegate*. *(Makofi)*

Sasa mimi ninaomba kabisa, Mheshimiwa Waziri nenda ukaulizie hawa wataalam wanafanya nini wako nyumbani? Huyu mtu nimeongea naye jana, ili kuhakikisha kwamba ninalosema ni sahihi, akanimbia mama niko huku kwangu nauza mayai na chakula cha kuku. Hivi kweli; halafu tunalalamika hatuna wataalam wenye uwezo? Hili tatizo lazima liishe. Tuache mambo mengine, tuzingatie ubinadamu, uzalendo wa kuangalia Tanzania katika sekta zote, inatoka hatua moja kwenda nyingine, kwa kutumia nguvu tulizonazo, fedha na rasilimali watu kama hiyo. Ninaomba hata Waziri aje atupe *briefing* baadaye kuwa hawa watu wamepangiwa vituo vinavyoeleweka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kwa upande wangu ukurasa wa 31, hili ni suala la *Hunting Blocks Allocation Advisory Committee*. Mimi nilikuwa nasema, sijui kama wenzangu wamelisema huko nyuma, lakini nilikuwa naomba, inapendekezwa tena Mwenyekiti awe ni mtumishi wa umma. Mimi nilikuwa naomba siyo watu wenye uwezo wa mambo ya wanyamapori tu ambao wako utumishi wa umma, hebu tutoke huko kidogo maana yake wanaofuatia wote wako kwenye utumishi wa umma. Nilikuwa nafikiria kwamba, labda huyu Mwenyekiti, tungeangalia atoke kwingine kokote ilimradi awe na utaalam na uelewa wa masuala ya *hunting* na sekta hii kwa ujumla itasaidia. Tumeona hivyo kwenye mashirika mengine, mradi unampata mtu nje, maana mkishachukuana wote Watumishi wa Serikali inakuwa vipi? Mimi nilikuwa naomba hilo tuliangalie sana kwa macho ya umakini, inaweza ikatuletea shida.

Kipengele kingine hapo hapo 3(d), ukurasa wa 32, kuna mmoja wa Wajumbe, ambaye ni Mkuu wa Chuo cha Mweka, nimeangalia hadidu za rejea *(terms of reference),* sioni kwa nini Mkuu wa Chuo cha Mweka awekwe pale? Sioni chochote kinachohusiana *na college or whatever* hapa kwenye hizo hadidu za rejea kwenye *hunting blocks*. Isitoshe vyuo vinavyotoa elimu ya wanyamapori kuna SUA wanatoa *wildlife management,* Pasiansi kinatoa japo kwa ngazi ya chini lakini ndiyo kinachotoa watenda kazi asilia; *why specifically* Mweka? Mimi nilikuwa nafikiria hili suala la Mweka, tungeliacha kwanza, sioni sababu yake na hata ukiangalia kwenye *terms of reference,* hakuna kinacholenga kwenye chuo ambacho kinatoa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mengi yamesemwa ya kwangu yalikuwa ni hayo, Mheshimiwa Waziri kwa leo nitanyamaza kimya sisemi chochote kuhusu kuunga mkono hoja au kutounga. *I sympathize,* ni juu yako mpira uko miguuni pako, wewe ndiye unayejua ufanyaje nini ili ufunge goli, amka ufanye kazi tuko nyuma yako tutakusaidia kukupa taarifa nyingine. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja hii ya Muswada wa Wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa kuandaa vizuri kabisa hoja hii na baadaye kuiwasilisha kwa kiasi ambacho imeeleweka vizuri sana kwa walio wengi. Ninampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii, kwa namna ya pekee kabisa, kuwapongeza wataalam wote ambao wamehusika katika kuuandaa Muswada huu na hivyo kuuwezesha kuwasilishwa ndani ya kipindi cha miaka kumi. Ninadhani sote tunajua kwamba, ulianza kuandaliwa tangu mwaka 1999 na sasa unapowasilishwa ni mwaka 2009 na kwa kweli wangezembea pengine ungechukua muda mrefu na kuwasilishwa miaka ya mbele labda tuseme hata mwaka 2011.

Kwa kuzingatia kwamba, Muswada huu ulikuwa na changamoto nyingi na nzito na wakaweza kuuwasilisha katika kipindi hiki, wanastahili pongezi.

Vilevile tuipongeze Wizara chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, kwa sababu ninaamini kabisa, hawa wameweza kutoa msukumo mzuri kiasi kwamba, wameweza kufanikisha. Ninadhani hawa wangelalala, wangechelewa kuwasilisha Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu unahusika sana na usimamizi bora wa mazingira, hasa kwa kuzingatia matumizi endelevu ya maliasili, hifadhi ya mazingira na ustawi wa jamii. Kwa hiyo, una kila sababu Muswada huu kuungwa mkono na kwa maana hiyo basi na mimi ninaungana na wenzangu kusema kwamba, ninauunga mkono Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kuyataja hayo mambo matatu; yaani matumizi endelevu ya maliasili, hifadhi ya mazingira na ustawi wa jamii; ningependa niongelee jambo moja tu la ustawi wa jamii. Ninazungumzia hili kwa sababu moja kwamba, mambo mengi sana yamejitokeza katika Muswada huu, ambayo yanazungumzia ustawi wa jamii, lakini yamekuwa hayatafsiriwi moja kwa moja na baadhi ya wananchi au pengine watu walio wengi.

Kwa namna hiyo basi, ningependa nizungumzie suala la *WMA,* ambalo lipo kwenye kifungu cha 30 na kifungu cha 68 ambacho pia kinazungumzia udhibiti wa *Human Wildlife Conflicts,* pamoja na kifungu cha 7(8), ambacho ni uanzishaji wa ile Mamlaka ambayo Waheshimiwa Wabunge wengi wamekuwa wakiitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ustawi wa jamii tunaweza kuupata kutokana na uanzishwaji wa *WMA* kwa mambo yafuatayo:-

Kwanza kabisa ni zile shughuli za utalii ambazo zinaweza zikawa zinaendeshwa na hizi *WMA*, ambapo hapa utakuta kwamba, wananchi wengi ambao wanaishi katika maeneo hayo yenye WMA wanaweza wakaajiriwa, kutokana na hayo basi wanaweza wakaongeza kipato.

Vilevile wanaweza kuendesha shughuli nyingine za kijamii, kwa mfano, shughuli za kielimu, ujenzi wa shule, shughuli za afya kama ujenzi wa zahanati na mengineyo. Mfano mzuri unaweza kuonekana kwenye *WMA* ambayo tuliweza kuiona kule Fort Ikoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine la udhibiti wa wanyama waharibifu, ambalo tunaliona katika kifungu cha 68 na hii ni njia mojawapo ambayo Wizara inazungumzia udhibiti wa *human wildlife conflicts.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika udhibiti huu wa wanyama waharibifu, tunaweza kupata faida hapa katika ustawi wa jamii kwa namna nyingi; lakini mojawapo ni ile ya kuzuia uharibifu wa mazao kwa njia ambayo labda tunaweza tukaisema siyo ya moja kwa moja, lakini itamwezesha mwananchi kupata kipato pale anapolima na kuhakikisha kwamba mazao yake yanakuwa salama kwa kipindi chote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia kile kifungu cha 7(8), ambacho kinahusu Uanzishaji wa Mamlaka katika maeneo yale ambayo yanasimamiwa na *Wildlife Division* ya Wizara. Mamlaka hii itafanya kazi kama vile *TANAPA* na *Ngorongoro Conservation Area Authority*, ambapo wananchi wanaweza kufaidika kwa njia mbalimbali; kwanza, kwa kuajiriwa katika mamlaka hii kwa kuwa kuna upungufu mkubwa sana katika maeneo mengi ya hifadhi hizi ambazo zipo nje ya *Ngorongoro Conservation Area* na nje ya *TANAPA*, kwa mfano, *Selous* kuna upungufu mkubwa wa watumishi. Kwa hiyo, tutakapokuwa na Mamlaka hii, itaweza kuajiri watumishi wengi na hivyo kuwawezesha kuongeza kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile kuna suala moja la ujirani mwema, ambapo Mamlaka ya Ngorongoro, huwasaidia wananchi katika maeneo ilipo na wengine pia kule ambako *TANAPA* ipo, huwa wanafaidika na miradi hii. Kwa hiyo, maeneo haya kwa mfano, Selous na maeneo mengine, yatakapokuwa yanasimamiwa na hii mamlaka ni wazi kwamba, wananchi watafaidika kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia hayo masuala kwa kifupi, kuhusiana na ustawi wa jamii, ningependa sasa nitoe mapendekezo machache kama ifuatavyo:-

Pendekezo la kwanza, ninajua tunatarajia kwamba siku zijazo baada ya kuupitisha Muswada huu, basi tutaandaa kanuni. Ningependekeza kwamba, hizi kanuni ambazo tutaziandaa, zitafsiri moja kwa moja kwamba ni kwa ajili ya kumnufaisha mwananchi. Sheria hii ya *Wildlife* iwe ni ya kumnufaisha mwananchi na siyo kumnyanyasa kama vile ambavyo wananchi walio wengi sasa hivi wamekuwa wakifikiria kabla ya kupewa ufafanuzi.

Vilevile masuala ya uanzishaji wa *WMA* yasisubiri muda mrefu, kama uwezekano upo wa kutanguliza hata zile *guidelines* za jinsi ya kuanzisha *WMA* ni vyema wakawezeshwa wananchi hawa kuzianzisha *WMA* hizi ili ziweze kuwasaidia na pia kuna uhifadhi. Kwa sababu nadhani tumekuwa tukitegemea sana au tukiamini haya masuala ya *common property resources* ambazo ni mali ya jumla isiyokuwa na mwenyewe, lakini tutakapokuwa na *WMA*, tutakuwa na *commonly owned property,*ambapo wamiliki sasa watakuwa ni hawa wanakijiji. Kwa hiyo, kwa namna moja au nyingine, tutakuwa na uhifadhi ambao ni endelevu na vilevile tutakuwa na matumizi endelevu ya maliasili zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalo la tatu, ambalo linahusiana sana na ile migogoro ya wanyama na binadamu. Kuna kifungu cha 73 ambacho kinaelezea kwamba, makazi au shughuli zozote zinazoweza kuathiri wanyamapori, zisifanyike ndani ya mita 500 kutoka kwenye mipaka. Nimekuwa nikijiuliza kwamba, hapa sijui tunawezaje tukazuia migogoro hii maana hapa tunazungumzia tu kwamba pengine tusiathiri wanyamapori? Sasa kwa upande wa wanadamu, siyo rahisi kuwa-*restrict* wanyama kwenda kwenye makazi. Mara nyingi mauaji yanapokuwa yakitokea katika maeneo mengi na hasa kule Nanyumbu, taarifa katika vyombo vya habari zimekuwa zikisema kwamba, wanyama wale wanakuwa wakienda kwenye makazi ya binadamu wakitafuta maji.

Kuna mfano mmoja, wenzetu wa Namibia wao walisema kwamba, katika maeneo mengi migogoro hii imepungua, kwa kuwawekea *water points* wanyama kwenye maeneo yao; na hivyo kuwazuia wasiweze kuingia katika maeneo ya binadamu. Vilevile kuhakikisha kwamba, wananchi wale wanaoishi karibu na zile mbuga za wanyama, wanawekewa maji katika maeneo ya karibu. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani ni vizuri katika kanuni, Wizara ikaliangalia hili ili kuweza angalau pale inapowezekana, kuwawekea wanyama yale maeneo ambayo yanataarifiwa kwamba wanyama wanawaua wananchi kutokana na kutafuta maji, basi maji yawekwe kule ndani ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina pendekezo la nne ni katika uanzishwaji wa ile mamlaka. Katika uanzishwaji wa mamlaka Wizara ijitahidi sana kuhakikisha wale watumishi katika mamlaka hawawi wale wa kukaimu kaimu kama ilivyo katika Ngorongoro kwa sasa hivi ambapo Mhifadhi Mkuu amekaimu zaidi ya miaka mitatu nadhani. Kwa hiyo, hili likiangaliwa vizuri wale watumishi watakuwa na ule utendaji kazi wa kujiamini. Kwa sababu wanapokuwa wakikaimu wanakuwa hawana *confidence* na maamuzi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina pendekezo la tano, wakati wa mchakato wa sheria, tuliwahusisha wananchi wengi wa Kaskazini ambao ni wafugaji zaidi, lakini wakati wa utungaji wa kanuni, nilikuwa nina pendekeza kwamba, wananchi wa Kusini wote pamoja na hawa wa Kaskazini, wahusike ili waweze kutoa uzoefu wao ambao kidogo ni tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina pendekezo la sita, hili ni la kiutendaji tu kwamba, maandalizi yafanyike mapema katika kuanzisha zile *Wildlife Corridors, Dispersal Areas* na *Buffer Zones* na hasa kuwashirikisha wananchi ili angalau kuweza kuzuia migogoro kati ya Mamlaka na kati ya Wizara na Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Muswada uliopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja Wataalam wote kwa pamoja, kwa kuweza kuuleta huu Muswada mbele

yetu ili tuweze kuchangia mawazo kuuboresha zaidi na hatimaye uwe kwa manufaa ya nchi hii na watu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo asubuhi nilikuwa na swali kuhusu uharibifu wa wanyama katika Jimbo langu la Pangani. Kama inavyofahamika, Pangani kuna Hifadhi ya Taifa ya Saadan, wanyama wanaongezeka na kama ilivyosema Serikali; binadamu nao wanaongezeka na kuongeza shughuli mbalimbali za kilimo. Niliiambia Serikali nayo wakiri kwamba, wanyama kama ndovu nao wanaongezeka, kwa sababu ndiyo uhifadhi. Kwa hiyo, sisi wananchi hatuna budi kulinda rasilimali hii ya wanyama kwa kushirikiana na Serikali, lakini wananchi nao wapate amani na hao wanyama ili wafanye shughuli zao kama sisi tunavyowalinda wanyama hawa. Wasiuawe na wao waone kwamba, wanaishi kwa amani na binadamu, lakini wao hawana akili kama sisi; sisi ndiyo tuna mawazo mazuri ya kuweza kuwadhibiti wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa lengo langu ninataka kusema kwamba, hii sheria inayokuja, nina hakika itaboresha mambo mengi, pamoja na kuweka taratibu nzuri za kuwalinda binadamu na hao wanyama waharibifu. Zipo njia nyingi kama Muswada unavyosema, lakini tukumbuke kwamba, wakati tunapofikia kuwalipa kifuta machozi au fidia wananchi hao, ambao wanaharibiwa mazao yao hasa na ndovu, Serikali inachukua muda mrefu sana kuwalipa kifuta machozi na ile ilikuwa ni rasilimali yao, ambayo ilikuwa inawaendeshea maisha. Baada ya kuondokewa na rasilimali zile, wamekuwa maskini zaidi na lengo la hifadhi ni kuwafanya wananchi wa maeneo yale wajikwamue na tatizo la umaskini ili waweze kuishi vizuri zaidi kwa kuitumia hifadhi ile na wao wafaidike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali inapochelewa kulipa kifuta machozi, inarudisha nyuma. Serikali inaposema kwamba, wanafanya uhakiki; mimi ninataka kusema kwamba, kwa uzoefu ambao tumeupata pale Pangani, minazi ile ilianza kuharibiwa mwaka 2004. Nilitoa hoja binafsi hapa Bungeni na Wizara ya Maliasili na Utalii ilikwenda kuchunguza, hatimaye taarifa ile ilipotoshwa na baadhi ya watu. Baadaye waligundua kwamba, ile taarifa ilikuwa ni ya kupotosha, lakini ikachukua muda kuwalipa kifuta machozi. Wasisahau kwamba, ndovu wale waliendelea kufanya uharibifu, pamoja na ile orodha ya zamani kwa kipindi chote hiki cha kutoka mwaka 2004 mpaka sasa, wameendelea kufanya uharibifu. Sasa watakuta yale majina yanajirudia, siyo kwa maana ya takwimu za nyuma, isipokuwa kwa sababu wale ndovu waliendelea kushambulia mazao yao.

Mimi sizungumzii mahindi, tunazungumzia minazi. Sasa ndovu anaingia anavunja labda minazi 200 anaondoka, mwaka ujao anarudi pale pale anavunja minazi mingine 100. Sasa utakuta lile jina linarudia, kwa sababu shamba la yule mwananchi halikumalizwa lote. Inafika mahali pamoja na kwamba, aliyeathirika kipindi cha kwanza kwa kuharibiwa mazao yake akafikiria Serikali itamsaidia, lakini mara ya pili ile wanaingia ndani na kuharibu tena minazi mingine. Hali hii inawakatisha tamaa, hatimaye inaonekana kwamba na sisi wawakilishi wao hatuwashughulikii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana ukaona kila mara tunauliza masuala ya fidia, juu ya wananchi wanaoharibiwa mazao yao kwa mimi ni minazi. Mnazi unachukua miaka saba mpaka uanze kuvuna, lakini ndovu anaingia kwa mara anavunja minazi 100. Anauwekea kifua mnazi unaanguka, anachukua zile nazi ndogo ndogo anameza, baada ya muda *digestion* hakuna inatoka kama ilivyo. Sasa kwa kweli yeye akifanya hivyo, anaona ameshimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba, pamoja na Muswada huu unaokuja, ninaamini utaboresha mambo yote haya, lakini tuharakishe kulipa kifuta machozi wananchi hao ili watafute maeneo mengine ambayo wamekwishayatayarisha ili waendelee kushughulika na shughuli zao za kilimo ama sivyo tutakuwa tunawakosesha haki yao na ni ya msingi. Wanayo haki ya kuishi kama tulivyokubaliana kwamba, waishi pamoja na wanyama, basi na wao tuwape *priority* kama tunavyowapa wanyama wale. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni kwamba, sheria iangalie vizuri kuhusu masuala ya *WMAs*; ni sera nzuri na tumekwishaona inawasaidia wananchi wengi. Hifadhi mpya hizi kama ya Saadan ambayo ipo Pangani, hili ni jambo geni kwetu na hifadhi sasa hivi imeshapita muda wa miaka mitatu, minne, wale wananchi wanatakiwa wapewe elimu ya juu ya *WMAs.*

Hivi sasa wanajitokeza watu katika maeneo yale, ambao wanaelewa maana ya kuwa jirani na hifadhi. Watu hao wameanza kuhodhi maeneo katika maeneo yale, kwa maana siku za mbele wataanza kuweka miundombinu ya ujenzi wa mahema, bila wanakijiji kuelewa. Tukiweka utaratibu mzuri katika hili na hatimaye kuwakodisha au kuwapa maeneo, hao ambao wanataka kuweka *camps* ili wafaidike vizuri; mkichelewa kufika na wao watakuwa wamekwishakula hasara, kwa sababu walikuwa hawaelewi na maeneo wamekwishamaliza kuyatoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba baada ya kupitisha Muswada huu, Idara ya Wanyamapori na nimekwishazungumza na Bwana Tarimo, tafadhali njooni kule Saadani katika Wilaya ya Pangani, muwaelimishe wananchi. Tunapakana na Bagamoyo kwa upande wa Chalinze. Watuandalie michoro ya jinsi ya kupanga mipango mizuri ya kuweka sio hoteli, labda *tents* zaidi ili zinapojengwa zile *tents* na kijiji kiweze kufaidika na mapato yatakayotokana na uendelezaji ule wa utalii. Hilo ni la msingi, lakini ni lazima kuwe na mipango endelevu, lazima kuwe na michoro itakayoonesha ile *master plan* ya eneo lile itakuwa vipi katika eneo la kijiji na hatimaye wale wanyama watakapokuwa wanakuja katika maeneo yale, basi na hapo watalii waweze kunufaika na kijiji na wananchi wote kwa ujumla wanufaike. Hilo la pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalotaka kusema ni *special case* kwa sisi watu wa Pangani; ni kwamba, hifadhi yetu inapakana na bahari au iko baharini, upande wa *coast* na wanyama wanavuka kwenda kuramba chumvi katika eneo lile. Kwa hiyo, pale tuna hifadhi ya wanyama na tuna *beach*, pamoja na kuwa ni kivutio kizuri cha utalii, lakini sasa yale maeneo ya *beach* ni mashamba ya watu na wamekwishakuja niseme wengi wao wanajiita wawekezaji, lakini ni *speculators*, wameshanunua yale maeneo

tayari. Mtu anapouza lile eneo lake, huwezi kumkataza asiuze, hatuna mamlaka hiyo na wala Serikali haina mamlaka, isipokuwa tutazitumia sheria kuhakikisha kwamba, utaratibu wa kuuza kupima yale maeneo na kuacha hatua 60 au mita 60 kutoka baharini, hayo ni masuala ambayo yapo katika Wizara ya Ardhi na tuhakikishe kwamba hizi taratibu zinafuatwa. Kinachotia wasiwasi sasa ni kwamba, hatuna *master plan* inayoonesha hizi hoteli zitajengwa kwa utaratibu upi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakuja kujikuta tunajenga hoteli nyingi katika eneo dogo, kwa sababu ni eneo ambalo linavutia sana watalii na hatimaye kutakuwa hakuna maeneo au nafasi ya kutosha kwa wale watalii watakaokuja katika zile hoteli. Kutakuwa na msongamano na hasa kule *beach* na itaharibu mpango mzima wa ule utalii unavyotakiwa, kwa maana ya kuhifadhi mazingira na ile *eco-system* ibaki kama ilivyo. Sasa sijui Wizara ya Maliasili na Utalii itasemaje, lakini ninaiomba ikishirikiana na Wizara ya Ardhi, kwa makusudi kabisa katika maeneo haya ya ufukwe, kuwe na *master plan* ni jinsi gani hizi hoteli zijengwe.

Tukiwaachia wale wanaojiita wawekezaji, wajenge kama wanavyotaka wao; *eco system* ile na mazingira ya hifadhi katika maeneo yale itabadilishwa na hatimaye inawezekana kabisa tukawasogeza wale wanyama wasiweze kupata ule uhuru wa kufika kule *beach* na kulamba ile chumvi. Hiki ni moja ya kivutio kwamba, wewe upo *beach* inawezekana mita 200, ukakuta yuko mnyama kule, ukapiga picha na hatimaye ukafurahia utalii ule. Hilo namwomba Mheshimiwa Waziri, atakapokaa na wataalam, wajaribu kuona tunafanyaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni mipaka kati ya vijiji na hifadhi. Ramani ya hifadhi ipo, kama kule Saadani na au niseme vijiji vinavyopakana na hifadhi, vyote vimepimwa na kuna ramani zake. *Practicaly*, kwa maana ya *physically*, ukienda katika maeneo yale, *beacons* zilipo na barabara za hifadhi zinapopita, barabara hizo zimeingia ndani ya vijiji, lakini *beacons* zipo nyuma. Wanavijiji wanalalamika kwamba, *TANAPA* wameingia ndani ya eneo la kijiji. Nimewauliza wameingia vipi? Wamesema wametengeneza barabara ndani ya kijiji na walitegemea zile barabara zitapita mpakani kati ya kijiji na hifadhi.

Sasa hili ni suala la maelezo mazuri na wananchi waeleweshwe na hatimaye Wataalam wafike kule *physically*. Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, mimi ninawaomba mje mtembee, ninawaalika mje mjionee hali halisi ilivyo na hatimaye tuwape matumaini na kuwaondolea wasiwasi wanakijiji kwamba, Serikali imeongeza maeneo ya hifadhi kinyemela kwa sababu mipaka inajulikana na imo ndani ya ramani. Tukifanya hivyo, tutakuwa na maelewano mazuri na wananchi na watakuwa na moyo wa kuwahifadhi wale wanyama na mahusiano mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake. Kusema kweli, Mheshimiwa Waziri, kazi hii anaiweza na anaimudu. Ninapenda kumtia moyo kwamba, kuteleza sio kuanguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, wenzangu wamezungumza mengi sana na nisingetaka kurudiarudia, isipokuwa ninakwenda kwenye Muswada moja kwa moja. Katika Muswada huu, nimefurahishwa na mambo mengi; mojawapo ni zile *objectives* za Muswada huu na zipo nyingi, lakini moja ambayo imenivutia ni kifungu cha 5(k). Kifungu hiki kinazungumzia kwamba, makusudi ya Muswada huu, kwa Lugha ya Kiingereza *is to mitigate human-wildlife conflicts wherever they occur*.

Mheshimiwa mwenyekiti, hili ni jambo zuri sana kwa sababu mara nyingi nimekuwa nikisimama hapa nikigombana na Mawaziri, kuhusiana na matatizo ya wanyamapori na wananchi wangu wa Jimbo la Karagwe; nitalizungumzia hapo baadaye. Pili, kifungu cha 30(2) nacho ni kizuri sana, kimenivutia kwa sababu kinazungumzia kukuza uchumi na kupunguza umasikini. Sehemu ambayo ni muhimu kwangu ni ile inayosema kwa Kiingereza, *enhancing economic development and poverty reduction.* Mimi ninafarijika zaidi kwa Muswada huu. Kama ilivyo kawaida, Muswada mara nyingine unakuwa na upungufu wa kawaida, ambao ningetaka niuzungumzie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha kwanza ambacho nilitaka nikizungumzie ni cha 5(2), kinachozungumzia namna ya kuchukua ardhi ya mwananchi yeyote au ya kijiji ili kuifanya ardhi hiyo iweze kuwa ya hifadhi. Kifungu hiki kimeendelea kuzungumza kwamba, kama ardhi hiyo itachukuliwa, itakuwepo *fair compensation* ya hiyo ardhi. Mimi ningependa kusema kwamba, Serikali katika hili iwe makini sana, kabla haijachukua ardhi ya watu ni vizuri malipo yakatangulia na wakapewa muda wa kutosha wa kuweza kuondoka maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kingine ambacho ni muhimu sana hapa ni cha 17(2). Kifungu hiki kinapiga marufuku, kwa mtu yeyote kuchunga mifugo yake katika maeneo ambayo ni ya *game reserve* au eneo oevu. Ninakubaliana nacho, lakini tabu yangu inakuja pale kwenye 17(4) ambayo inataja kosa. Mtu yeyote akichungia kwenye maeneo ya *game reserve,* makosa yake ndio yananipa shida. Pale imetolewa kwamba, yeyote atakayechungia kwenye eneo hilo atatenda kosa, lakini pia imetolewa faini. Faini inayopendekezwa hapa ni shilingi laki tatu mpaka shilingi milioni tano za kitanzania na pia inapendekezwa kifungo cha miaka miwili mpaka miaka mitano. Ukiangalia *definition* ya *livestock*, yaani ya wanyama ambao watachungiwa mle, inajumuisha ng'ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe, farasi, punda na ndege pia wamo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tuwe wakweli kwamba, faini hii ni kubwa sana, hailengi kumsaidia Mtanzania bali inalenga kumkomoa. Ninasema hivyo kwa sababu wananchi wangu wa Jimbo la Karagwe ni wafugaji wa ng'ombe, mbuzi, kondoo na mifugo mingine. bahati nzuri tunapakana na Hifadhi aa Kimisi, Brigi, Ibanda, Rumanyika na Orugundu. Tuchukulie mbuzi mmoja tu ameingia kwenye hifadhi na akakamatwa na *game officer,* sheria inasema hivi; huyo mbuzi mmoja kama atakuwa

ameingia kwenye *game reserve* basi huyu mtu atozwe faini ya shilingi laki tatu mpaka milioni tano na ikiwezekana afungwe miaka miwili mpaka mitano, yaani vyote vinaweza kwenda pamoja; hivi kweli hii sheria ni nzuri kwa Watanzania? Tunatunga sheria hii kwa faida ya nani; maana sheria hii ni kali kupindukia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu akina Mheshimiwa Ole-Sendeka na Mheshimiwa Lekule Laizer wamezungumza, wao ni wafugaji pia. Mimi pia ni-*declare interest* kwamba ni mfugaji mzuri tu, tena ni mfugaji mkubwa. Ninataka niseme, kama tunatunga sheria hii, sisi tutakapoondoka hapa; Mheshimiwa Lekule Laizer na Mheshimiwa Ole-Sendeka, ng'ombe mmoja akiingia kwenye hifadhi, msije kushangaa mtakwenda jela miaka mitano kwa sababu ya mfugo mmoja tu. Sasa nilikuwa ninapendekeza kwamba, kifungu hiki kifanyiwe marekebisho, faini ianzie shilingi laki moja na isizidi shilingi laki mbili, kwa kuzingatia hali halisi ya huko vijijini kwetu. Kifungo kisizidi mwezi mmoja, miaka mitano yote ni ya nini? Vinginevyo, kama tutaiacha sheria hii ikawa hivi na ikatumika *strictly,* wale *game officers* wasipokuwa makini, wananchi wetu wengi sana wataishia jela na hilo lengo la kuondoa umaskini halitakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kingine ambacho nina *concern* nacho katika Muswada huu tunaoupendekeza ni kifungu cha 12. Kifungu hiki kinawaruhusu Watumishi wa Maliasili, kumiliki silaha na kuzitumia na sio kuzitumia kwa wanyamapori tu, kuzitumia kwa mtu yeyote ambaye atatenda kosa. Wanasema *any person who, having committed an offence;* hilo neno ni kubwa sana. Tunapozungumzia *any person who, having committed an offence* katika sheria hii, inamaanisha hata yule atakayeingia kwenye hiyo hifadhi hata kwa kutembea kwa miguu ni *offence,* atakayeingia kuchuma ua ni *offence.* Sasa huyu Afisa Wanyamapori, amepewa mamlaka chini ya Muswada huu kuhakikisha kwamba, anapoingia mle anaruhusiwa kumpiga risasi mtu yeyote, hata kama hana silaha tunaambiwa kwamba atumie risasi ya moto kuweza kumpa *punishment.* Tukipitisha kifungu kama hiki ni hatari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningependekeza kitu kimoja kwamba; ni vizuri *game officers* wawe na silaha kwenye hifadhi kwa ajili ya kujihami na majangili na ni vizuri wakatumia risasi hizo, lakini itumike kama *defence* pale ambapo *game officer* anajilinda dhidi ya wale majangili. Kitendo cha kukutana na bibi kizee au kijana anapita anachuma majani ya mboga au dawa halafu akam-*shoot;* hii haikubaliki. Kwa mfano, mtu amepita pale ana fimbo yake ya jadi, hilo ni kosa kuingia kwenye hifadhi, lakini hiki kifungu kinaonesha kwamba yule *game officer* kama hatakuwa *reasonable,* ataleta madhara kwa watu wa kawaida. Mimi ningependekeza, Mheshimiwa Waziri, aifanyie mabadiliko ya kuonesha kwamba, risasi zitumike pale inapokuwa ni lazima na hasa katika masuala mazima ya *defence.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie eneo moja, ambalo lipo kwenye kifungu ambacho mimi ninakiita ni hatarishi; kifungu cha 70(1). Kifungu hiki kinazungumzia masuala mazima ya *compensation* kwamba, mnyama yeyote akiharibu mazao au akiua mtu, Muswada huu hauonyeshi ni malipo kiasi gani atakayopata yule mwathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada unasema, hakutakuwa na *compensation* wala kitu chochote. Wanyama wakiharibu mazao, basi hicho kifuta jasho hakitazidi heka tano. Kwangu mimi kuna watu wanalima mpaka ekari 100, ekari 200, Tembo wanaingia mle, wanaharibu kila kitu. Unasema usimlipe zaidi ya ekari 5; huyu mtu atakuwa maskini na tunasema Muswada huu ni wa kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue mfano mdogo; nitumie mfano wa Mtani wangu Prof. Sarungi ni Profesa wa Mifupa, anatoka kwenye sehemu za wanyama wakali, hivi leo akakumbane na Tembo au Simba, natumia mfano tu; bahati mbaya, akapoteza maisha yake, hivi thamani ya Profesa Sarungi ni shilingi ngapi? Watu wanaomtegemea ni wangapi? Hata mimi Mbunge thamani yangu ni kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kusema kwamba ni lazima tuangalie *fair compensation* katika hii. Siyo suala la ubani kusema kwamba ni *consolation*, huwezi ukacheza na maisha ya mtu. *(Kicheko/ Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huku kwenye mifugo, tumeonyesha ukimuua Tembo au Simba, utatozwa faini shilingi kadhaa, inapokuja mnyama anamuua binadamu, unasema tutakupa tu ubani kidogo usijali! Mheshimiwa Hi sheria tukiiacha hivi, itakuwa ni sheria mbaya sana, ambayo Bunge hili limeipitisha. Lazima tujali wananchi wetu na lazima tuwasaidie. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka niliseme ni kifungu cha 99 kinachozungumzia kwamba, yeyote yule ambaye atatenda kosa, umekutwa kwenye hifadhi ukakamatwa ni jukumu lako kupelekwa mahakamani kuthibitisha kwamba wewe hukutenda hilo kosa. Mimi ninapingana na hii, kwa sababu kama wewe umemkamata mharifu kwenye hifadhi ni jukumu la yule aliyemkamata kuthibitisha kwamba, huyu kavunja sheria hii. Tusitake ku-*shift* ile tunaita *onus*, *burden* of *proof* kuitoa kwa yule mkamataji, tukaipeleka kwa yule *accused person*; tutawaonea wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, nitapenda kwenda haraka haraka. Nataka nizungumzie suala zima la ile Kamati ya Kugawa Vitalu. Hivi ile Kamati ina kazi gani? Ni Kamati ya nini? Mimi nimeusoma Muswada huu, sijaona chochote watakachokifanya zaidi ya kukaa kikao kimoja cha kusema wanataka wagawe vitalu. Hivi unataka kuniambia kwamba, Wizara yetu ya Maliasili na Utalii, haina watumishi ambao wanaweza wakafanya hii kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza ni kwamba, Kamati hii itakuwa haina uwezo wowote wa kusema kwamba, maamuzi yao ni *final*, maamuzi yote yanabaki kwa Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, mimi sioni sababu ya Kamati hii kuwepo katika sheria hii, isipokuwa ninalopendekeza ni kuwa na Mamlaka *(Authority)*; hiyo ndiyo itakayotatua matatizo na migongano yote tunayoizungumza humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niseme kwamba, kule kwetu kuna mnyama mkali, tunatumia majina yetu ya kilugha anaitwa “*entahulila*”. Yule mnyama hana masikio, ndio maana wanamwita hivyo kwamba hasikii. Mnayama huyu ni mkali sana na

ni hatari. Mwezi Desemba, 2008, alileta mtafaruku karibu kwenye Kata nzima; ni mnyama mdogo lakini hatari. Sikumwona kwenye *schedule number four* ya wanyama hatari, labda pengine wataalam baadae tunaweza tukaonana nikawasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnyama huyu ana tabia moja chafu ya kuwashambulia watu na kuchukua nyeti zao. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Blandes, nakushukurru sana kwa mchango wako huo na hasa hiyo hoja uliyokuwa unataka kumaliza nayo ilikuwa nzito. Vilevile hoja yako ya kumteua mtani wako Mheshimiwa Prof. Sarungi kama mfano humu ndani, sijui ulizingatia nini; nadhani mnaelewana ninyi kwa mahusiano yenu.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na sasa naomba nimwite Mheshimiwa Juma Killimbah, naona ameshasimama kabla ya kuitwa na Mwenyekiti. Mheshimiwa Killimbah, unawahisha shughuli kabla ya wakati wake! Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya ajiandae. *(Kicheko)*

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote, labda kwanza, nikutake radhi ya kuwahisha hii shughuli, lakini nilikuwa najua kwamba ni utaratibu na hasa pale Mheshimiwa Blandes alipomaliza muda wake wa kuzungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami pia nichukue nafasi hii, kumpongeza sana dada yangu, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii. Pili, nimpongeze Nabu wake, Mheshimiwa Ezekiel Maige, kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii, kuwapongeza Watendaji wote wa Wizara hii ya Maliasili na Utalii, kwa kuandaa Muswada mzuri, ambao una lengo la kutuongezea kipato na kuleta maisha endelevu kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niipongeze sana Kamati ya Maliasili na Mazingira, chini ya Mwenyekiti wa Bunge, Mheshimiwa Job Ndugai, kwa kazi nzuri ambapo wametoa ushirikiano wao kwa suala zima la kuleta Muswada huu katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia niweze kuwapongeza wale wote walioshinda nyadhifa mbalimbali na wapo ndani ya Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; kupitia Jumuiya mbalimbali za Chama cha Mapinduzi. Nawapa hongera sana hususan, nimpongeze sana dada yangu, Mheshimiwa Diana Chilolo, kwa ushindi mnono wa kuwa Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Singida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije moja kwa moja kwenye Muswada huu. Kwa sisi watu wa Singida na hasa ukiongelea Singida ni kweli unaweza ukasema hatuna

wanyamapori. Wanyamapori waliopo ni wale wanyama ambao hawana mazingira yanayoangaliwa, lakini pia hatuna mbuga ambayo pengine inatambulika.

Ninachoweza kusema ni kuwa, pamoja na kwamba, tumeingia katika Muswada huu mzuri, ninaomba sasa yale yote yaliyo kwa ujumla katika Muswada, kama kweli tunataka kuangalia suala la wanyamapori na suala la kuangalia misitu tengefu, tusiangalie maeneo ya upande mmoja; tuangalie pande zote za nchi yetu na ili tuweze kutoa kipaumbele mahali pale ambapo panaonekana panahitaji kupewa msukumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri, naweza kuzungumzia juu ya Mkoa wetu wa Singida; tuna kitu kilikuwa kinaitwa Mbuga ya Wembele, ambayo ilikuwa inatokea eneo la Meatu Mkoani Shinyanga na imepita Jimboni kwangu Iramba Magharibi. Vilevile inapitia katika Kata za Kidaru, Tuliya, pia imepita Kata ya Ntwike, Shelui, imekwenda moja kwa moja mpaka Mtoa na imefika mpaka Urughu ambako tunapakana na Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nazungumzia namna ya kutaka kuja kuboresha, kwa sababu najua Muswada una mambo mazuri. Sasa na kama una mambo mazuri, lazima tuelekee pande zote, kwa sababu mimi ninapozungumzia maeneo haya ni maeneo ya asili na yalikuwa na wanyama wengi sana. Pamoja na kwamba, baadhi ya maeneo yamevamiwa na yamekuwa vijiji na baadhi ya maeneo bado yapo, maeneo kama ya kutoka Msansao yaliyopo ndani ya Jimbo langu, bado kuna mapori mazuri ambayo ni tengefu. Maeneo ya Msansao, unakwenda Ujungu, ukitoka Ujungu unakwenda Urughu, haya yote mpaka Mlandala ni maeneo mazuri ambayo bado wanayama wanapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri, tutakapokuwa tunapitisha Muswada huu ambao mimi sina tatizo nao; basi tuangalie na maeneo haya tunaweza kuyapa kipaumbele cha aina gani ili wananchi wa maeneo hayo nao waweze kufaidi masuala haya ya wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumzia eneo hilo ambalo ni Mbuga ya Wembele, lakini juzi juzi mwaka 2008, Mtukufu Rais alikuja Mkoani Singida na alifika Jimbo la Iramba Magharibi. Alipofika alifanya kazi moja kubwa sana ya kuja kuuzindua msitu tengefu, ambao umezungumziwa katika Muswada kwamba, umechukua eneo lote lile la Mlima Sekenke takriban ekari 36,500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tutakapopitisha hii sheria, moja ya maeneo ambayo tunaweza sisi tukajivunia kwa watu wa Iramba, tunaomba Waziri tupate chochote kupitia msitu huo ambao umezinduliwa na Rais mwaka 2008. Msitu huu ni mzuri sana na una wanyama. Ninaomba kwa sheria hii, msitu upewe usimamizi ili tuweze kupata maslahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende haraka haraka kwa sababu nilikuwa na yangu machache ya kuzungumzia katika Jimbo langu. Nakwenda sasa kwenye kipengele ambacho kimezungumziwa sana, ambacho kipo sehemu ya nane pale kifungu cha 70(1)

na hii ametoka kuizungumzia sasa hivi Mheshimiwa Blandes. Kipengele hiki kinazungumzia juu ya suala la fidia pale mnyama anapoweza kufanyiwa madhara na binadamu. Ninazungumzia pale binadamu anapofanyiwa madhara na hao wanyama na imeeleza kwamba, huyu binadamu akipata madhara yanayotokana na huyo mnyama, fidia yake kama ilivyozungumzwa, itakuwa ni ya kukadiriwa. Papo hapo Muswada unataja bayana juu ya fidia anayotakiwa kufidiwa mnyama, pale anapofanyiwa madhara na binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaamini kabisa hata kwa sheria za nchi, pale mtu anapofanya kosa la kuuwa adhabu zinajulikana. Akipelekwa kwenye Mahakama za kisheria ma ikionekana ameuwa kwa kukusudia, kosa lake na adhabu yake inajulikana. Sasa hatuwezi kuacha sheria hii ikabaki ina-*hang* kama walivyozungumza wazungumzaji waliotangulia kwamba, ifike mahali mnyama ndio awe na thamani zaidi kwa kuonekana kwamba, akifanyiwa yeye madhara basi yule aliyefanya madhara afidie kiwango ambacho kinajulikana, lakini binadamu anapofanyiwa madhara basi pasiwepo na fidia inayojulikana! Hili ni kosa kubwa sana, lazima tufike mahali tuweke vitu bayana vitu ambavyo vitaweza kumsaidia huyu binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini hawa wanyama wapo chini ya Serikali na Serikali ndiyo yenye mali. Kama zilivyo sheria tulizonazo, maeneo ya kwetu ukiwa na mifugo ikaenda ikaharibu shamba la jirani, unayewajibika ni wewe kuweza kulipa ule uharibifu uliotokea pale kwenye shamba.

Kwa hiyo, juu ya suala la uharibifu unaoweza kufanywa na hawa wanyama hatarishi ni lazima Serikali iwajibike na itaje. Nilikuwa nataka niseme lazima ijulikane na iwe na kiwango kikubwa, sio cha kusema tu, kama hivi juzi watu wa Singida wameliwa na Simba kwa kiwango kikubwa na leo fidia yake haijulikani watalipwa nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana tutakapofika katika eneo hili, Mheshimiwa Waziri, afanye utaratibu wa kufanyia marekebisho eneo hili ili fidia ijulikane. Mapendekezo yangu ni kwamba, iwe kati ya shilingi milioni tano hadi kumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu kwa kusema, naamini Muswada ni mzuri sana na kama ulivyoelezwa, una malengo ya kutoa elimu. Muswada unaweza ukatoa elimu, mafunzo na utafiti juu ya wanyamapori na pia Muswada utakuwa unasisitiza suala la ulinzi, usimamizi na matumizi endelevu ya wanyamapori. Kwa hiyo, nataka niseme tu kwamba, Muswada ni mzuri sana na naunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, Mungu wetu apewe sifa kwa siku ya leo. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, pamoja na timu yao yote, kwa kuuleta Muswada huu lakini kama ilivyo kawaida, michango yetu ni muhimu ili kuuboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala bora ni pamoja na kufuata utawala unaozingatia sheria na sheria zilizotungwa si lazima ziwe ni sheria bora. Kwa hiyo, tunawajibika kuhakikisha kwamba, vifungu vile ambavyo vina utata, tunavizungumzia kwa dhati ikizingatiwa kwamba, wananchi wametutuma tukae kwenye hili geti ambalo ni nyeti. Kwa hiyo, tunazungumza si katika kulenga kuyeyusha au kupunguza punguza, bali kuuboresha ili uweze kukubalika na wananchi wajisikie kwamba Serikali yao inawajali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ni-*declare interest* kwamba, kuna mwananchi ambaye alichangia Muswada huu kuhusiana na kifungu namba 12(3)(a), ambacho pia Mheshimiwa Blandes amekizungumzia. Nimeona nisisitize hilo, huyo Mwananchi anaitwa Arthur Karomba, akiwa na yeye ana wasiwasi kuhusu kifungu hiki. Mimi pia sikiungi mkono, kama mwananchi amekatiza kwa sababu moja au nyingine katika zile mbuga, halafu ikaonekana ameshakosa na anatakiwa apigwe shaba. Ninadhani sio sahihi, sina nia ya kufufua hoja, lakini juzi tu Wabunge hawa hawa wamepiga kelele juu ya mtu ambaye anadiriki kumuua mwenzake ambaye ni albino; kwamba kwa nini hatua zichukuliwe mtaani bila kufikishwa mahakamani; sasa je, iweje kwa mtu ambaye yupo katika eneo la ufugaji? *(Makofi)*

Tunao wajibu wa kufikiria kama wawakilishi wa wananchi, kwa misingi kwamba, kuna mazungumzo yanaweza yakatokea kwamba, matamshi yamepita kidogo katika hali ile ya kuwakilisha lakini la msingi ni mantiki ndiyo tunayotakiwa kuipigia kelele. Sasa unakuta sisi tunahama wakati mwingine kwenye nafasi zile za misingi ya haki na ukweli, tunamtetea hata yule ambaye anadhulumu. Katika hili, huyu lazima atetewe kwa sauti zote, huyu mwananchi ambaye anakuwa yuko kwenye eneo la wanyamapori. Achukuliwe hatua kali kama hiyo ya kupigwa hata kwa chombo cha moto, endapo labda anakimbia kwa gari, angalau tutaelewa kuna helikopta ilikuwa inamfuata; wakiweza kuiwahi sawa, lakini kwa nini asichukuliwe hatua za kisheria za kawaida? *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninaomba kifungu hiki aidha kiondoke kabisa au iongezewe kwamba, endapo huyo mtu alikuwa anajaribu kukimbia, kwa kutumia kifaa ambacho hawezi kukamatwa kama vile chombo cha moto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kwa niaba ya wanawake wenzangu na vilevile wewe mwenyewe Mwenyekiti wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa uchungu mkubwa, nimzungumzie yule nyani mwanamke mwenzetu aliyekuwa analea mtoto kule porini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo haki ya kuzungumza hivyo kwa sababu ifuatayo; si jambo la kawaida nyani kulea mtoto. Imekuwa ikizungumzwa kwenye magazeti na ni jambo ambalo sio la kawaida, lakini sijajua, ninahitaji kufahamu zaidi. Baada ya kutokea hayo, yule mtoto ambaye ameathirika, kwa sababu yeye alikuwa akiishi porini kwa kulindwa na yule mnyama, wengine tunaona labda ni kitu kizuri sana au cha kawaida.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninamlinda Mheshimiwa Manyanya, kwa sababu tunazungumzia Muswada wa wanyamapori na hata nyani ni mnyama anayeishi porini, hebu tumsikilize.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninadhani mara nyingi, likiwa jambo jipya sana, wengine wanakuwa hawalipendi. Ninachotaka kusema ni kuwa, yule mtoto alikuwa akikaa porini siku zote na alikuwa akiishi katika mazingira hatarishi, lakini yule mnyama alikuwa kidete kumlinda yule mtoto. Kama sio hadithi za uwongo au kweli, ninaomba basi tuthibitishiwe kwa sababu yule mnyama alisimama kwenye nafasi ya mzazi wake.

Sawa kuna mama amejitolea kumlea, pamoja na kwamba kuna kifungu cha Sheria Na. 70 kinachozungumzia kwamba askari au ofisa akichukua hatua ya kumuua mnyama kwa maslahi ya kulinda maisha ya mtu, basi hilo ni sawa na sio kosa. Kwa upande mmoja sawa, lakini yule mnyama hakuwa hatarishi kwake. Yule mtoto sasa hivi anapelekwa kwenye TV kuzungumziwa anahitaji kusoma, lakini wale ambao wamehusika kuhakikisha mama yule ambaye alikuwa akiishi naye hayupo duniani, hawajazungumza lolote.

Kwa hiyo, nilikuwa ninafikiria kwamba, pamoja na nia njema iliyokuwepo ya kumwokoa, basi hiyo nia njema iendelee yule mtoto asaidiwe aweze kusoma kwa kutumia pesa hizo hizo tunazozipata kutokana na wanyamapori. Hii ni kwa sababu kwanza, tumepoteza rasilimali kubwa sana ya taifa kwa kumpoteza mnyama kama yule. Pili, bado naona kuna sababu kubwa zaidi pia ya kumtunza yule mtoto, yanawezekana ana mambo makubwa zaidi ya sisi kuweza kujifunza. Kwa sababu kama alikaa miaka mitano, kawaida mtoto akiwa na miaka mitatu, anakuwa tayari ameshajua kuzungumza. Inawezekana hata lugha ya wanyama anaijua, anaweza hata aka-*translate* maisha fulani ambayo sisi hatuyajui. Vilevile kuna masuala mengine ya utafiti tunaweza kujifunza. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninachoomba, mtoto yule asichukuliwe tu kama anayehangaika; ile ni *special case* ambayo haijawahi kutokea duniani, naomba kwa kweli kama mzazi, mtoto yule asaidiwe. Ninaomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa anahitimisha, atuambie mikakati itakayohusika katika kumsaidia mtoto yule, ambaye kwenye gazeti nilimsoma anaitwa Faraja Rose, basi tujue anasaidiwa na anaingia vipi katika kumbukumbu za taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, niunge mkono suala ambalo amelizungumzia Mheshimiwa Anastazia Wambura, kuhusiana na kutengeneza visima. Amesema kwa kusikia, amesikia kutoka Namibia wanafanya hivyo. Bahati nzuri niliwahi kufika *Cruga National Park*, huo ni ukweli wanyama wana akili na wanaweza kuji-*tune*; kuna sehemu ambayo imetengenezwa kabisa visima na wanakunywa maji yaliyopo. Ikitokea yale maji yamekwisha, wanakaa foleni wakisubiria kwamba muda ukifika saa kumi *motor* itawashwa na mashine zitaanza kufanya kazi na hivyo kuwapa maji. Kwa hiyo, hata kwetu Tanzania inawezekana ili kuweza kunusuru maisha ya watu wanaoishi jirani na mbuga hizo za wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusiana na mabadiliko yanayoendelea. Sasa tayari tunajiunga katika jumuiya mbalimbali; tuko kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki na pengine tukawa kwenye Bunge la *SADC* kama litakuwepo au *SADC* yenyewe ikajiunga na Jumuiya za Afrika kwa ujumla. Kwa hiyo, nilichokuwa nazungumza kuna suala la Watanzania nao kuweza kurithishwa rasilimali zikiwemo mbuga za wanyama.

Sasa basi kwa sababu hatua zake mbalimbali zinachelewa, matokeo yake hata urithishwaji wa rasilimali kama hizo unakuwa ni mgumu kutambua huyu sasa ni Mtanzania au huyu ni mtu wa nchi nyingine. Kwa hiyo, pamoja na kwamba Muswada huu unazungumzia wanyamapori, lakini niombe kwa upande wa Waziri wa Mambo ya Ndani, suala vitambulisho liongezewe nguvu ili wananchi tuweze kumiliki hizo rasilimali. Hata itakapofikia kwamba, tunaingia katika hayo mashirikisho, angalau na wewe mwananchi uweze kujulikana huyu ni Mtanzania wa asilia, huyu ni Mtanzania wa kufika, ama sivyo itakuwa ni ngumu kutofautisha kati ya yule Mtanzania wa asili na aliyeamua kujifanya Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho kabisa, niseme tu kwamba, kimsingi naupongeza Muswada na kumweleza Mheshimiwa Waziri, pamoja na timu yake kwamba, mambo yote yanayojitokeza humu ni katika kujenga. Ninaamini yaliyotokea juzi ni katika kujifunza na ndiyo wajibu wetu kama Wabunge na pia ni wajibu wa Serikali kuwa sikivu, pale ambapo Wabunge wanashauri.

Kwa maneno haya niliyoyazungumza, naomba niunge mkono hoja na niombe marekebisho hayo. *(Makofi)*

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie.

Kwanza, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Wataalam wote wa Wizara, kwa kuuleta Muswada huu. Kwa kuwa Muswada huu ulingojewa sana na sasa muhusika ni Muswada kamili lakini tunachangia visehemu vichache vichache ili kuufanya ufanane fanane na mawazo ya Kiafrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeusoma Muswada, kwa sababu umepita katika mikono ya wadau wengi, kuna mawazo ya Kiafrika na ya Kizungu humu ndani. Mawazo ya Kizungu yanatuletea matatizo; Mzungu anapothamini mnyama na binadamu, mnyama atakuwa nambari *one* na hii nafikiri ndiyo imeleta matatizo. Kwa sababu sidhani kama Waziri na timu yake hasa wangeweza kuleta Muswada hapa, unaosema binadamu akiuawa fidia yake itajadiliwa, sio haki lakini mnyama akiuawa fidia yake ni hii. Haya si mawazo ya Kiafrika. Sasa kwa sababu sisi mawazo yetu ni haya, tunaomba Mheshimiwa Waziri na timu yake, wakubali kubadilika hapa kwamba binadamu anapouawa lazima fidia yake iwe haki na itamkwe, unaweza ukaacha kutamka nambari lakini unaweza kuweka wazi kabisa ni haki na atafidiwa. *(Makofi)*

Mimi naiangalia sheria hii na kule kwangu ninakotoka, ninatokea eneo la Kaskazini la Selous, vijiji 22 vinazunguka Selous si vijiji vya kisasa. Wananchi wake hawana nyumba za *self contained*, wanatoka nje usiku kwenda kujisaidia kwenye vyoo vyao ambavyo viko mbali. Mara ya mwisho nilipozungumza, nilizungumzia juu ya mgeni aliyefika Dutumi akaliwa na simba. Sasa mwananchi huyu akiliwa na simba kule hana fidia, ila mwananchi huyu akitoka akipambana na simba akimuua lazima alipe; mimi silielewi kabisa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili lazima libadilike, nadhani ni wazo geni, linakuja kwetu kukandamizwa na mimi silikubali lazima mwananchi afidiwe.

La pili, kuanzia Kisaki Station, Mgomelo, Mngazi, Dutumi, Mvuha, mpaka Selebara, uharibifu wa mazao unaofanywa na wanyamapori hawa ni kitu cha kawaida kabisa. Ndovu anaingia kwenye shamba, anakula eka tatu anaondoka. Sasa unapomwambia huyu mwananchi kwamba, fidia yako sisi tutaifikiria, maana yake nini; watu waache kulima? Wakiacha kulima watakula nyama kwa wizi. Hawa wameishi nao miaka yote wanawalinda kwa heshima kabisa, wangeweza kuwapiga ovyo, lakini kwa sababu wanaheshimu na sisi kule tumemaliza tatizo la mpaka wa pori la Selous na wananchi, hakuna matatizo hayo.

Wale wanyama ambao wapo kwenye pori la wananchi; wananchi hawawapigi ovyo ovyo kwa kuheshimu tu. Sasa wanapowaharibia mazao yao, wananchi hawa wasiweze kufidiwa, wanapouawa wanyama wananchi hawa lazima walipe; wananchi wale hawawezi kuielewa sheria hii hata kidogo. Mimi naomba hapo ibadilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie askari wanaoishi kwenye Kambi ya Matambwe, hii ni kambi ndani ya Selous. GTZ imesaidia sana ulinzi na maendeleo ya Selous na imewasaidia Wananchi wa Morogoro Vijijini kwa elimu na kwa maendeleo, lakini mazingira wanayoishi askari wa wanyama ambao wapo Matambwe ni magumu sana. Ukienda kufanya mkutano, Ndovu anakuwepo dirishani anatafuta maji. Kule hakuna ruhusa kufunga madirisha, unakuta Ngiri wamelala chini ya magari tu na wanyama wengine. Kule ni mnyama anayetawala tabia, sio tabia ya binadamu itawale.

Nilipozungumza nao, waliniambia mishahara yao ni duni kabisa na hali zao ni ngumu kabisa, lazima wafikiriwe hawa kukaa mahali kama pale sio mchezo. Huwezi ukapiga redio unavyotaka, lazima ufuate utaratibu; wanyama wana mamlaka sio binadamu. Hata watoto wale ambao wako pale shuleni, hawawezi kuimba ovyo ovyo, kwa sababu wanyama wanaweza wakawafanyia fujo. Kwa hiyo, lazima wawe na mazingira mazuri na mojawapo ni mishahara na marupurupu mazuri ya kuwawezesha kuishi pale mahali. Ukizungumza nao, kwa kweli wanatia huruma, ila wanao moyo tu wa kufanya hiyo kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kuna mazalia ya wanyama, moja ya sehemu hiyo inaitwa Gonabisi. Mahali hapa pana maajabu kabisa, wakati wa wanyama kuzaa, wanajumuika pale wanyama wa aina mbalimbali. Sasa kule Kidunda, ambapo kijiji hicho kipo ndani ya Selous, kunajengwa bwawa la kuwawezesha watu wanaoishi Dar es

Salaam wapate maji. Sehemu ya Selous na sehemu ya hiyo Gonagusi, itazama kwa bwawa hili. Je, Wizara imechukua tahadhari gani ya wanyama hawa kwa sababu mwanzoni watakuwa wageni na wataathirika sana? Kwa hiyo ni vizuri Wizara ikajitayarisha kuwaokoa wanyama hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie wenzetu *game scouts* na maaskari wengine, ambao wanakutana na wananchi wanaoingia kwenye pori. Sisi kule kuingia porini ni kitu cha kawaida, lazima ukatafute kuni. Mabwana nyama wale au *game scouts*, wakikukuta umeingia kwenye pori, hawajali umri wako; wanawachezesha kichura chura wazee kabisa vikongwe mpaka wanazimia. Hii tabia inatoka wapi, makosa gani; mimi nawalinda wanyama na nimeingia kwenye msitu kwenda kutafuta kuni, sasa wewe unaniambia niruke kichura chura! Akikamatwa na samaki aliyemvua Mto Ruvu, anasimamiwa mpaka amalize kumtafuna mbichi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki si kitendo cha ubinadamu hata kidogo. Sasa wanaongezewa nguvu kwamba, ukiwaona wameingia na wanafanya kitendo kama hicho, wapigwe risasi. Hii sasa ni hatari kubwa, kwa sababu huyu wakati wote atakuwa na mamlaka ya kumpiga risasi mtu anayeingia kwenye pori na kueleza sababu. Mimi ninafikiri waruhusiwe kupiga risasi majangili sio wananchi wa kawaida. Mwananchi wa kawaida asiyekuwa na viatu, ameingia kwenye pori kule halafu wewe unampiga risasi eti kwa sababu ameingia hapo; sasa yeye ana nini cha kujilinda nacho? Ninadhani hili litahadharishwe; ni hatari sana kwa sababu watu watapigwa sana risasi.

Binadamu ana kiwango cha kuvumilia, kama sisi tutaruhusu kupitisha sheria hii wapigwe risasi, wao watatumia magobole kurudishia, tutawafanya nini? Mimi nafikiri tusifanye upande mmoja, lazima tumwangalie mwananchi huyu kwamba, anahitaji mahitaji mengi kwenye msitu na sio lazima afuate wanyama. Sasa ukimwona kwenye msitu, isiwe kosa la kumpiga kwa risasi; suala hili lazima tuliangalie tena. Ninamwomba sana Mheshimiwea Waziri alifikirie hili tena.

Mheshimiwa Spika, lingine ni *Wildlife Management Area (WMA)*, kule niliko mimi ipo, lakini Waheshimiwa Wabunge kupata *WMA* bado hakuwawezeshi wananchi ku-*allocate* vitalu mpaka wapate A, A. Mimi ni Mbunge kwa miaka kumi na tatu sasa hakuna, tunaomba na kufuatilia hakuna. Labda sasa tupate maelezo; hii faida ya *WMA* mpaka kupata A ili kuweza kuwa na madaraka na wanyama hao inakuwaje; wananchi wafanye nini? Maana yake tusichekelee *WMA* hapa tukafikiri tumepata, inawezekana tumepatikana, tunaomba maelezo juu ya hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu kuna pori moja, *open area*, linaitwa Mkuraza; hivi sasa kule kuna amani, wanyama kutoka Selous wanavuka Mto Ruvu wanakwenda kwenye *open area*. Kuanzia mwezi Julai, mpaka Desemba, kule hakuna amani hata kidogo; si bunduki hizo kutoka Dar es Salaam na kutoka kila mahali. Mimi nashangaa, hata kama bado hawajapigana risasi, nafikiri labda wamepigana risasi wananyamaza tu. Wawindaji wengi sana wanaingia kwenye pori hili na wengine wanaingia usiku, ambapo ni kinyume kabisa na masharti ya kulinda, lakini wanapiga wanyama usiku kwa tochi na magari.

Sasa mimi naiomba Serikali ichukue hatua na hii ni kwa sababu ya ukosefu wa maafisa wa wanyamapori katika wilaya, hata akiwa mmoja hana gari afanye nini atatembeaje wilaya kubwa kama Morogoro vijijini kote kwenda kulinda. Lazima tuwasaidie maafisa wa wanyamapori wa wilaya ili waweze kusaidia hatua za kulinda wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sheria yetu, kuna Bodi nimeangalia kazi zake ni bora iachwe tu ile Bodi basi, maana sioni inafanya nini. Bodi ipo lakini kazi sio lazima zifanywe pale. Vilevile kuna Kamati ya Ushauri ya Vitalu; inashauri nini kwa sababu hatimaye lazima mtu mmoja ataamua mwishoni, ingekuwa ile Kamati ndiyo inaamua ingekuwa vizuri.

*(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kengele ya pili.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Ya pili hiyo, mbona imekuwa haraka? Nakushukuru. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana, naona maandalizi yako yalikuwa makubwa mno lakini hakuna jinsi. Labda Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamruhusu Mheshimiwa Mpina kuzungumza, niseme tu kwamba, hoja hii tutaifanyia maamuzi kesho baada ya kipindi cha maswali na majibu. Kwa hiyo, kukiwa na mchangiaji mmoja ama wawili, tunaweza kuwapa fursa, kulingana na shughuli zetu zitakavyopangwa kesho.

Sasa kwa orodha yetu niliyonayo leo, Mheshimiwa Mpina ni mchangiaji wa pili kutoka mwisho. Mchangiaji aliyetakiwa kufuata alikuwa ni Mheshimiwa Dkt. Samson Mpanda, ambaye simwoni hapa ndani, huenda tukamruhusu yeye kesho kabla hatujahitimisha hoja hiyo. Sasa ninaomba nimwite Mheshimiwa Mpina, kama mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku hii ya leo.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Wenzangu wamezungumza kwa kirefu sana, juu ya fidia ya uharibifu wa mali, kudhuru, kujeruhi na hata kuua binadamu. *(Makofi)*

Mimi ninachotaka kukisema hapa katika sheria hii ambayo tunaizungumza leo, sijaona ni nani hasa anayewajibika kuhakikisha kwamba, anawazuia hawa wanyama au hata wanapoingia kuwafukuza ili wasiweze kuvamia wananchi, pamoja na mali zao. Sheria hii inamtaja *authorized officer* kwamba, kutakuwa na *authorized officer* wa wilaya, mkoa au kitaifa ndiyo anayewajibika na jukumu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamekuwa wakipata matatizo makubwa sana na hatujui tumwambie nani; ukienda kwa afisa wanyamapori anasema jukumu hili

linawahusu *game reserves*. Ukienda kwa *game reserves* wanasema jukumu hili linamhusu afisa wa wanyamapori!

Kwa hiyo, wananchi wetu wanapata tabu sana pale wanapokuwa wamevamiwa mazao yao yanaharibiwa, hata pengine kuuawa. Chui anavamia anakaa kwenye kijiji, anajeruhi watu, anaua watu kwa muda hata wa siku tatu, hakuna chombo chochote cha Serikali ambacho kimekuja kusaidia. *(Makofi)*

Halafu sasa wilaya yenyewe ambayo ndiyo inazungumzwa kwamba, inaweza kuokoa lile jehazi, kwa sababu lengo hasa sio wananchi hao kufikia kufidiwa baada ya kuuawa, lengo ni kuokoa kwanza maisha yao. Sasa afisa wa wanyamapori, ambaye anapewa jukumu zito sana la kuhakikisha kwamba analinda hawa wanyama wasivamie wananchi, amekuwa akilalamika sana, Wilaya yangu ya Meatu hakuna gari la kuwawezesha kuwafikia hao wanyama, hawana askari wa kutosha kwenda kushambulia wale wanyama. Kwa hiyo, wananchi hawa sasa wanabaki yatima, hawana wa kuwasaidia. *Contrary,* upande wa *game reserves* kuna magari ya kutosha, upande wa afisa wanyamapori hakuna magari, upande wa askari wa *game reserves* kuna askari wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii ina-*justify* kabisa kwamba, Serikali inaangalia zaidi mambo ya wanyamapori zaidi kuliko binadamu wenyewe, ambapo wanyamapori wapo kwa ajili ya binadamu. *(Makofi)*

Asilimia 25 ambazo zinatolewa kila mwaka, kwanza, zinatolewa kwa kusuasua wakati mwingine hazitolewi kabisa. Katika Wilaya yangu ya Meatu na sehemu nyingine za wilaya mbalimbali, mpaka sasa hivi hatujapokea hii asilimia 25. Sasa unakuwaje hivi sasa na shughuli za uhifadhi wakati uhifadhi hauko kwa ajili yako? Wananchi wangu wanapata mateso makubwa, wanashambuliwa mazao yao wanaambulia njaa kila mwaka. Wananchi wangu wa Semu, Mbuga ya Banya, Mwanindwa, Ming'ongwa, Butuli, Matale, Mwamashimba, Mwasengela, Nghanga na Mwamhago wanapata mateso makubwa bila msaada wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyozungumza wenzangu katika kifungu cha 12 (3) (a), (b) na vipengele vingine vya (4) mpaka (5), nawaomba sana na Wabunge wenzangu labda kama sisi hatujui kusoma, lakini kama kweli ndivyo hivyo sheria hii ambayo imempa mtu mmoja kutumia busara yake, kuwaua wenzake; kama Waziri hatafanya marekebisho katika Muswada huu basi tuukatae. Kama sheria hii itapita, aidha, kama Serikali imeamua kuwaua wananchi wake kwa risasi, basi ifanye hivyo, lakini sisi kama Wabunge hatuwezi tukakubaliana wananchi wauawe kwa risasi na maaskari wa *game reserve*. *(Makofi)*

Kama walivyozungumza Wabunge wenzangu hapa kwamba, ku-*commit an offence* hata kuingia tu kwenye *game reserve* ume-*commit offence*. Mheshimiwa Maige, alikuja jimboni kwangu Kisesa na nilimpeleka mpakani. Mpaka wa *game reserve* na wanapoishi wananchi. Mipaka hii imetenganishwa na tuta tu, kiasi kwamba, mwananchi huyo ambaye hata mbuzi amekimbilia kuingia kwenye *game reserve,* anakwenda kuwaswaga halafu anakimbia anapigwa risasi na sheria haisemi apigwe risasi sehemu

gani? Kwa hiyo, wananchi wetu sasa watakwenda kuuawa kikatili. Mwamuzi wa hapa ni mtu mmoja tu, ambaye anaitwa *authorized officer*, yaani atakavyofikiria yeye sawa basi anatwanga risasi, *then* anasema sheria Wabunge mliipitisha. Waheshimiwa Wabunge, kataeni Muswada huu kama marekebisho haya hayawezi kufanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani Waziri, pamoja na Naibu Waziri, wanafahamu vizuri sana maeneo ya wananchi wetu. Sioni sababu ya wao kujifanya hawajui mazingira ya wananchi ambao wanawawakilisha. Kwa sababu kama wangekuwa wanajua, wasingeleta Muswada kama huu wa kuwakabidhi wananchi wako kupigwa risasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu haujawatendea haki wafugaji hata kidogo. Wakati tunapewa ufafanuzi katika kifungu kile cha 17 katika kipengele cha (2), sheria inakataa kabisa kuchungia ndani ya *game reserve*. Katika kifungu cha 20, sheria inakataa kabisa kuchungia ndani ya *game controlled area* isipokuwa kwa idhini ya Mkurugenzi. Labda hapa niulize; kwa sababu wakati ule wanatueleza kwenye semina walituambia kwamba, wananchi wataruhusiwa kuchungia kwenye *game reserve* na kwenye *game controlled area*, pale panapotolewa kibali na Mkurugenzi. Sasa hivi kwa sheria hii ilivyokuja hapa, si hivyo ambavyo tumeelezwa kwenye Kamati, inazungumzia tu suala lile la *game controlled area*. Wananchi hawa wanaoishi kandokando mwa *game reserve*, hawajapewa hiyo haki ya kuchungia kwenye *game reserve* pale, hali ya hewa inapokuwa mbaya kwa maana ya ukame wa kutisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii katika kifungu cha 44, inamhurusu kabisa Mheshimiwa Waziri, kutenga maeneo kwa ajili ya uwindaji wa kiraia kwa maana ya wananchi kupata kitoweo. Hili nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Shamsa Mwangunga, kwa sababu ni kilio kikubwa ambacho niliwapigania Wananchi wa Jimbo langu na Watanzania kwa ujumla. Zipatikane sehemu wananchi hawa waweze kupata kitoweo.

Mheshimiwa Waziri, ningeomba kwamba, kama utayafanya marekebisho katika Muswada wako na Muswada huu tukiupitisha, basi nakuomba uanzie Kisesa kwenda kutangaza maeneo ya uwindaji wa kiraia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mfugaji katika Muswada huu kama nilivyotangulia kusema, hajatendewa haki. Tunatunga sheria wakati wananchi wetu tayari wanaishi tofauti sana na zamani sheria hizi zilitungwa wakati wananchi hawajafika mpakani. Kwa hiyo, unaweza ukaona tofauti; Bunge la akina Mzindakaya la mwaka 1965 wakati linatunga hizi sheria, lilipitisha sheria wakati ule wananchi walikuwa hawaishi kandokando mwa hifadhi, yaani hawajatenganishwa na tuta kulikuwa na *buffer zone* kubwa tu. Sasa hivi tunatunga sheria, wakati wananchi wanaishi kwa kutenganishwa na shughuli za uhifadhi na tuta tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeomba sana, Waziri aone umuhimu wa kutenga *buffer zone* katika maeneo ambayo yanatenganishwa na tuta. Ipatikane *buffer zone* wananchi watakuwa wanachungia maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyozungumza wenzangu wakati wanachangia, ukweli ni kwamba, sheria hii imempa adhabu kubwa sana mfugaji. Katika sheria nzima, hakuna faini ya *five million,* hata yule aliyechoma msitu hajatozwa *fine* hiyo. Hapa mfugaji ndiyo huyo anayetozwa *five million*. Ninashangaa sasa Naibu Waziri ametoka kwa wafugaji, naye Mwagunga Wagogo ni wafugaji; sijui kwa nini wafugaji katika Muswada huu wanaonewa hivyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningependekeza kwamba, *five million* iondoke iwe *five hundred* na hiyo miaka mitano ni miaka mingi sana kwa mfugaji, tuweke miaka miwili inatosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 95(4), kinampa mamlaka Mkurugenzi baada ya kuwasiliana na Waziri kwamba, wanaweza kuendesha mafunzo ya kujenga uwezo kwa maafisa wanyamapori. Bunge hili limekuwa likipitisha sheria ngumu, pamoja na hii Sheria ya Maliasili ni moja ya Sheria ngumu ambazo tunazipitisha. Wananchi hawa tunawatungia sheria, hatuwaandalii mazingira ya kufahamu nini tunachokitunga, ina maana kwamba tunaandaa sheria tu i tuwafunge na tuwatoze faini wananchi, kutumia ufahamu wao mdogo.

Ningeomba sana, sheria haijawekwa hapa mafunzo yametengwa kwa ajili ya wafanyakazi wa wanyamapori. Mimi naona vijiji vyote vinavyopakana na maeneo ya uhifadhi, zipate mafunzo. Wananchi waendeshewe mafunzo kupitia mikutano ya hadhara, waelezwe juu ya umuhimu wa uhifadhi, lakini pia na sheria ambazo zinatawala uhifadhi ili wananchi wawe na uelewa mkubwa juu ya shughuli nzima za uhifadhi, kuliko kuwasubiria kuwatungia sheria ili baadaye tuwafunge. Sheria zetu nyingi zina-*base* kumpa mamlaka yule anayekwenda kuhukumu au kusimamia, lakini mhukumiwa mtarajiwa, hafundishwi juu ya sheria zinazotawala. Sheria hizi zichapwe na ziandikwe kwa lugha rahisi, wagawiwe wananchi kule vijijini ili kuongeza ufahamu juu ya uhifadhi na Sheria zinazotawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokwisha kusema pale mwanzo, siwezi kuunga mkono Muswada huu mpaka yale marekebisho ya msingi yawe yamefanyika. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo; Kaimu Mkurugenzi wa Utawala na Utumishi, ameniomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Tafrija kwamba, baada ya kuahirishwa Shughuli za Bunge leo tarehe 2 Februari, 2009; Wajumbe hao wakutane kikao cha dharura na maalum, Jengo la Utawala, eneo la mapokezi. Waheshimiwa Wabunge, kanuni ya 28(5) inasema; iwapo shughuli zilizopangwa kwa siku hiyo zimemalizika kabla ya saa 1.45 usiku, Spika ataliahirisha Bunge bila kuhoji. Lakini iwapo zimesalia dakika kumi kabla ya kufikia muda wa kuahirishwa Kikao na Bunge au Kamati ya Bunge Zima au Kamati Matumizi, bado haijamaliza shughuli zake, Spika anaweza kuongeza muda usiozidi dakika 30 bila kulihoji Bunge au Kamati ya Bunge Zima au Kamati ya Matumizi ili kukamilisha shughuli zilizobaki.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa kanuni hiyo, ambayo nimeisoma, naona kwamba shughuli za leo kwa maana ya orodha ya wachangiaji ambayo ilikuwa Mezani kwangu imekamilika. Kama nilivyosema kwamba, Muswada huu tutaumaliza siku ya kesho; kwa hiyo, kwa mujibu wa Kanuni hiyo ya 28 kipengele cha (5), muda wetu wa kuahirisha Bunge haujafika, lakini nimepewa mamlaka ya kufanya hivyo.

Kwa hiyo, kwa kutumia kanuni hiyo, sasa naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi, ndani ya Ukumbi huu wa Bunge.

*(Saa 01.40 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,*
*Tarehe 3 Februari, 2009 Saa Tatu Asubuhi)*